

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tano – Tarehe 19 Juni, 2012**

*(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2011 (*The Annual Report of Energy and Water Utilities Regulatory Authority for the Year ended 30th June, 2011*).

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 35

**Tatizo la Maji Muhamwe**

**MHE. FELIX FRANCIS MKOSAMALI** aliuliza:-

Katika Kata za Kibondo Mjini, Mabamba, Busunzu, Rogongwe, Kizazi na Misezero kuna tatizo kubwa la maji.

- (a) Je, ni lini tatizo hilo litakwisha kwa kukarabati visima vyote vilivyoharibika katika Jimbo hilo?
- (b) Kwa nini kiasi cha shilingi 50,000,000/= zilizotengwa kwa ajili ya utafiti wa kisima kimoja Kibondo Mjini zisitumike kuchimba visima vinne (4)?
- (c) Je, ni lini mradi wa kuchimba visima kumi (10) Wilayaya Kidondo utakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhammadi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba baadhi ya miundombinu ya maji katika Halmashauri ya Kibondo imeharibika na inahitaji kufanyiwa ukarabati. Kwa kuzingatia hilo, Halmashauri katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilitumia jumla ya shillingi millioni 335.0 kwa ajili ya ukarabati wa visima vifupi vitano, visima virefu 25, miradi ya mserereko minne na miradi inayoendeshwa na mitambo mmoja. Aidha, katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, Halmashauri imetenga shillingi millioni 664.0 kwa ajili ya ukarabati wa visima vifupi 20, visima virefu 50, miradi ya mserereko minne na miradi ya kuendeshwa na mitambo mmoja. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa ukarabati unakamilika kwa wakati ili kuhakikisha huduma hiyo inatolewa kwa wananchi inavyokusudiwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali ilitenga shilingi milioni 50.0 kwa ajili ya utafiti wa upatikanaji wa majiardhi katika Kata ya Kibondo Mjini.

Fedha hizi hazikupatikana. Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa utafiti, fedha zinazotengwa kwa ajili ya utafiti haziwezi kubadilishwa matumizi kwa kuwa utafiti ndiyo hatua ya mwanzo muhimu ya uhakika wa upatikanaji wa majiardhi.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Halmashauri iliidhinishiwa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya utekelezajiwa ujenzi wa Miundombinu ya maji. Hatua iliyofikiwa ni kwamba Zabuni imetanazwa tarehe 06 Juni, 2012 kwa ajili ya kuwapata Wakandarasi watakaojenga mifumo hiyo katika Vijiji vya Kibindo, Minyinya, Nyabitaka, Muhamabwe na Nyagwijima. Aidha, Vijiji vilivyobaki vimetengewa shilingi bilioni 3.4 katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji na mifumo ambata.

**MHE. FELIX FRANCIS MKOSAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imekuwa inatoza fedha kwa watu waliounganishiwa mabomba bila mita yaani wanakadiria wanavyojisikia wakiamua kukupangia milioni ngapi ni wao, elfu hamsini ni wao. Sasa Serikali inatoa kauli gani juu ya hili kwamba mita zitaanza kufungwa lini ili watu hawa wasiendelee kutoza fedha jinsi wanavyotaka wao na kuendelea kuwaumiza wananchi?

Lakini swali la pili, nataka kujua kwamba Wabunge wengi tumekuwa tunauliza juu ya miradi hii ya visima kumi kwa nini Serikali isituletee ratiba kwamba visima hivi kumi vitakamilika kwa muda huu ili tuache kuuliza maswali ya namna hii ambayo yamekuwa yanaaulizwa na Wabunge wote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Felix Mkosamali, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ya maji iliyopo katika maeneo haya ambayo Mheshimiwa Felix Mkosamali anaizungumzia ina taratibu za kuunda kamati zake na ina taratibu za kuwa na kila kijiji kinawakilishwa katika hizo Kamati.

Ni kweli anachozungumza hapa anazungumzia habari ya mita na kama mita haipo pale wanachofanya ni kwamba wanafanya utaratibu wa *flat rate*. Sasa anachozungumza hapa ni huu utaratibu wa mita ambao ni utaratibu wa kisasa ambao unakuwa na uhakika kwa sababu utamtoza mtu maji kulingana na maji aliyoyatumia, *it makes a lot of sense to us*, wote sisi tunalona hiyo. *At this particular moment* kinachotokea pale ni hicho ni hicho anachokisema kwamba wana huo utaratibu wa *flat rate*, nitawasiliana na watu wako. Suala la metering ni suala la gharama na mambo mengine na utaratibu mzima uliowekwa pale.

Hili la pili analoliuza kwa sababu nilijua kwamba Mheshimiwa Mkosamali atakuja na maswali haya mimi hapa ninalo tangazo na ninataka nimwambie kabisa kwamba ninayo barua inayotoka Wizara ya Maji ambayo imeandikwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma inayomwarifu kuhusu hii miradi inayozungumzwa hapa na kwamba miradi hii sasa ifanyiwe kazi na zimetengwa 1.8 billion na utaratibu unafuatwa. Pia, ninayo orodha na tangazo lipo hapa linalotangaza ili wale *bidders* wanaotaka kuomba kazi hiyo waende wakafanye kazi.

Sasa ndugu yangu Mkosamali kama kuna tatizo lolote katika hilo ninalolisema baada ya kujibu maswali tukutane lakini mimi nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Kibondo na anaelewa ninachozungumza hapa sasa hivi. Inawezekana

kwa vile wewe unatoka huko unakotoka unajua zaidi kuliko mimi ninavyojua, tunaweza tuka *compare notice* lakini jambo hili linafanyiwa kazi wala usiwe na wasiwasi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na swali linalofuata nali linaulizwa na Mheshimiwa David Silinde.

Majibu ya nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji Profesa.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongezea juu ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ya vijiji kumi imekuwa na mlolongo wa hatua za utekelezaji ambao ni mrefu kidogo lakini hatua ambayo imefikiwa sasa na hii inahusu Wilaya 61 ni kwamba Wilaya hizi sasa zimepewa *no objection* na Benki ya Dunia kuanza kutekeleza miradi ya vijiji vitatu katika Wilaya hizo 61. Wilaya nyingine 16 zinangojea kupewa *no objection* wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika kipindi cha mwaka huu wa fedha unaokuja na tutatangaza hili kwenye bajeti, vijiji zaidi vitaongezewa katika orodha hiyo ya vijiji vitatu na utekelezaji wa vijiji hivyo nategemea kwamba utakuwa umekamilika katika Bajeti hii na Bajeti nyingine itakayofuata mwaka 2013/2014.

Na. 36

### **Kuungua kwa Masoko Mbozi Magharibi na Mbeya Mjini**

**MHE. DAVID ERNEST SILINDE** aliuliza:-

(a)Je, Serikali inafahamu sababu za kuungua kwa masoko ya Mbozi Magharibi na Mbeya Mjini?

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha hali hiyo haijirudii tena katika masoko hayo na maeneo mengine kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Jimbo la Mbozi Magharibi soko la Tunduma liliungua mnamo tarehe 28 Novemba, 2011 majira ya saa 11.00 jioni. Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, chanzo cha moto huo ni hitilafu ya umeme wa jenereta iliyokuwa inatumiwa na mfanyabiashara katika soko hilo wakati wa kuifanya majaribio. Moto huo ulisambaa na kuunguza vibanda vya biashara vilivyokuwa jirani. Aidha, masoko yaliyoungua Mbeya Mjini ni Soko la *SIDO*, Soko la Uhindini na Soko la Mwanjelwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio la kuungua kwa soko la *SIDO* lilitokea tarehe 16 Julai, 2011 kwa mujibu wa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, chanzo cha moto huo ni jiko la mkaa liliokua katika kibanda cha mama lishe kilichokuwa kimefungwa. Kwa upande wa tukio la moto katika soko la Uhindini chanzo ni moto ulioachwa na Mama lishe. Aidha, sababu za kuungua kwa soko la Mwanjelwa kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya ni pasi ya Mkaa iliyoachwa na Dobi ndani ya chumba ikiwa na mkaa, hivyo kutohana na upenpo mkali, moto huo ulisambaa na kuenea katika vibanda vya soko hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha hali hii haitokei kama ilivyotokea, hatua zifuatazo zinachukuliwa:-

Kujenga masoko ya kisasa yenye miundombinu ya barabara, kutoa elimu kwa wananchi hasa watumiaji wa masoko hayo kuhusu majanga ya moto na namna ya kukabiliana nayo, kuacha nafasi ya kutosha kati ya kibanda na kibanda, kuweka vifaa vya kubaini na kuzimia moto (*fire extinguisher*) kila kibanda zikiwemo ndoo zenye mchanga, kuweka vituo vya kuchukulia maji (*fire hydrants*) karibuna maeneo ya masoko, kuhakikisha magari manne (4) ya zimamoto ya Jiji la Mbeya yanakuwa imara na yanatumika ipasavyo kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya moto na kujenga matanki ya kuhifadhia maji ya akiba kwenye masoko yanayoendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuviiamarisha vikosi vya Zimamoto kwa kuvipatia magari ya zimamoto ili kukabiliana na majanga ya moto kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana.

**MHE. DAVID ERNEST SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyasikia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini ningependa mambo mawili ya ziada kupatiwa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dhana ambayo imejengeka kwa wananchi kwamba masoko hayo yanapokuwa yanaungua inasemekana Serikali inatumika kuwaunguzia wananchi masoko ili wahame katika hayo maeneo na mpaka sasa hakuna kauli yoyote ambayo Serikali imewahi kuitoa. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya tuhuma hizi?

Pili, katika Wilaya ya Mbozi tumekuwa na gari la kuzimia moto ambalo tulipatiwa na Serikali lakini gari hili tangu limefika halijawahi kufanya kazi ya kuzima moto na magari haya

yaligawiwa nchi nzima na yameshindwa kufanya kazi ya kuzima moto.

Je, ni kwa nini Serikali ilinunua magari ya zimamoto ambayo hayafanyi kazi?

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Serikali inachoma moto masoko.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya namna hii itakuwa ni Serikali ya ajabu sana, yaani Serikali ambayo inawajengea wananchi soko na barabara na hata hospitali, halafu Serikali hiyo tena ikatoka ikafanya hivyo.

Mheshimiwa Silinde mimi nataka niseme kwamba wakati nakuja hapa nimekuja hapa kwa sababu najua kwamba inawezekana mtu akafikiri vyovyote vile anavyotaka kufikiri. Si kweli hata kidogo, Serikali hii iliopo madarakani haiwezi hata siku moja ikafikiri kwamba leo ipeleke watu waende wakachome masoko kule. Mimi nilipokuwa naulizwa hapa kwamba ni nini kilichosababisha na Mheshimiwa Silinde nimekuja na barua hapa kwa sababu utataka ushahidi kwamba hii umeipata. Tumeitisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya tukawaambia moto huu umetokea hapa si kwamba nimechukua habari hii mtaani tu, habari hizi ni authentic na nimezungumza na *Regional Administrative Secretary* kumwuliza kuhusu habari hii ya moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba moto huu umetokana na ajali hizi nilizozitaja hapa na nakala ya majibu hayo inayotoka katika Kamati hiyo ninayoizungumza ninayo hapa.

Kwa hiyo, si kweli hata kidogo kwamba Serikali inawaambia watu waende wakafanye hivyo, haitafanya hivyo kwa sababu Serikali kwanza inapata mapato mle ndani, Serikali inawapenda watu wake, Serikali inawasomesha watu wake, Serikali hiyohiyo haiwezi kutoka tena hapa iseme hivi, nenda kachome moto kule. Mimi nataka tukae tushirikiane na wewe na kama una mahali popote ambapo unafikiri kwamba Serikali kwa namna moja ama nyingine imeshiriki katika mpango huo utuletee ushahidi.

Lakini ninachojuu mimi Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, haiwezi kufanya jambo la namna hiyo hata kidogo. (*Makof*)

Kwa hiyo, nataka nimdhibitishie rafiki yangu Silinde kwamba ni hivyo. (*Makof*)

Hili la pili, alilolizungumza yaani kuhusu gari la Zimamoto ni kweli, anachosema ni kwamba gari lile linapokwenda kule halina tenki la maji, ni magari haya ya kisasa ambayo unatakiwa uende ukali-*plug* kwenye *Water Hydrant*.

Sasa kwa Mwanjelwa na maeneo ya Mbozi kule tunavyozungumza hatuna hizo *gargets* kama anavyosema, *it is true* kabisa na gari hilli wala halitumiki kwa ajili ya kupeleka maji bali linatumika kwa ajili ya kufanya matangazo pale mjini.

Kwa hiyo, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge unachozungumza hapa, nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hii ya Mbozi, nimemwambia kwamba afanye mambo yafuatayo, ninyi mnafanya *priorities* ya magari matano pale yaani *ambulance* na magari mengine basi wekeni *priority* mojawapo muweke katika gari la zimamoto. Moto huu ulipotokea hapa waliagiza gari kutoka Mbeya kilomita 70 wanafika pale soko limeshaungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakiri hapa mbele yako kwamba sisi tutakwenda na kufuatilia jambo hili kuona kwamba tunapata gari ambalo litahakikisha kwamba moto ukitokea tutaweza kuuzima mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nawaona Waheshimiwa Wabunge wa Mbeya, Mheshimiwa Kamishna Zambi kubali tu tumwachie tu dada yako Mheshimiwa Mary Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa, wakazi wengi wa Tunduma na Mbeya Mjini ni wafanyabiashara wa maeneo haya ya masoko. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuwalipa kifuta jasho wahanga hawa kama ilivyokuwa kwa wahanga wa mabomu ya Mbagala? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usiwe na wasiwasi na sauti yangu hii, ni msisitizo tu. Niseme hili la Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwamba ukifanya hivyo uta-set precedence hapa ambayo sisi wote hatutaweza kuibeba, ukitokea Mwanza Serikali itafidia, ukitokea moto Dodoma Serikali itafidia.

Ni kweli kabisa naiona *concern* ya Mheshimiwa Mbunge kwamba kweli watu wamepoteza mali pale, lakini ni ajali kama tulivyoeleza hapa.

Sasa kama Halmashauri yenyewe itafika mahali kutokana na mapato yake ya ndani ikaona kwamba ina uwezo wa namna hiyo sasa hili ni jambo ambalo tuta-debate lakini ki-

*policy* mimi sioni mahali ambapo ninaweza ninaweza nikajibu nikasema ni sawasawa tutakwenda kuwafidia wananchi.

Hatuna utaratibu wowote na tunasikitika kwamba ajali hizi zinatokea lakini tunachoweza kusema hapa ni kutoa rai kwa wananchi wetu na viongozi wetu kule mliko kuweza kuchukua tahadhari za kutosha kuhakikisha kwamba mioto hii inapotokea pale hatupotezi mali kama Mheshimiwa Silinde alivyokuwa anaeleza hapa ili hali hii isijiendeleze tena. Lakini kwamba naweza nikatoa tamko kwa niaba ya Serikali hapa kwamba tutakwenda kuwafidia wananchi ambao wamepata hayo majanga, haipo na sifahamu mahali ipo, *I sent to be corrected* na kuelimishwa zaidi katika hili. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, tunasonga mbele na swali linalofuata ni Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba, Mbunge wa Dole.

Na. 37

### **Uwiano mzuri wa Wanyamaporini na Hifadhi za Taifa**

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA** aliuliza:-

Tanzania kama Taifa tunajivunia Maliasili nyingi na urithi tulionao, lakini pamoja na ukweli huo:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba uwepo wa makundi makubwa ya wanyamaporini katika hifadhi zetu unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira katika hifadhi hizo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uwiano mzuri wa Wanyamaporini na hifadhi zetu za Taifa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa huu ni muda muafaka wa kuanzisha viwanda vyataga kusindika nyama zitokanazo na

wanyapori ili kuvuna wanyama hao na kupunguza uharibifu na hata kuhamasisha wawekezaji wa nje kama ilivyofanya kwenye minofu ya Samaki?

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi yetu imejaliwa kuwa na urithi wa maliasili nyingi na ni dhahiri kwamba kuna makundi makubwa sana ya wanyamaporii katika hifadhi zetu. Hata hivyo, mfumo wa kiikolojia ambapo wanyamaporii hao huishi unajiedhesha kwa namna ambayo raslimali zilizopo ndani ya mfumo huu zinaishi katika uwiano wa kutegemeana katika maisha yao.

Kwa mfano; baadhi ya wanyama wanakufa kwa kuliwa na wanyama wengine (*food chain/web*) na kufanya mzunguko wa mfumo wa ikolojia kukamilika bila kusababisha madhara kwenye mazingira. Mapori ya Akiba mengi yamepakana na Hifadhi za Taifa na katika Mapori ya Akiba kuna vitalu vya uwindaji wa kitalii, ambavyo hupatiwa mgawo wa kuwinda kulingana na taarifa za sensa ya wanyamaporii na hivyo kutokuathiri mfumo mzima wa kiikolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Serikali inahakikisha kuwa kuna uwiano mzuri kwa kutoa matumizi endelevu ya uwindaji wa kitalii na ule wenyiji. Hii ni pamoja na utoaji wa vibali vya kuvuna mamba katika sehemu ambazo wanyama hawa

wameongezeka na wanaweza kuleta madhara kwa wananchi. Shughuli zote hizi zinalenga kuhakikisha kuwa hakuna uwezekano wa makundi haya kusababisha uharibifu wa mazingira.

- (b) Serikali imekuwa ikifanya sensa za wanyamapor kila baada ya miaka mitatu na hivyo kupata taarifa za uwiano wa wanyamapor katika hifadhi. Taarifa hizo ndizo zinazotumika katika kutoa mgao na kudhibiti uwindaji wa aina za wanyamapor ambao itaonekana wamepungua sana.
- (c) Kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha viwanda kwa ajili ya kusindika nyama zitokanazo na wanyamapor kwa kuwa wanyama hawajazidi kupita kiasi ambacho ikolojia ya sasa imeshindwa kumudu, na kuanzishwa kwa viwanda vya kusindika nyama zitokanazo na wanyamapor kutachochaea kuongezeka kwa vitendo vya ujangili dhidi ya wanyamapor.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa, Serikali imekiri kwamba inatoa vibali kwa ajili ya vitalu vya uwindaji ili kuweka uwiano wa wanyama katika hifadhi zetu. Je, vitalu vya uwindaji vimechangia kiasi gani katika pato la taifa?

(ii) Kwa kuwa, ni kweli kwamba wanyama hutoka katika hifadhi na kuingia katika maeneo ya wananchi na kusababisha usumbufu na hasa uharibifu wa mazao yao. Je, Serikali ina mpango gani katika kufidia hasara ambazo wananchi wanazipata?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu; kwanza vitalu ni sehemu ya uwindaji wa kitalii na uwindaji wa kitalii umeendelea kuongezeka katika nchi yetu. Tutakuwa tayari kuangalia *data* na *statistics* tulizonazo ili niweze kumletea Mheshimiwa Mbunge hapa asilimia kamiri ya changizo katika ukuaji wa pato la Taifa unaotokana na ile sekta ndogo ya uwindaji wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Serikali imeendelea kufanya juhudzi za kila namna kuhakikisha kwamba, kwanza tuna-control na tunapunguza athari au madhara yanayoweza kutokana na wanyama waharibifu kwa mazao ya wananchi au kuvamia na kuumiza wananchi kutokana na kwanza doria tunazozifanya, na pili kutokana na kushiriki sisi na wananchi kuhakikisha wanafahamu na wanaendelea kuwa na uhifadhi shirikishi katika maeneo yanayohusika.

Hili jambo tunafanya sisi pamoja na wananchi katika maeneo yote ambayo yanapakana na hifadhi, maeneo yote ambayo yanapakana na WMAs na maeneo yote ambayo yanapakana na Mapori ya akiba.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza, sasa twenda Mbuga za Katavi, Mheshimiwa Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, yemekuwepo mabadiliko ya tabia ya nchi na ukame na hifadhi ya Katavi inategemea chanzo cha Mto Katuma peke yake; na kwa kuwa ina idadi kubwa sana ya Viboko na wengi hufa.

Je, sasa Serikali kupitia Shirika la TANAPA watakuwa tayari kujenga mabwawa ili kunusuru Viboko katika Hifadhi ya Katavi?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, swali muhimu sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inafahamu umuhimu wa Mto Katuma katika *eco-system* ya eneo zima la Katavi. Vilevile, *survival* ya Viboko na wanyama wengine nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba, inatokana na umuhimu wa mto huu kuendelea kuwa na maji.

Vilevile nakiri kwamba kutokana na tabianchi ambayo imeendelea kubadilika, maji katika mito yetu yameendelea kupungua na hali kadhalika mvua. Tunaendelea kufanya mazungumzo na *TANAPA* kwa kuangalia moja, juu ya *plans* zilizopo za hifadhi zetu ikiwa ni pamoja na Katavi kuona kama kuna mahali ambapo italazimika kabisa kuweka mabwawa ya kutengenezwa na Wanadamu hatutasita kufanya hivyo.

Na. 38

### **Migogoro iliyoko Kandokando ya Pori la Akiba la Maswa**

**MHE. ALLY SALUM AHMED (K.n.y. MHE. LUHAGA JOELSON MPINA)** aliuliza:-

Kutokana na migogoro iliyodumu kwa zaidi ya miaka saba kati ya wananchi waishio kandokando ya Pori la Akiba la Maswa (*Maswa Game Reserve*) Wahifadhi wa pori hilo, matukio mbalimbali kama mauaji, kubakwa, kubambikizwa kesi, majeruhi, kutekwa, ng'ombe kupigwa risasi au kupotea, kulipa faini bila risiti, viongozi kupigwa, kuwekwa mahabusu na kushtakiwa nje ya Wilaya yamekuwa yakiripotiwa:-

- (a) Je, Serikali inafahamu uwepo wa matatizo hayo?
- (b) Je, ni wananchi na askari wangapi wameuawa kuanzia mwaka 2005 hadi sasa?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kutatua migogoro hiyo?

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mbunge wa Kisesa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukiri kuwepo kwa hali tete na isiyoridhisha kuhusiana na mwenendo wa migogoro iliyodumu kwa muda sasa katika Pori la Akiba la Maswa. Aidha, tuhuma zinazotokana na migogoro kati ya Wananchi na Wahifadhi wanaoishi katika eneo husika kama ilivyoanishwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kisesa, Luhaga J. Mpina ni za kusikitisha. Kuanzia mwaka 2005 hadi sasa Serikali ina taarifa ya kutokea mauaji ya wananchi watatu (3) na askari wa wanyamapori watatu (3) katika Pori la Akiba la Maswa. Nachukua nafasi hii kutoa pole na kutuma salamu za rambirambi kwa familia za wafiliwa popote pale walipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya mauaji kwa raia ama raia kuua wahifadhi, vitendo vya ubakaji, kubambikiziwa kesi, majeruhi, vitendo vya kutekwa, ng'ombe kupigwa risasi, kudhalilishwa kwa viongozi wa wananchi kwa kupigwa, vyote hivi ni vitendo vya kusikitisha sana na Serikali haiko tayari kuona wananchi wa hifadhi au Watalii wawindaji wakinyanyasika katika kufanya shughuli zao kwa hali ya hofu na mashaka juu ya usalama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na unyeti wa tuhuma alizozitoa Mheshimiwa Mpina hapa na ukweli kwamba, Serikali inataka haki itendeke kwa wote nimeazimia kuunda Tume huru ya uchunguzi dhidi ya tuhuma hizo. Tume hiyo ifanye kazi kwa siku thelathini (30) na kuwasilisha taarifa yake kwa ajili ya hatua zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho Wizara inamshukuru sana Mheshimiwa Mpina pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo ya jirani na Pori la Akiba la Maswa, kwa kuwa karibu na wananchi na kwa kuhakikisha kwamba uhifadhi endelevu unatoa mchango wa kimaendeleo kwa wananchi wa maeneo husika na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

**MHE. ALLY SALUM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Lakini ikumbukwe kwamba hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye jimbo la Kisesa aliahidi kuunda Tume hivi hivi kwa masuala hayahaya, lakini sina hakika kabisa kwamba Tume hiyo imeanza kazi au aliishachukua hatua zipi.

Mheshimiwa Naibu Waziri anasema hivyo hivyo. Sasa naomba aniambie Tume hii itaundwa lini na itafanya kazi lini kwenda kuokoa maisha ya wananchi wa jimbo la Kisesa kama alivyoahidi?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katika jibu lake alianisha, nakuomba urudie tena Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika jibu letu la msingi tumeamua kuunda Tume na hii inaundwa mara moja.

Hii Tume hii itafanya kazi kwa siku thelathini (30), italeta taarifa yake na tutachukua hatua zinazohusika mara moja na Waheshimiwa Wabunge wa maeneo yote ya Maswa tutawajulisha hatua zote ikiwa ni pamoja na Ripoti ya Tume huru ambayo tunaiunda mara moja kuanzia sasa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Naona swali hili tuendelee kulibakiza Maswa, Mheshimiwa Opulukwa, swali la nyongeza.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo la *Maswa Game Reserve* linafanana sana matatizo yanayotokea maeneo yanayozunguka WMA ya Makao huko huko Meatu; na kwa kuwa, matatizo yanayotokea WMA yamechangiwa kwa kiasi kikubwa sana na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya aliyehamishiwa Wilaya la Momba, Mheshimiwa Yudi Saudea ambaye alihongwa gari aina ya GX T. 147 ASX ili kuweza kum-*facilitate* mwekezaji ambaye ni *Mwiba Holdings* ili kuweza kuwahamisha watu na kuwanyang'anya maeneo yao akishirikiana na *OCD* wake. (*Makof!*)

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari katika Tume hiyo pia kuwachunguza hao watu wawili niliowataja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza nirudie tu kwamba Kanuni zetu zinakataza kuwataja majina na kuwashirikisha ndani ya Bunge hili watu ambao hawawezi kujitetea.

Lakini pili, kwa utawala Bora tu Mheshimiwa Waziri Mkuu angependa kupata vielelezo na ushahidi wa tuhuma hiso kwa sababu kama ni kweli Mkuu wa Wilaya anaweza akahongwa hata sisi Serikali hatupendi ahongwe.

(*Hapa Baadhi ya Wabunge walizomea*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naombauzuie hii tabia mbaya ya kuzomea. Hivi hamwezi kusikiliza nyie CHADEMA?

**WABUNGE FULANI:** Hatuwezi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE):** Eeh!

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, naomba utulivu wenu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema ni hivi, hata sisi Serikali hatuwezi kuvumilia kuwa na Mkuu wa Wilaya anayehongwa, hilo siyo jema mpaka mnazomea? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba tu Mheshimiwa Mbunge akabidhi kitichako vielelezo ili Serikali iweze kuchukua hatua. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Kanuni zetu ziko wazi kuhusu kuwa makini sana na kuwataja watu wenye heshima zao kwa majina na kuwahusisha na mambo ambayo ni ya uvunjifu mkubwa sana wa maadili katika uendeshaji wa nchi.

Kwa hiyo, katika jambo hili halihitaji Tume kwa vile Mheshimiwa aliyeongea ameongea kwa uhakika kwamba, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya alihongwa gari na namba yake ameitaja akishirikiana na *OCD*. Kwa hiyo, *ruling* yangu nakutaka Mheshimiwa Opulukwa katika muda wa siku saba (7) uwe umeishatuletea ofsiini vielelezo vinavyothibitisha... (*Makofî*)

Naomba wanaopiga makofi wasubiri kidogo tuelewane, vielelezo vinavyothibitisha jambo hilo kuhusiana na kiongozi huyo wa Serikali kuwa amehongwa gari.

### **Fidia Kwa Waliopisha Mradi wa EPZ – BUNDA**

**MHE. ESTHER A. BULAYA** aliuliza:-

Baadhi ya wananchi katika kijiji cha Tairo, Jimbo la Bunda wamelipwa fidia kupisha utekelezaji wa Mradi wa *EPZ*, lakini wengine mpaka sasa hawajalipwa.

Je, ni lini Serikali itawalipa wananchi waliobaki kwa kutumia sheria ya malipo ya sasa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali hili kuitia kwako ningeomba nitoe ufanuzi ufuatao:-

Ningependa Bunge lako Tukufu lielewe kwamba *Export Processing Zone (EPZ)* ipo kwa ajili ya sisi wote. Serikali kuitia Wizara ya Viwanda na Biashara na vilevile Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji hapa nchini, imetenga na inaendelea kutenga maeneo ya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuza nje ya nchi. Mamlaka hii imetoa fursa kwa mikoa yote nchini.

Kwa hiyo, nawatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba wasifikirie kwamba mbona kwenye hotuba ya Bajeti maeneo yao ambayo wanatoka hayajatajwa. Nataka ieleweke wazi kwamba, fursa ipo kuitia mamlaka hii ambayo nimeitaja ya *EPZ* kwamba kila mkoa utapata fursa hii. *EPZ* imeishaanza, mikoa yote itaenea. Si kweli kwamba *EPZ* ipo Bagamoyo, Kigoma wala Dar es Salaam.

Utaratibu unaendelea kupitia mamlaka hii mikoa yote itaenea. Ninasema hivi kwa sababu ya hili swali ambalo liko mbele yangu ambalo linatoka Bunda. Bunda kwa bahati nzuri imekuwa Wilaya ya Kwanza, au Mkoa wa Mara kupitia Bunda limekuwa na eneo la kwanza kwa *EPZ* kuweza kutenga maeneo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2007 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (*EPZ*) na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ilitenga eneo la hekta 2,316 katika kijiji cha Tairo - Bunda, ikijumuisha vitongoji vya Kirumi, Mabatini na Bushigwamara kwa ajili ya uwekezaji wa *EPZ* na *Special Economic Zone (SEZ)*.

Mamlaka ilikamilisha uthamanishaji wa mali katika maeneo hayo ambapo jumla ya shilingi bilioni 3.4 zilihitajika ili kulipa fidia kwa wananchi wanaomiliki maeneo hayo.

Kutokana na kiasi cha fidia kuwa kikubwa, Mamlaka ya *EPZ* kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara, walikubaliana kupunguza vitongoji viwili kati ya vitatu vya awali, hivyo kubakiwa na kitongoji cha Kirumi tu. Jumla ya fidia kwa kitongoji hiki cha Kirumi ilikuwa ni shilingi 2,142,852,910 na wahusika wa fidia walikuwa 280. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya fidia yalilipwa katika awamu mbili na yalifanyika kupitia akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda. Mwaka 2009, jumla ya shilingi bilioni moja zililipwa kama awamu ya kwanza ya malipo hayo kwa hundi toka *Export Processing Zone Authority (EPZA)* namba 814534 na awamu ya pili ya malipo ya shilingi 100,000,000 ililipwa mwaka 2010 kwa hundi toka *EPZA* namba 6064316.

Hadi sasa katika awamu hizo mbili, jumla ya watu 116,000 wameshalipwa fidia yao. Fedha iliyobaki (shilingi bilioni 1,042,852,910) tayari imeshatengwa na Hazina na inatarajiwa kulipwa mwezi Julai, 2012 kwa wahusika 164 waliobakia ili kukamilisha idadi ya watu 280 waliostahili kulipwa.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nashukuru kwa watu ambao tayari wameshaanza kulipwa 116,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mchakato huu ulianza muda mrefu na tathmini ilishafanywa tangu mwaka 2007 na kama tunavyoju siku zinavyozidi kwenda thamani ya ardhi na yenyewe inakua na wananchi wale wamesitisha kuendeleza maeneo yao kwa muda mrefu. Je, Serikali hao waliobakia watalipwa kwa thamani ya ardhi ya sasa au kwa ile thamani ya tathmini iliyofanywa ya mwaka 2007?

Swali langu la pili, kwa sababu kwenye Bunge hili hili ahadi ya kuwalipa wananchi wa Bunda kitongoji cha Tairo ilishatolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Sababu zilitotolewa za kutokuwalipa kuanzia mwaka jana mwezi Desemba ilikuwa ni kutokana na Bajeti ndogo. Mheshimiwa Naibu Waziri ameendelea kutoa ahadi kwamba wananchi wale watalipwa. Swalilangu. Je, wasipolipwa Serikali itakuwa tayari kusitisha mradi huu mpaka watakapojandaa ndio waanze tena kufanya tathmini upya ya kuwalipa wananchi hao. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali. Vilevile niwapongeze Wabunge wote wa Mkoa wa Mara hususan wale wanaotoka Bunda akiwemo Mzee wangu Wassira pamoja na Mbunge wa Mwibara Lugola kwa kufuatilia jambo hili sana.

Mheshimiwa Wassira analifuatilia sana na amekuwa akiandikiana na EPZ mara kwa mara kuhusu suala hili. Kwa hiyo kwa ujumla wao Wabunge wa Mkoa wa Mara nawashukuru sana kwa ufuatiliaji wa jambo hili. Kwanza nianze na ile ahadi ambayo anataka nimhakikishie kwamba imekuwa ni muda mrefu ni maneno tu lakini watu hawalipwi.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha ya kuwafidia hawa ambao wamebaki haina tatizo. Hazina tayari wameshatupatia fedha mwezi huu wa Juni na ndio maana nisema kwamba ifikapo Julai wote watalipwa. Si mpango kwamba itakuwa kwenye bajeti hii ambayo tunaiongelea sasa 2012/13 hapana. Hii bajeti inahusisha bajeti ya mwaka 2011/2012 ambayo fedha yake tumeshapokea na watalipwa kama nilivyosema na isitoshe kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba muda umeshapita sana na thamani ya ardhi inabadilika je itakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari sisi tumeshachukua hatua kwamba watakaolipwa katika awamu ya sasa watalipwa riba stahiki kwa mujibu wa Sheria namba 5 ya Ardhi ya Vijiji ya Mwaka 1999 na kanuni zake za Ardhi na Vijiji ya Mwaka 2002 kanuni namba 19 kipengele cha 1 mpaka cha 3 watu walipwa kwa mujibu stahiki hiyo. Na wale ambao nimesema kwamba walikuwa nao vitongoji vile ambavyo vilibaki vilikuwa 3 kimoja ndio vikapitishwa, viwili havikupitishwa nao hao tunasema kwa mujibu wa tathmini ambayo imefanyika na Mtathmini Mkuu wa Serikali nao watalipwa usumbufu.

Na. 40

### **Hitaji la Mawasiliano ya Simu Kilombero**

**MHE. ABDUL R. MTEKETA** aliuliza:-

Je, ni lini maeneo ya Masagati na Uchindile Jimboni Kilombero yatapata minara ya simu kwa ajili ya mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolijia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweka utaratibu mpya wa kuharakisha upelekaji wa mawasiliano katika maeneo ambayo hayana mawasiliano nchini. Gharama za kupeleka mawasiliano katika kila eneo la nchi yetu inatathminiwa. Mwezi Septemba mwaka huu, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCAF) unatarajiwala kutangaza zabuni za ujenzi wa minara katika maeneo mbalimbali yasiyokuwa na mawasiliano. Kama kila kitu kitaenda kama tulivyopanga, ujenzi wa minara katika maeneo ya Tanganyika Masagati na Uchindile Wilayani Kilombero unaweza kuanza kabla ya mwisho wa mwaka huu. (*Makofii*)

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kutokana na majibu mazuri ya Naibu Waziri kwamba tatizo la Tanganyika Masagai ni tatizo la miaka mingi na niliwahi kuzungumza hapa Bungeni kwamba wananchi hao wametupwa kabisa ina maana kwamba hamna mawasiliano ya aina yoyote hususan upande wa barabara na simu. Kwa hivyo, wametupwa hawawasiliani na watu wengine. Sasa Serikali napenda ihakikishie kwa sababu hili suala nimeshalileta hapa mara nyingi maana uhakika kweli wawaambie wananchi wa Kilombero kwamba, je, Desemba hii watapata mnara?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba

Jiografia ya Uchindile, Tanganyika Masagati ni ngumu. Ukitaka kutoka Ifakara kwenda Uchindile lazima uende Mikumi, Iringa, Njombe ndio uende Uchindile. Kwa hiyo tunafahamu kwamba wanahitaji mawasiliano kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niseme kwamba msingi wa Mfuko wa *UCAF* ni kutoa ruzuku kwa Makampuni ya Simu kupeleka mawasiliano katika maeneo ambayo hayana mvuto wa kibashara au yamechelewa kupelekewa mawasiliano. Mwaka jana tuliweka utaratibu wa kutangaza zabuni katika maeneo 140 nchini ambayo ingeweza kutusaidia kujua gharama halisi za kupeleka mawasiliano na kutoa ruzuku iliyo sahihi. Bahati mbaya zabuni ile haikufanikiwa kwa sababu tulipanga kutumia dola 4,000,000 lakini mzabuni aliyejitokeza mmoja alitoa zabuni ya dola milioni 6 kwa hiyo hatukuweza kufanikiwa. Tumeajiri Mshauri atusaidie kwenda kila kijiji cha nchi hii kwa sababu Waheshimiwa Wabunge waliorodhesha maeneo ambayo hayana mawasiliano na jumla vijiji vilifika ilikuwa ni vijiji 2,175. Tunachofanya sasa na jana tulikuwa na mkutano kati ya Mfuko na Serikali na wenyewe Makampuni ya Simu ili kujua gharama halisi ya kupeleka mnara kwenye kila kijiji kisichokuwa na mnara nchini. Zoezi hili nadhani litaisha mwezi Agosti mwezi Septemba tutatangaza zabuni mpya na utaratibu mpya wa ruzuku ambao utazingatia gharama halisi.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba kuanzia mwezi Septemba na bahati nzuri tumepata fedha shilingi bilioni 45 kutoka Benki ya Dunia kwa hiyo fedha zipo na tunahitaji tuzitumie kabla ya mwezi Februari 2014. Tunaamini kwamba tutatekeleza ahadi hii na kuanzia mwezi Septemba tenda zitatoka Makampuni yatatoa zabuni na yataanza kujenga kabla ya mwisho wa mwaka huu.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nipongeze majibu mazuri ya Naibu Waziri na kwa kauli yake nilituma maombi kwa ajili ya mawasiliano Kata ya Kidaru, Twike pamoja na Hurugu na Mtekente kwa upande

mwingine tangu Bunge la Novemba, 2011 na wataalamu wakawa wametupa fomu za kusaini. Kwa kauli hii ningemwomba Naibu Waziri anithibitishie. Je, kwenye vile vijiji vya mwanzo vitakavyoanza ambavyo vinategemea kupata mawasiliano kama mambo yameenda vizuri kabla ya mwisho wa mwaka huu je na vijiji vyangu hivyo vitakuwa mionganini mwao?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nchomba kwa suala ambalo ni *concise and precise*.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana katika vijiji 2,175 ambavyo vimeorodheshwa kwamba havina mawasiliano kabisa au havina mawasiliano ya kuridhisha vijiji vya Jimbo la Mheshimiwa Nchomba vimo, vijiji ambavyo zabuni zitatoka kwa ajili ya kupatiwa mawasiliano na wenyewe vitakuwemo.

Kwa hiyo, napenda kumuahidi Mheshimiwa Nchomba na wananchi wa Jimbo lake kwamba tutawasaidia wapate mawasiliano na wenyewe wawe sehemu ya ustaarabu wa Tanzania kama maeneo mengine.

**MHE. SULEIMAN M. N. SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Jimbo la Kishapu pla ni mionganini mwa majimbo yenyeye matatizo makubwa ya mawasiliano na ukizingatia kinamama wengi wanapotaka kujifungua katika maeneo ya Kata ya Lagana, Mwamalasa, Bunambiu na Somageji wanakosa mawasiliano hata ya kuita *ambulance*.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kuwaagiza vijana wakafanye tathmini ili uingize hayo mambo katika Bajeti yako na wananchi wangu wanufaikeni na mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya vijiji

ambavyo havina mawasiliano ilitokana na mambo muhimu mawili. Kwanza ni kwa Waheshimiwa Wabunge wenyewe kuorodhesha maeneo katika majimbo yao ambayo hayana mawasiliano.

Nakumbuka mwaka jana watu wa *UCAF* walikuja kwa ajili ya zoezi hilo. Kwa hiyo, naamini kwamba Mheshimiwa Mchambi aliorodhesha vijiji katika majimbo yake.

Lakini vilevile hata sisi Serikali kuitia Mfuko wa *UCAF* na sisi tumefanya tathmini yetu kujua maeneo ambayo hayana mawasiliano na kwa kuwa maeneo aliyoyataka katika jimbo lake hayana mawasiliano nataka kumhakikishia kwamba yatakuwa sehemu ya mpango huu ambao tunaupanga kuutekeleza.

Na. 41

### **Matatizo ya Mawasiliano ya Simu – Liwale**

**MHE. FAITH M. MITAMBO** aliuliza:-

Tatizo la mawasiliano ya simu Liwale limekuwa ni la muda mrefu sana licha ya kwamba katika mpango wa mawasiliano kwa wote *UCAF* Wilaya ya Liwale ilipangiwa minara tisa (9):-

- (a) Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa mpango huo na wananchi wategemee lini miradi hiyo itaanza kufanya kazi?
- (b) Je, ni Kampuni gani imepangiwa minara hiyo tisa (9)?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faith Mitambo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inatambua kwamba maeneo mengi ya Wilaya ya Liwale hayana mawasiliano ya simu za mikononi. Maeneo tisa yamebainishwa katika maeneo yenyé mahitaji ya mawasiliano katika Wilaya hiyo.

Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*) ilitangaza zabuni za miradi ya awali ambayo, licha ya kufanikisha kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo vile vile ilisaidia Serikali kupata taarifa za gharama halisi za kupeleka mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini. Hata hivyo, zabuni hiyo haikufanikiwa kwa sababu mzabuni mmoja aliyejitokeza alikuwa na mahitaji makubwa ya fedha kuliko fedha iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali inapitia utaratibu mzima wa kupeleka mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini kwa nia ya kuharakisha zoezi hili. Tumebainisha vijiji 2,175 nchini ambavyo havina mawasiliano. Ndani ya wiki nne kuanzia sasa tutajua gharama halisi za kupeleka mawasiliano katika vijiji vyote vya nchi hii katika maeneo yote ya nchi hii ambayo hayana mawasiliano.

Jana tu tarehe 18 Juni, 2012 tulikuwa na Mkutano wa Mafanikio kati ya Mfuko wa Mawasiliano (*UCAF*), Serikali na wenye Makampuni ya Simu kuhusu kukubaliana juu ya utaratibu mpya wa kuongeza kasi ya kupeleka mawasiliano vijijini.

Tumepata fedha, tayari kama nilivyosema takribani kama shilingi bilioni 45 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya shughuli hii

na mwezi Septemba tutafungua zabuni mpya zitakazokuwa ndani ya utaratibu mpya ambao tumeutengeneza.

Tunaamini kwamba kila kitu kikienda sawa kabla ya mwisho wa mwaka huu minara mingi itaanza kujengwa nchini ikiwemo katika maeneo ya Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Mitambo alitaka kujua ni Kampuni gani imepangiwa kujenga minara hiyo 9. Ifikapo mwezi Oktoba, mwaka huu Serikali itakuwa katika nafasi nzuri ya kueleza kwamba ni Kampuni gani imepangiwa kujenga minara katika maeneo ya Wilaya ya Liwale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mitambo kwa juhudzi zake zilizowezesha kampuni ya *Airtel* kupangakujenga mnara katika eneo la Lilombe Wilayani Liwale. Nampongeza pia kwa kuwajali wananchi wake na kuisukuma Serikali ya CCM kutekeleza ahadi yake ya kupeleka mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa mradi huu wa *UCAF* tangu uanzishwe umechukua muda mrefu bado Serikali iko kwenye *logistics* na kwa kuwe Serikali tayari imeshapata shilingi bilioni 45 kutoka Mfuko wa Benki ya Dunia. Na kuwa fedha hizi haziwezi kutosheleza kujenga minara kwa ajili ya vijiji 2175.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuanza kujenga minara hii kwa awamu Tanzania nzima ikiwemo Wilaya ya Liwale?

Kwa kuwa Kampuni ya *Airtel* iliahidi kujenga minara minne Wilayani Liwale katika kijiji cha Lilombe, Makata, Barikiwa na

Likombola. Na kwa kuwa tangu umeahidi mpaka sasa hivi ni miaka miwili.

Je, Mheshimiwa Waziri unanisaidiaje kwa hili ili wananchi hawa waweze kupata hii minara minne ambayo tayari *Airtel* ilishakubali kujengewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwa na fikra mbalimbali kuhusu utaratibu sahihi zaidi wa kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano. Ni muhimu kutambua kwamba upelekaji mawasiliano ni shughuli ya kibiashara.

Haya Makampuni binafsi yanafanya uamuzi wa kibiashara kuhusu kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ambayo wanadhani watafanya biashara. Serikali ilianzisha Mfuko huu makusudi ili kutoa ruzuku ya kurahisisha Makampuni haya yapeleke mawasiliano kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano.

Serikali ilifanikiwa kupata kama alivyosema Mheshimiwa Mitambo na kama nilivyosema awali shilingi bilioni 45 kwa ajili ya shughuli hii. Kikubwa ilikuwa ni utaratibu. Tumekuwa na majadiliano ya muda mrefu kwa sababu lazima kujadiliana na Makampuni binafsi kuhusu utaratibu rahisi zaidi.

Tunaamini kwamba utaratibu wa kutambua kila kijiji na gharama halisi ya kupeleka mnara kwenye kijiji hicho ni utaratibu mzuri zaidi. Kwa hiyo, tenda zitakazotoka zitatoka kwa msingi huo na Makampuni yatahimizwa kuchagua vijiji ambavyo tayari yana minara katika maeneo yanayozunguka. Kwa hiyo, tunaamini kwamba tumechelewa kuanza kwa sababu na kuweka utaratibu kumechukua muda mrefu.

Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mitambo kwamba chanzo cha fedha za *UCAF* sio fedha hizi za Benki ya Dunia peke yake. Kwamba kila mwaka Makampuni ya Simu yanachangia asilimia 0.3 ya mapato yao. Mwaka jana Makampuni haya yalipata jumla ya shilingi Trillioni 1.6, kwa hiyo tunazo shilingi bilioni 4.8 nje ya hizi za Benki ya Dunia.

Kwa hiyo, tutaendelea kujenga kwa awamu pamoja na kwamba hizi fedha bilioni 45 zinaweza zisitoshe. Lakini kila mwaka tutakuwa tunapata fedha naamini kwamba Serikali itakuwa inapanga Bajeti kwa ajili ya kujenga minara.

Kuhusu minara ya *Airtel* katika maeneo ambayo ameyataja, jana nilizungumza na watu wa *Airtel* waliniyahidi kwamba katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mitambo ameyataja wako tayari kuanza ujenzi mwaka huu katika eneo la Lilombe na maeneo mengine matatu niliyoyazungumza wataenda siku zijazo na inawezekana yakaingia kwenye mpango huu wa *UCAF*.

Lakini eneo la Lilombe litaanza kujengwa mnara hata kabla ya mpango huu wa *UCAF* amba tunauzungumza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mkiangalia muda wetu kwa kweli hauko upande wangu na nimebakiwa na maswali mawili naomba tuwatendee haki Waheshimiwa waliobaki. Naomba nimwite Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje.

Na. 42

### Sheria ya Kodi ya Pango

**MHE. EZEKIA D. WENJE** aliuliza:-

Licha ya kuwepo kwa Sheria ya Kodi ya Upangishaji nyumba imeonekana kwamba wenye nyumba ndio huamua kiasi cha

kodi wanachotaka na kuchukua kodi ya muda gani bila kujali thamani na ubora wa nyumba husika:-

- (a) Je, huu sio muda muafaka kwa Serikali kuweka utaratibu elekezi kwa wamiliki wa nyumba kuwekewa ukomo wa kodi kulingana na ubora wa nyumba?
- (b) Je, kwanini Serikali isisimamie kwa nguvu Sheria ya pango kwa kuwachukulia hatua wenyewe nyumba wanaodai malipo ya pango ya ziada ya miezi mitatu kwa mkupuo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI aijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba kutoa maelezo ya awali juu ya swali la Mheshimiwa Ezekia Wenje. Mwaka 1984 Serikali baada ya kutambua kero wanazopata wapangaji hususan wale wa nyumba za wamiliki binafsi ikiwemo kudaiwa kodi kubwa sana na kutakiwa kulipa kwa mwaka mzima mara moja, kutolewa nyumba bila taarifa wala sababu ya msingi ilitunga Sheria ya uthibiti wa upangaji wa kodi za nyumba. *"The Rent Restriction Act No. 17 of 1984."* Sheria hiyo ilifanya kazi hadi mwaka 2005 ilipofutwa kuitia marekebisho ya Sheria Na. 2 ya mwaka 2005 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) No. 2) Act 2005*). Moja ya mambo yaliolalamikiwa na wadau wa Sheria hiyo ni kuwa Sheria ilimpendelea sana mpangaji kuliko kwenye nyumba. Kufutwa kwa Sheria hiyo kulitokana na Serikali kubaini kuwa haikuwa rahisi kudhibiti kodi katika mazingira yenyewe uhaba mkubwa wa nyumba kuliko mahitaji.

Hadi sasa mahitaji ya nyumba kwa mwaka ni nyumba 250 wakati uwezo wetu yaani ukichukua mashirika yote ya Umma yaliyopo Shirika la Nyumba la Taifa, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na PPF, NSSF PSPF, LAPF na Wakala wa Majengo wana uwezo wa kuzalisha zisizozidi 3,000 kwa mwaka.

Kuwepo kwa Sheria inayoelekeza wamiliki kiwango cha kodi kwa nyumba kulisababisha wawekezaji kukwepa kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba hivyo kudumaza soko la nyumba nchini. Hii ilisababisha kuwepo kwa upungufu mkubwa sana wa nyumba nchini na hivyo kulazimisha wahitaji kukubali masharti wanayopewa na wamiliki ikiwa ni pamoja na kupokea nyumba bila kuhoji ubora, kulipa kodi ya mwaka mmoja au zaidi na kukubaliana na masharti mengine bila kutoa taarifa Serikalini ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mbunge wa Nyamagana, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa uko umuhimu wa kuweka kodi elekezi (*indicative rent*) kwa wamiliki wa nyumba ili kuzuia utaratibu wa kila mmoja kujipangia kodi bila kuzingatia ubora na mazingira ya nyumba yake.

Hata hivyo kwa kuzingatia mazingira ya soko la nyumba ambapo mahitaji ni makubwa kuliko uzalishaji wa nyumba kwa sasa haitakuwa busara kuthibiti kodi ya nyumba.

Pamoja na maoni hayo napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa hivi sasa Serikali inaandaa Sera ya Taifa ya Nyumba. Tunayo matumaini kuwa Waheshimiwa Wabunge wote wakiwa ni wadau muhimu watapata fursa ya kuchangia maoni katika mjadala wa sera hiyo.

Inatarajiwa kwamba sera hiyo itaweka misingi itakayosimamia mahusiano baina ya wamiliki na wapangaji wa nyumba nchini. Baada ya sera kukamilika Serikali itatafakari uwezekano wa kutunga Sheria itakayoweka chombo cha kusimamia maendeleo ya sekta ya nyumba nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hatuna Sheria inayoipa Serikali mamlaka ya kuweka na kusimamia utekelezaji wa viwango vya kodi ya nyumba baada ya Sheria ya Kodi ya Nyumba Na. 17 ya 1984 kufutwa.

Badala yake mahusiano baina ya mmiliki na mpangaji huwekwa na kutekelezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 77 hadi 110 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005. Sheria hiyo pamoja na mambo mengine inatoa fursa kwa mwenye nyumba kupanga bei ya pango ya soko na kumtoa mpangaji kwenye nyumba yake asipozingatia na kufuata matakwa ya mkataba wa upangaji. Aidha Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Nyumba Na. 2 ya 2002 imeanzisha Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya iliyopewa mamlaka ya kusikiliza na kutatua migogoro ya nyumba na mali nyingine yenye thamani isiyozidi shilingi milioni hamsini (50,000,000/-). Migogoro ya nyumba au mali yenye thamani zaidi ya hiyo hushughulikiwa na Mahakama Kuu ya Tanzania.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ni takribani miaka saba toka hii Sheria ya *the Rent Restriction Act No 17 of 1984* ilipofutwa na katika maisha lazima tuangalie *opportunity cost*. Sasa uzoefu unaonyeshwa leo hii kwamba matatizo yanayopatikana leo baada ya Sheria hii kufutwa ni mengi sana kuliko ya huko awali hii Sheria ilivyokuwepo.

Sisi Wabunge tunaotoka mijini watu wetu wengi sana wanapanga nyumba kwa sababu hawana uwezo wa kupanga nyumba na mjini kuna watumishi wa Serikali wanaishi wakiwemo walimu, askari kada zote za watumishi wa Umma. Ukilinganisha leo mtu anaenda kupanga nyumba, mwalimu ndiyo anakuwa *posted* mjini anakuja anatakiwa kulipa kodi ya mwaka mmoja, mshahara wake wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Swali langu

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba kwa matatizo haya yaliyopo. Je, Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka wa kurudisha hii Sheria kama ilivyokuwa ya mwaka 1984 ya *the Rent Restriction Act* hata kama tunaweza tukafanya *modification* ndogo ili ku-balance haki ya mwenye pamoja na anayepanga. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hii Sheria itarudishwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Wenje na kumpongeza kwa namna ambavyo amekuwa mstari wa mbele kushughulikia kero za wananchi wa Jimbo lake pamoja na wananchi wengine kwa ujumla.

Kama nilivyoeleza katika maelezo ya awali tulisema kwamba tatizo liliopo ni uhaba wa nyumba. Natumaini kwa wale ambao wametumia *principles* za kiuchumi kuna kitu kinaitwa *priceless assist of demand. Demand* ikiwa kubwa wakati *supply* ni kidogo bei inakuwa kubwa. Sasa hali ya soko ya nyumba nchini ni baya. Kwa miaka mingi nyumba zilikuwa hazijengwi ni Shirika la Nyumba ndio sasa hivi limeanza baada ya kuandaa mpango mkakati kujenga nyumba kwa nguvu kubwa.

Kwa mfano sasa hivi pale Kigamboni kuna nyumba zaidi ya 200 za gharama nafuu ambazo zinajengwa ili wauziwe wananchi. Kuna nyumba tumepanga kujenga hapo Kongwa, kuna nyumba zimeshakamilika pale Arusha, kuna nyumba zinajengwa Mchikichini na maeneo mengine tunajenga nyumba.

Lakini kwa mfano tukisema leo tunarejesha Sheria ile ya mwaka 1984, maana baada ya Sheria ile kufutwa tumeona kwa mfano maeneo ya Kariakoo mabadiliko yaliyotokea na maeneo mengine. Yale mabadiliko ni nyumba watu wanaingia

sasa kujenga nyumba baada ya watu kuona kwamba kumbe sasa Serikali haina nia ya kutunyang'anya tena nyumba wala kutuzuia wala kuingilia sisi kupangisha tunavyotaka.

Marekebisho haya ya Sheria ingawa kweli imefutwa lakini viko vigezo ambavyo vinatakiwa vizingatiwe katika kupanga kodi. Kwanza tunatambua nyumba inajengwa juu ya ardhi kwa hiyo *rent* ambayo yule analipa tunaangalia ile *rent* ni kubwa kiasi gani. Kuna *Premium of the Insurance* yaani Bima, Kuna kodi ya majengo ambayo inalipwa pia na kodi nyinezo ambazo wenyе nyumba wanalipa. Sasa tukirejesha ile Sheria kasi ya kujenga nyumba maana kama unavyoona watu wana-*scramble* viwanja, wana-*ramble* sio kwa sababu wanataka waishi wao. Wanataka kujenga wapangishe. Tukishaanza kudhibiti wakati bado hatujawa na *balance* katika ya *supply na demand* tutapata tatizo. Mimi naomba tuwe na subira maoni haya tuyatoe tutakapoleta hiyo rasimu ya sera, mtupe maoni ya tufanye nini. Sisi tumesema ikiwezekana tutatunga Sheria na pengine kuwa na chombo kitakachosimamia maendeleo ya sekta hiyo ya nyumba. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge muwe na subira na tutakapokuja na rasimu ya sera mtupe maoni yenu ambayo yatatuwezesha kuandaa Sheria itakayotupeleka miaka mia moja ijayo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Swalii la mwisho kwa siku ya leo Mheshimiwa Sungura.

Na. 43

### **Wavuvi na Askati wa Doria Kupotelea Majini**

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA** aliuliza:-

Kumekuwepo na wimbi la wavuvi kupotelea majini na askari wa doria kuuwawa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru hali hii?

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na matukio kadhaa ya uhalifu unaofanyika majini ikiwemo uporaji kwa vyombo vinavyotumiwa na wavuvi, kuwashambulia wavuvi na hata baadhi ya askari wetu wa doria. Tukio la hivi karibuni la kuuawa kwa askati wetu kule ziwa Tanganyika ni ushahidi tosha wa jambo hili. Hata hivyo. Napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba matukio ya aina hiyo yamekuwa yakipungua kutohana na hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi kwa mashirikiano na vyombo vingine vyatuzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, Serikali inachukua hatua madhubuti za kupambana na uhalifu majini kwa kuongeza doria zinazofanywa kwa kutumia boti za Polisi na pale inapojitokeza dharura boti za JWTZ hutumika. Aidha wavuvi nao wameanzisha vikundi vyao vyatuzi na wanashirikiana na Polisi katika doria hizo kuitia mkakati wa Polisi Jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo tumekuwa pia tukifanya katika vikao vyatuzi ujirani mwema na wenzetu wa *DRC* Zambia na Burundi vyenye lengo la kuimarisha ushirikiano katika kupambana na uhalifu kwenye mipaka ikiwemo mipaka ya maji. (*Makofi*)

**MHE. SABREENA HAMZA SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa katika matukio haya wananchi na na askari wamekuwa wakipoteza maisha.

Je, Waziri sasa Serikali iko tayari kutoa mkono wa pole kwa familia za askari na wananchi waliopoteza mali na maisha yao?

Swali la pili, nataka kujua kwanini Serikali sasa haipo tayari kutoa silaha za kisasa na imara kuwapatia askari wetu pamoja na posho motisha na mishahara kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu mkono wa pole kwa askari na wahanga wengine ambao ni raia. Kwa upande wa askari kuna utaratibu maalum wa kufidia askari wanaopata au kujeruhiwa au kupata majanga ya namna hii ambayo yatasababisha kifo. Kwa upande wa raia ... (*Hapa Hapakusikika*)

**NAIBU SPIKA:** ... karibuni sana hapa Bungeni. Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Vicent Nyerere, ambaye ni Dr. Mazara. Karibu sana. Baada ya wageni hao sasa matangazo ya vikao vya kazi nikianza.

Nikianza na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Abdulkarim Shah anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa saba katika ukumbi wa Pius Msekwa C.

Mheshimiwa John Lwanji anaomba Kamati hiyo ikutane saa saba mchana Ukumbi 227 ghorofa ya pili Jengo la Utawala. Mheshimiwa Peter Serukamba Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane ukumbi namba 231 saa saba mchana. Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja  
na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2012/2013  
na Makadirio ya Mapato na Matumizi  
ya Serikali kwa mwaka 2012/2023**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea na kama nilivyosema mchangiaji wetu wa kwanza asubuhi hii ya leo atakuwa ni Mheshimiwa James Mbatia na atafuatiwa na Mheshimiwa Kulikoyela Kahigi. Mheshimiwa Mbatia dakika kumi.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kwanza asubuhi hii ya leo. Hoja iliyoko mbele yetu ya Hoja ya Bajeti waswahili wanasema kupanga ni kuchagua. Ukiilinganisha Bajeti hii na Bajeti zilizotangulia, alipokuwa anawasilisha maoni ya Kamati Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge alisema thamani ya shilingi yetu mwaka jana ukilinganisha na dola iliwa ni shilingi 1449.5/- kwa dola moja.

Mwaka huu shilingi yetu imeshuka thamani, kwa sasa ni shilingi 1599.98/- kwa dola moja. Ukiilinganisha na anguko la thamani ya fedha yetu na mfumko wa bei kutoka asilimia nane mpaka asilimia 18.7 ni kwamba Bajeti ya mwaka huu haina nyongeza ya aina yoyote. Haipo.

Ukiweka kwenye uwiano huo utaona kwamba Bajeti hii ungechukua thamani ya shilingi kama ilivyo triliioni 13.5 za mwaka jana itakuwa ni sawa sawa na triliioni 14.9 ambayo ni karibu triliioni 15 hizi zinazoombwa na Serikali leo hii hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisikia michango iliyotolewa na Wabunge wote tangu jana, Tanzania ni yetu sote, ningeshauri kwamba mchangano uliotoka kwa Wabunge wote uzingatiwe

kwa sababu naamini wazo zuri ni zuri tu hata kama lingetoka kwa mtu ambaye hupendi sura yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikufurahishwa sana jana na michango yote iliyotolewa na Kambi ya Upinzani si lolote si chochote, siyo sahihi kabisa. Tanzania watu tunao, takribani milioni arobaini na tano. Kwa hivyo *Human Resources* tuliyonayo tukiitumia vizuri, tukatumia ardhi tuna kilomita za mraba zaidi ya laki tisa arobaini na saba elfu na mia tatu, ardhi ipo, tukirejea kauli ya mwalimu kwamba ili tuendelee tunahitaji Watu, Ardhi, Siasa Safi na Uongozi Bora, kuna tatizo kubwa kwenye siasa zetu na tuna tatizo kubwa kwenye uongozi wetu.

Ninasema hivyo kwa sababu ukiangalia makusanyo yetu ya humu ndani trillioni nane, inaonesha utamaduni wetu sisi Watanzania au utamaduni uliowasilishwa hapa, yaani tuseme ni Bajeti ya utamaduni wa Watanzania wa kupenda kutumia zaidi na siyo kwenye maendeleo. Kwa sababu huwezi ukatumia zaidi ya asilimia sabini na maendeleo ukayawekea asilimia thelathini na zaidi ya asilimia hamsini ya Bajeti wenyewe ya maendeleo ikawa ni fedha ya kutoka nje.

Sasa ni kwamba Je, Bajeti hii tunategemea wafadhili ili tuweze tukafanya shughuli zetu, tunategemea wafadhili ili tuweze tukasomesha watoto wetu, tunategemea wafadhili ili tuweze kufanya shughuli zetu ambazo hata za kujhudumia sisil wenyewe kwa miaka yote tangu tumepata uhuru wa Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 tutapimwa kwa malengo ya Milenia, lengo la kwanza la milenia ni kupunguza umaskini, lengo la pili ni elimu kwa wote, lengo la tatu ni masuala ya jinsia na kuwawezesha akina mama, lengo la Nne ni masuala ya vifo vya watoto wadogo, vifo vya akina mama ni lengo la Tano, magonjwa ya Ukimwi na mengineyo, mazingira na *global partnership* ya nane. Je, Bajeti hii imeweka namna gani kwenye jedwali dogo tu la kuonyesha kwamba

malengo ya milenia tumefikia wapi moja baada ya jingine, au ni historia ndefu tu ambayo ina *confuse* hata Wabunge katika kuisoma Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma zile *Volumes, volume (I)* mpaka (IV) inaonekana ni kuchanganya changanya tu, ingewekwa jedwali dogo zuri, hata kama mtu siyo mchumi kama mimi hapa niweze nikalielewa vizuri. Lakini kuja na tarakimu nyingi tu. Je, *efficiency* ya Bajeti ya mwaka jana ilifanikiwa kwa kiasi gani. Je, Bajeti hii naweza nikadiriki kusema kwamba ukisoma kwa makini na ukiangalia Bajeti hii imeshindwa hata kuondoa msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba Jiji la Dar es Salaam kwa takwimu ambazo zipo miaka mitatu iliyopita tunapoteza zaidi ya shilingi bilioni nne kila siku na hii inatokana na mafuta tunayotumia, muda wa kazi ambao ni zaidi ya asilimia thelathini unapotea tukiwa kwenye foleni barabarani, uchafuzi wa mazingira tunaoufanya *cabondioxide* inayotoka kwenye magari haya, ukiangalia uzalishaji yaani *man power efficiency* ya wafanyakazi wetu takribani sasa tunasema milioni kumi wanaoishi katika Jiji la Dar es Salaam, tunajiongezea umaskini siku hadi baada ya siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Bajeti hii uwezo kama ni triliuni kumi na tano, hapa nilinganishe kwamba yupo Daktari ambaye ana wagonjwa wa malaria wapo mia moja na uwezo wake wa kuwatibu ni wagonjwa ishirini na tano tu. Je, utatibu wa wagonjwa 25 ili wapone au utagawa robo robo ili utibu wagonjwa wote mia moja ili wapone? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya miundombinu inasikitisha sana, usafiri ambao ni rahisi kuliko wote duniani wa kwanza ni maji, wa pili ni reli na watatu ni barabara na wa nne ni anga. Lakini ukiangalia Bajeti hii kwenye bandari, kwenye reli kwenye anga ni bilioni takribani mia tatu tu. Hii ni Bajeti ya

kuongeza umaskini kwa Watanzania na wala siyo Bajeti ya kuleta ahueni kwa Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia misamaha ya kodi tunayoizungumzia, hii misamaha ya kodi ukiangalia zile taasisi ambazo zinasamehewa kodi, ukiangalia kama *NGOS* unaweza ukachukulia *NGOs* kama *Aghakan Foundation*, imekuwa ikipewa misamaha ya kodi tangu Serikali ya awamu ya kwanza mpaka leo hii. Je, hospitali za *Aghakan* zinatoa huduma zilizo bora zaidi kuliko hospitali nyingine na aghali zaidi. Je, zinawasaidia maskini hapana! Je, haki inatendeka? Je, wazawa wa Taifa hili wanaolima pamba, wanaofanya biashara ya pamba, watu wanasema *no book no cotton* nakubaliana nao kabisa.

Je, wanasaidiwa namna gani akina ndugu Gungu na wenzake? Je ukiwasaidia wazawa ukatoa upendeleo wa maksudi kwa wazawa ambaao Watazalisha zaidi humu humu ndani, ukawa wazawa takribani kama elfu mbili ambaao wana uwezo kama akina Reginald Mengi, wakaweza kuajiri watu labda elfu tano tano kila mwaka ni kwamba tatizo la ajira tutakuwa tunaajiri zaidi ya watu milioni kumi na tutakuwa tumeondokana na tatizo la ajira. Tatizo la ajira siyo la Serikali peke yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna msemo unaosema makosa yetu ya jana japo yanositisha sana ni mafundisho yetu ya leo, sioni dhamira yangu inapinga. Tumeanza hapa kwa kusoma dua ya kusema ewe Mwenyezi Mungu atujalie ili tuweze kufanya maamuzi yaliyo sahihi mimi siungi mkono kabisa Bajeti hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikubali, Waziri na Serikali yote *collectively* wakae, maoni yanayotolewa yote hapa warekebishe Bajeti hii kwa maslahi ya Taifa la Tanzania kwa kuwa Tanzania ni yetu sote na hakuna watu wenye Hati miliki ya kuwaongoza Watanzania milele. Hili tukilisema vizuri

kwa utaratibu tutaelewana, isionekane kwamba kuna mtu mwenye mawazo bora kuliko mwingine au kila wazo lichukuliwe kwa ubora wake, kila wazo lisikilizwe kwa ubora wake na tukisikilizana vizuri ninaamini masuala ya MKUKUTA, sioni hata suala la MKURABITA huku mnasema mabenki yawepo, MKURABITA iko wapi, watu wana samani gani za kuweza kurasilisha mali zao. Kwa hivyo kuna mambo mengi ya kinadharia zaidi kuliko vitendo ndani ya Bajeti hii. Niombe *efficiency*, na *reliability* tutaweza tukafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, siungi mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa James Mbatia kwa hotuba yako ya kianzio. Nilisahau tangazo moja la Mheshimiwa Zedi Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, ambalo anawaomba Wajumbe wa Kamati husika wakutane saa saba mchana ukumbi wa Msekwa (B).

Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie. Mimi nitaanza kwa kuungana na wenzangu wanaoikataa Bajeti hii kama illivo, na ninaungana na wale ambao wanaunga mkono hoja kwamba Bajeti hii iende ikafanyiwe marekebisho na Serikali halafu irudishwe tena hapa tuijadili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi yameshasemwa na msemaji wa Kambi ya Upinzani na mengine yameongezewa leo na Kiongozi wa *NCCR Mageuzi* ambaye namwunga mkono kwa yale ambayo ameyasema yanajenga. Kwangu mimi, kwa kuwa mengi yameshasemwa nitazungumzia mambo machache tu na yale nitakayozungumzia ni ya kushadidia tu yale ambayo yameshasemwa na kusositiza baadhi ya mambo.

Kwangu mimi naona kwamba tatizo tulilonalo kama ambavyo imeshadokezwa na wengine ni kwamba Serikali iliyopo ina tatizo la mazoea au tabia ya kutoa ahadi au kupanga mipango ambayo haitekelezeki kwa kiasi kikubwa na kwa wakati ambao umepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linatokana na mazoea pia ya kutokukusanya mapato ya kutosheleza kutekelezea mipango au ahadi ambazo zimetolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri wa ahadi ambazo hazijatekelezwa kwa zaidi ya miaka kumi ni ahadi ya umeme katika Jimbo la Bukombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi Bukombe huko ni kama kwenu unapafahamu, hakuna umeme na Serikali ya Chama hiki ambacho ni Chama changu cha zamani imekuwa ikifika Bukombe hasa wakati wa uchaguzi ikitoa ahadi ambayo baadaye watu wanapouliza unaambiwa kwamba kuna matatizo haya na haya visingizio vitupu. Huu ni mfano mmoja tu lakini mifano ipo mingi sana, na mifano katika Bajeti ambayo inaisha mwezi huu ni mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ambayo inaisha mwezi huu haijatekelezwa kwa kiasi kikubwa.

Je, Bajeti hii ambayo tumesomewa itatekelezwa? Kwa sababu sera ni zile zile, vipaumbele ni vile vile na makusanyo ya mapato yanatumia vyanzo vile vile. Mimi nina shaka kabisa kwamba hii Bajeti inaweza kutekelezeka, Haiwezi! Hilo ni tatizo la kwanza. Tatizo la kutoa au kupanga mipango ambayo haitekelezwi kwa wakati na kwa kiasi cha kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la pili ambalo ninaliona katika Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ni tatizo la kukosa utashi wa kisiasa wa kukusanya kodi licha ya kwamba nchi hii

ina rasilimali za kutosha. Nakumbuka Mwalimu Nyerere kuna wakati fulani alipokuwa anazungumza na wafanyakazi akasema kwamba Serikali ambayo ni *corrupt* haikusanyi kodi na alitoa mfano wa Italy lakini wakati huo huo alikuwa anazungumzia Serikali ya Chama chake Chama cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza, maoni yote ambayo yanatolewa hapa yachukuliwe na yafanyiwe kazi. Tuna watalaan wengi ambaa wana utalaam wa kodi na utalaam wa uchumi kama Profesa Lipumba sijui kwanini hamatumii huyu msomi, mimi nilisoma naye ni msomi mzuri sana wa uchumi, Dokta Ngowi ambaye juzi alikuwa anatueleza kuhusu masuala kama haya haya kwanini hatuwatumii hawa?

Tuondokane na tabia ya kujifungia kwenye vyumba vyetu na kusahau kwamba huko nje kuna watalaan ambaa labda wanawazidi. Tutumie rasilimali watu tuliyonayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mfupi nitazungumzia jambo la mwisho linalohusu kilimo. Nakubaliana na Mhehsimiwa Nundu aliyesema kwamba kwa hakika hatuna nia ya dhati ya kuendeleza kilimo kwa sababu hatuna viwanda. Hatuna viwanda vya kutengeneza matrekta, hatuna viwanda ambavyo vilikuwepo zamani vya kutengeneza zana za kilimo, kwa hiyo, hilo halikuzingatiwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine kuhusu kilimo ni kwamba hatutendei haki wakulima wetu wa pamba, korosho na kadhalika. Kwa hiyo, naungana na Wabunge wa Kanda ya Ziwa na Kanda nyingine ambazo zinalima Pamba, tumeambiwa na wapiga kura wetu kwamba kama hakuna '*buku*' hakuna pamba. Serikali hii ijifunze kutoka nchi zingine ambayo huwa inatoa ruzuku kwa wakulima ili iwasaidie kufidia hasara ambazo wanazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Serikali ikiongeza fedha kidogo hiyo buku itafika ili wakulima na wao angalau wapate hiyo '*buku*'.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine nitayachangia kwenye maandishi, ahsante sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mussa Kombo atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu na Mheshimiwa Kafulila ajiandae.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi natatizama matatizo ya Bajeti hii katika mafungu matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kiutawala tuna *Executive, Judiciary, Legislative*. Ukiangalia hii Bajeti haiko hivyo na ndiyo mawazo ya Wabunge wenzangu yame-side kwenye uchumi tu.

Sisi Watanzania tunajisifu sana kwamba ni watu wenyewe demokrasia na tunatekeleza haki za binadamu. Muhimili wa *Judiciary* ambao ndiyo unasimamia mazungumzo yote ya sheria leo walikuwa wanaomba au tulikuwa tunaombwa angalau wapewe asilimia asilimia mbili ya Bajeti ya nchi, lakini kipindi kilichopita walipewa billioni 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu bado ina matatizo makubwa sana ya usimamiaji wa sheria, leo hakuna Mahakama za Mwanzo kwa sababu hakuna pesa wanazopewa hawa watu. Sasa mahakama ya Mwanzo ndiyo inasimamia haki za Watanzania kule chini.

Hakimu mmoja wa Mahakama hiyo anakwenda vijiji vitano, sita. Leo sisi tunaokaa mijini na ambao tuna uwezo ndiyo tuna haki ya kuona kweli nchi hii iko huru na inatekeleza haki hiyo. Hili linatokea kwa sababu hawapewi ile asilimia mbili

ya bajeti wakapanga wenyewe nini la kufanya. Kwa hiyo, Mhimili huu pia hauna msingi zaidi ya yale maelezo wanayofanya wao. Sasa sisi kama Wabunge na tunataka kuisimamia nchi hii kwa uhalali huu, muhimu lazima wapewe fedha zao waweze kutekeleza majukumu waliyonayo. Inafikia mpaka Mwenyekiti wa Kijiji anampiga mtu bakora anamtoa mimba, kwa sababu hakuna anayesimamia sheria kule na kwa sababu hiyo *why* hii Mahakama haipewi?

Wanataka kuajiri wanasheria 300 ambao wametoka chuo ili kuisaidia hii *judicially* kwenda kufanya haki kule chini, hakuna kinachofanyika. Tuna matatizo hatuyaangalii na hatuyaoni. Kama hatuwezi tukaheshimu sheria haya tunayozungumza yote ni yanapita tu.

Tukienda hata Mhimili wa Bunge wa kutakiwa wapewe asilimia mbili ya bajeti hakuna. Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwenyewe anakuja kutuambia kwamba viwango vyta kodi sasa vimikuja kutohana na maamuzi ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Waziri angetueleza; je, haoni pia kwenye viwango hivyo vilivyopitishwa na Wabunge wa Afrika Mashariki akasema nao umefika wakati na hata mishahara ya Wabunge wa Tanzania sawa na Wabunge wa Afrika Mashariki? Haoni kuwa suala hili litasaidia kuweka uwiano? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, *TRA* inakusanya mapato katika Bandari ya Zanzibar na katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Bandari ya Zanzibar ipo chini ya Muungano na kwa kipindi chote hakuna hata mpango mmoja wa *kui-promote*; inapangiwa vipi, itaendelezwa vipi, itafanywa kitu gani, zaidi ya kukusanya mapato jioni yakaondoka Zanzibar kuja Bara. (*Makofii*)

Wanazungumzia njia ya mapato ya utalii. Zanzibar ni kisiwa kidogo sana ambacho kina vivutio vingi sasa, lakini watalii wote wanaokuja Zanzibar wanalipa kwenye Ubalozi nje, kodi ambayo ingetusaidia Zanzibar inalipwa kwenye Ubalozi.

Zanzibar wanafaidika kwa kitu kimoja tu nacho ni *airport service charge*. Mnatusaidiaje katika bajeti hii ambayo imepangwa katika maendeleo hayo? Inawezekana watu wanasahau au Waziri amesahau kwamba anapata pato hilo kubwa kutokana na visiwa vile ambavyo vina umaskini mkubwa. Ninaomba Waziri atakapokuja anisaidie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo makubwa ambayo tunayapata ni ya mfumko wa bei; leo Tanzania uko asilimia 20. Matatizo yake ni kwamba, sisi tunashindwa kupata chakula ambacho kina lishe. Matatizo hayo yanatokea sasa, akina mama wajawazito na watoto wachanga, wanazidi kupoteza maisha kwa sababu hawapati chakula chenye lishe kutokana na *cost exactly*. Naomba yale maneno ambayo amesema Waziri kwamba ataagiza mchele mwingi, ataagiza sukari, anapanda miwa kwenye mabonde mengi, sasa aangalie hatari hii tuliyonayo. Tunazungumza sana kama nchi kwamba tunazuia vifo vya akina mama na watoto lakini hatusemi sababu ya vifo hivyo. Kwa kuwa sote tunajua kuwa, haiwezekani gari zuri ambalo halitiwi *grease* na *oil* lisife injini; ndiyo maana wale wazee wetu au mabibi zetu ambao huwa hawali vizuri wanapokuwa wajawazito, wanakosa nguvu, wanashindwa kujifungua na watoto wanakufa. Tukubali kwamba ni sababu ya huu mfumko wa bei. Tuongeze nguvu tulime twende vizuri ili tuweze kuondoa matatizo ya Watanzania wenzetu. (*Makof!*)

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu sana tangu tulipokuwa tukikaa pamoja 1956, lakini kwa kuwa haya anayoyazungumza ni ya nchi, basi Mheshimiwa Waziri ningelikumba urudi ukakae na wenzako ili uweze kutekeleza kitu ambacho kitawasaidia Watanzania. Siwezi kuunga mkono hoja mpaka mabadiliko haya yatakapokuja. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nitaomba michango ambayo

Wabunge tunatoa, Serikali ichukulie kwa umakini na iifanyie kazi kama inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nataka nizungumzie kwenye mpango na mfumo wa utengenezaji wa bajeti. Lazima tukubaliane kwamba, mfumo ambao tunautumia kwenye kutengeneza bajeti, hauna uwiano na mlingano ambao unafaa. Nakupa mfano katika bajeti ambayo tumeipanga hii ya mwaka 2012/2013, Mkoa wa Lindi katika matumizi yake yote ya maendeleo na ya kawaida, tumepangiwa shilingi bilioni 14. Tunafanana na Mkoa wa Rukwa, pamoja na kuwa Katavi unashika mkia kwa kupata shilingi bilioni nane lakini Katavi una Wilaya mbili tu, sisi tuna Wilaya zaidi ya sita. Katika uwasilishaji wa Mpango wa Uchumi ambao umewasilishwa kwa mwaka 2011, tathmini iliyokuwa inatolewa na Mheshimiwa Wasira alisema, Mkoa ambao unaongoza kwa kuwa na mtawanyiko mdogo wa watu ni Mkoa wa Lindi. Sababu za kupelekea mtawanyiko huu kuwa mdogo ni kwamba, watu wengi kutoka Lindi wanakimbia wanahamia katika maeneo mengine, ndiyo maana tunasema mfumo huu wa bajeti una matatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote tumekuwa tunalalamika hapa tunahitaji tujengewe barabara na ielewewe barabara ambazo tunazungumzia sisi hatuhitaji kwa ajili ya misafara ya harusi kutoka na kwenda katika kumbi, tunahitaji barabara zijengwe ili mazao ambayo yanazalishwa na wakulima katika maeneo ya Njinjo, Miguruwe, Kandawale na Mikoa yote ya Lindi na Mtwara, yafike kwenye soko na yaweze kuchangia katika uchumi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alianzisha Dhana ya KILIMO KWANZA kwa nia nzuri sana. Ninaona sasa hivi imebadilika imekuwa KILIO KWANZA, kwa sababu sijaona ni namna gani ambavyo bajeti hii ambayo imepangwa itaweza kuinua kilimo katika nchi yetu. Wana wetu hawa Wasukuma na Wanyamwezi, wamekuwa wanalamika kuhusiana na tatizo la

pamba na sisi tunalalamika kuhusiana na tatizo la viwanda vyatkorosho. Kuna tatizo gani tukiondoa VAT kwa viwanda vyetu vyatndani vyatnguo ili soko la pamba liweze kushika kasi na tuweze kuzalisha hapa nchini kwetu? Katika uondoaji wa hili tuangalie, lazima tuvipe nafasi viwanda vyetu vyatndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia mishahara ya watumishi; ipo haja ya kuboresha maslahi yao, lakini kubwa ambacho nilitaka nikizungumzie, sasa hivi kumekuwa na *loan sharks* wengi sana ambapo mtumishi anakopa na analipa riba ya ajabu ambayo haijawahi kuonekana duniani. Mtu ambaye anakopa milioni mbili, inafikia wastani wa kulipa zaidi ya milioni 20. Kwa nini *NMB* isipewe uwezo ama mabenki yetu ya ndani yasipewe uwezo kuwakopesha watumishi waweze kujikimu katika maisha yao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la gesi. Leo hii kumekuwa na uvumbuzi wa gesi katika Mikoa ya Lindi ya Mtwara lakini fedha ambazo zinatokana na mapato ya gesi haya, tunaishauri Serikali isomeshe watoto wa Lindi na Mtwara, ambao siku zote wamekuwa wako nyuma. Huu ndiyo ukombozi pekee ambao utapelekea wao kujikomboa kutoka nafasi ambayo walikuwa nayo chini kabisa kielimu na itapanda kwa kiasi ambacho kinafaa kwa wastani wa kitaifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo ambalo tumekuwa tukilizungumzia hapa la Deni la Taifa. Naishauri Serikali kwamba, waanze kulipwa wakandarasi wa ndani kwa sababu wengine wamekuwa wakidai kwa kipindi kirefu na mzunguko wa fedha unakuwa na matatizo kwa sababu fedha hizi wamekuwa wanawalipa watu wa nje tu ambao hata hatujui fedha zilikopwa kwa ajili ya kitu gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kwenye mfumo wa ukusanyaji tozo za Halmashauri. Nazungumzia kwa wale wakulima ambao wanafanya biashara ya mazao asilia kama nazi, embe, machungwa na kadhalika. Leo hii mtu ambaye

ameshalipa ushuru kutoka kwenye Halmashauri ya Kilwa akifika kwenye Halmashauri nyingine kama Rufiji ni kama vile ametoka kwenye nchi nyingine ameingia kwenye nchi nyingine. Sasa Waziri wa Fedha hili inabidi aliangalie na atafute namna bora ya kuweza kuliweka sawa ili wananchi wetu wasiendelee kupata matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la mfumko wa bei. Wakati tunapitia Mpango wa Uchumi wa Maendeleo kwa Mwaka 2012/2013, kuna mtu mmoja kutoka Kamisheni ya Mipango alinijibu kwamba, mfumo wa kuwepo Tume ya Bei ili kuweza ku-regulate bei hasa za vyakula umepitwa na wakati na hutuwezi kurudisha Tume ya Bei. Nataka nimwambie kuwa, India na Marekani ni moja kati ya nchi ambazo zinafuata mfumo huria, lakini bidhaa zote ambazo zinazalishwa India na zikaingia kwenye soko la kawaida, zinaandikwa *maximum retail price*. Sijasema lazima turudishe Tume ya Bei, lakini ni lazima tuweke mfumo ambaao utawasaidia wananchi kuweza kunufaika na hali ya vyakula na kadhalika. Bei ya vyakula ni kubwa sana na mfumko wa bei uko juu. Lazima tuweke mfumo ambaao utatusaidia sisi kuweza kukabiliana na hili tatizo. Wananchi wanalamika na Viongozi pia wamekuwa wanalamika; sasa sijui nani ambaye hastahili kulalamika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilli, Jumamosi ya wiki hii, Mheshimiwa Spika alituagiza kwenda Iringa, Bodi ya Mazao Mchanganyiko inatakiwa sasa ipewe mtaji wa kuweza kuijendesha ili moja kwa moja iweze kuingia kwenye biashara ya vyakula. Tunataka Bodi ya Mazao Mchanganyiko ipewe uwezo ili iweze kushiriki biashara ya unga, biashara ya mchele na biashara ya sukari ili kushindana na wafanyabiashara wa kawaida ambaao wamekuwa siku zote wanawaumiza wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nilipenda nilizungumzie ni kuhusiana na suala la mgawanyo wa Wilaya.

Wananchi ninaowawakilisha siku zote wamekuwa wakilalamika kwamba, Wilaya yetu ni kubwa, inawiana na ukubwa wa Mkoa fulani ambao siwezi kuutaja lakini tunaona tu Wilaya nyingine zinagawanywa hata Mikoa inagawanywa ikiwa na Wilaya mbili. Sasa hili tuliangalie. (*Makof*)

La mwisho kabisa, nzungumzie kuhusiana na rada. Taarifa ambazo zimetolewa hapa Bungeni kwamba fedha za rada zilizorudishwa zinakwenda kwenye Mikoa mitatu; niseme tu kwamba, hilo ni jambo ambalo halitakubalika na wala isifikiriwe kwamba linaweza likafika hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, siwezi kukubali kuunga mkono hoja na wala siwezi kuikataa hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu ameamua kuwa popo.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia asubuhi ya leo kuhusiana na Hotuba ya Bajeti kwa mwaka huu wa fedha. Awali ya yote, ningeomba kama ambavyo baadhi yetu wamepata kushauri kwamba, mjadala huu wa bajeti unapaswa watu tuujadili bila ushabiki; ni hatari sana kuufanya mjadala huu kuwa wa kishabiki kwa sababu Watanzania wanaumia. (*Makof*)

Leo nazungumza hapa kwa mujibu wa Taarifa ya *WHO*, takriban watoto 183,000 wafariki kila mwaka kutokana na huduma duni za afya, sawa sawa na watoto 501 kwa siku, pia ni sawa sawa na takriban watoto 30 kwa saa. Kwa hiyo, unapozungumza kishabiki masuala ambayo yanahusu mgawanyo wa rasilimali za walipa kodi wa Taifa hili, unapoingiza ushabiki kwenye kujadili namna hii keki iweze kuwafikia hawa maskini, itafika mahali watachoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takriban miaka kumi Serikali imeshindwa kutanzua mlinganyo wa umaskini na ufukara katika nchi hii. Imeweza kukuza uchumi lakini imeshindwa kuondoa umaskini. Sababu kubwa ni moja; imewatenga wananchi wanaoishi vijiji. Leo uchumi wa vijiji, *rural growth* ni takriban asilimia moja tu. Uchumi wa Taifa zima ambao ni kati ya asilimia sita mpaka saba, nimemsikia Waziri wa Fedha anazungumza kwamba, tutajitahidi kuongeza ukuaji wa uchumi huu. Kwa stahili hii hata ukikua kwa asilimia 50 bado umaskini utakuwepo, kwa sababu Serikali imeshindwa kukuza uchumi vijiji. Jibu la kwanza la kutanzua mgogoro wa umaskini vijiji ni lazima Serikali iwekeze kwenye kilimo *serious*. *REPOA* wameshafanya utafiti kwamba kama tukuzu kilimo kwa asilimia kumi kwa miaka mitatu mfululizo, tutakata umaskini kwa asilimia 50. Tangu mwaka 2006, *REPOA* wamekuwa wanatoa ripoti mpaka leo kilimo kinakua kwa asilimia nne. Kwa hiyo, majibu yapo, leo ardhi ya Tanzania ni kubwa na inatosha kabisa kwa chakula cha ndani lakini kwa biashara, Taifa la Tanzania leo ni miongoni mwa Mataifa machache ambayo yanekuwa yakitegemewa *ku-export* chakula katika mazingira ya sasa ambayo Afrika inakabiliwa na janga kubwa la njaa.

Tanzania tuna takriban hekta 29,4000,000 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini kwa takriban miaka hamsini, Serikali imeweza kuwekeza kwenye ekari laki nne tu kati ya hizo. Kwa tafsiri nyingine ni kwamba, kama katika miaka hamsini tumewekeza kwenye ekari laki nne kati ya 29,4000,000, maana yake itachukua miaka 3,625 kukamilisha ardhi yote hii ambayo inatosha kwa umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili kwa sababu dunia ya sasa tunakabiliwa na tatizo kubwa la mvua, lakini Tanzania ni nchi ya 11 kwa mito mingi duniani. Tafsiri yake ni kwamba, kilimo cha umwagiliaji kinatosha kabisa kuwa biashara. *Ku-export* siyo lazima *tu-export* dhahabu au almasi tu, kwa mazingira ya sasa ambapo kuna njaa, chakula kinaweza kuwa biashara yetu. Kenya kuna njaa, Ethiopia wana njaa, Somalia

wana njaa, Waziri Mkuu anakwenda mpakani kuzuia watu wasiuze chakula kwa watu wa Kenya kwa sababu Tanzania itapata njaa, badala ya ku-export sasa tunakwenda kuzuia kwa sababu ya hofu ya kwamba kama tutauza chakula tutapata njaa. Hili ni tatizo, tungewekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji, tungeweza kabisa kuitumia njaa ya Kenya na Somalia kuwa *export* kwetu, lakini sasa tunakwenda kuweka *barrier* kuzuia watu wasiweze kuuza chakula chao kwa bei ambayo ingewanufaisha wakulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna kila sababu ya kuwa Taifa la watu ambao wanaweza kuishi maisha mazuri. Huu umaskini ambao Watanzania wanao ni wa kupakaziwa, tunalazimishwa kuwa maskini, hakuna sababu ya kuwa maskini. (*Makofi*)

Leo Tanzania ni nchi ya tatu kwa kupata misaada mingi duniani, tunapata misaada sawa sawa na nchi ambazo zipo vitani. Tunashindana na Somalia, tunashindana na nchi ambazo hali ya usalama ni mbaya, yaani ni sawa sawa na mtu mwenye afya ya kutosha anakunywa uji wa mgonjwa. Hii misaada ambayo tunaipata, ingetosha kabisa. Tungewaachia watu wa Congo na Burundi ndiyo waipate, siyo sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa utajiri tulionao, tunapaswa kuwa na *donor country*. Hii ni nchi ambayo tulipaswa tukae na Waingereza, Wamarekani na Mataifa yenye uwezo, tujadiliane nao namna gani ya kuzisaidia hizi nchi maskini; ni aibu. (*Makofi*)

Nilikuwa naangalia Ripoti ya *Economic Intelligence*, ni *current* kabisa wanaonesha kwamba, 2012 ukijumlisha misaada wanayoipata nchi ya Somalia, Cameroon na Serbia kwa ujumla wao, yaani nchi zote hivi nne ukijumlisha misaada yao haifikii misaada ambayo nchi moja tu ya Tanzania inaipata. Tanzania ni nchi ambayo ina rasilimali nyingi, tuna amani maana wanauchumi wanasema; *no peace no*

*production.* Katika watu wastaarabu duniani, hii ni nchi ya watu wastaarabu sana duniani. Tunazidi nchi nyingi za Ulaya kwa ustaarabu, lakini bado Serikali inashindwa kutumia fursa ya ustaarabu ya binadamu hawa, rasilimali ambazo zinawazunguka kuwafanya waishi maisha mazuri na wanabaki wanataabika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza hapa takriban asilimia 45 ya watoto wenyewe umri chini ya miaka miatano wamedumaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila, tunazungumzia bajeti, nakukumbusha endelea.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nayazungumza haya kwa sababu hamuwezi kupanga kama hamtambui hali halisi ya wananchi ambao mnapanga maendeleo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima mnapokaa kwenye *Cabinet* myaone haya. Nayazungumza haya, Wataalamu wa Saikolojia wanasema, moja ya tatizo kubwa la binadamu, wanazidiana viwango vya kufikiri. Kuna binadamu ambao uwezo wao wa kufikiri unaishia familia zao. Ukimpatia Uwaziri binadamu ambaye uwezo wake wa kufikiri unaishia kiwango cha familia yake, kazi pekee atakayofanya ni kujillimbikizla mali, anawaza kesho kutwa Baraza likivunjwa nitatokaje. Tunahitaji Viongozi ambao uwezo wao wa kufikiri unakwenda zaidi ya familia yao, zaidi ya Mkoa wao. Tunahitaji Viongozi ambao wanafikiri kuhusu nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imebarikiwa kuwa mionganoni mwa nchi ambazo kijiografia zina nafasi kubwa ya kufaidi uchumi wa nchi zingine ambazo tunapakana nazo. Tanzania, kijiografia tunapakana na nchi ambazo hazina Bandari. Mwenyekiti wangu amezungumza hapa kwamba, nafasi ya Tanzania inafanana sana na nafasi ya Netherlands

pale Ulaya. Pale Ulaya, Netherlands ni *hub* ya *transport*; wanauchumi wanaonesha kwamba, tukiwekeza kwenye Sekta ya Usafiri pekee yake, hii Sekta ya Uchukuzi inaweza ikachangia *GDP* kuliko sekta zingine zote kama madini au utalii. (*Makofi*)

Leo naambiwa bajeti ya reli miaka hamsini bado tunatumia *meter gauge*, yaani hii *meter gauge* hata viwanda vya kutengeneza *engine* ambazo zinapita kwenye *meter gauge* ni kazi kuvipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kutengeneza *engine* ya treni itakayopita kwenye *meter gauge*, itabidi utoe *order* maana hakuna tena duniani, kwingine huko hawafanyi tena hiyo biashara, wanatumia *standard gauge*. (*Kicheko/Makofi*)

Gharama ya kujenga kilometa moja, *a single track* ni takriban dola milioni 3.4, ni pesa kidogo lakini mpaka leo, kila siku bajeti zile zile, mikakati ile ile, maswali yale yale, hawawezi kupata majibu ndugu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inabidi ianze kuongeza uwezo wa kukusanya kodi. Ukitazama makampuni makubwa ambayo yanaongoza kwa kulipa kodi Tanzania, kwa miaka mitano (2006 mpaka 2011), kampuni za madini, mgodi kama wa Barrick na watu wa Barrick hawamo; nikajuliza hivi inawezekana kweli Serengeti ikawa mionganoni mwa kampuni ambazo zinalipa kodi kwa kiasi kikubwa halafu Barrick isiwemo? Yaani pombe, hii chang'aa; wauzaji wa pombe wanalipa kodi kubwa kuliko Kampuni ya Barrick ambayo ni *multinational*? (*Makofi*)

Haiwezekani Serengeti wanalipa, sigara wanalipa kodi kubwa, wako katika *best fifteen*, lakini Kampuni ya *VODACOM* haimo, Kampuni ya *TIGO* haimo; inawezekana kweli? Kwamba sasa mnaendesha uchumi kwa kutegemea pombe; watu wakiokoka? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *this is a challenge*. Tunahitaji muongeze mapato ya kodi kwenye kampuni za simu. Kampuni za simu wanaiba kodi kupita kiasi tumechoka. Tunahitaji muongeze mapato kwenye migodi ya madini. Leo kwenye migodi ya madini kuna viwanja, ndege zinaingia bila utaratibu na zinatoka bila utaratibu; hii nchi gani? (*Makofi*)

Hawa Wazungu ukikaa nao wanatucheka, tunasafiri kila siku kwenda kutafuta misaada. Ukiangalia kiasi cha misaada ambacho tunakipata, ukalinganisha na kiasi ambacho tunakipoteza kama tungekusanya kodi, hii nchi ni nchi ambayo kodi haikusanywi, kuna ukwepajji mkubwa wa kodi. Ukiangalia Taarifa ya *IMF* wanasema kwamba, Tanzania inao uwezo wa kukusanya asilimia 21. (*Makofi*)

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naanza kwa kumshukuru Mungu, kwa kupata fursa hii ya kuzungumza ndani ya Bunge hili Tukufu ili nami nitoe mchango wangu juu ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba, tukitanguliza ushabiki, tutaumiza wananchi wetu na nchi yetu, lakini kabla ya kuzungumza nani aliyeanza ushabiki, tunajua tumejikwaa wapi. Kwa hiyo, tusiangalie tunakoangukia, tuangalie tulikojikwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Waziri; amewasilisha bajeti vizuri, pamoja na kwamba ni mpya, lakini amejitahidi sana maana mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Bajeti hii lazima izingatie uwiano wa maeneo yaliyotengwa kwa muda mrefu. Wakati mwingine lazima tuseme ukweli, baadhi ya maeneo ya nchi yetu kuna watu walitangulia kupata elimu, wengine wakatumia madaraka kwa kupendelea kwao. Kwa hiyo, safari hii tutazame na upande mwingine na hao hao walionufaika ndiyo wanaopita sasa kutukana watu wengine kwamba ninyi mko nyuma, ninyi

makondoo, wakati baba zao na wazee wao ndiyo waliopeleka mali za watu wengine kwao. (*Makof*)

Kwa hiyo, tuseme ukweli; hii nchi yetu sote, hatuwezi kukubali kitokee kikundi cha watu ambao tunajua wao ndiyo walikuwa watu wa kwanza kunufaika na uchumi wa nchi yetu tena wanapita kuwatukana wagogo ninyi kondoo; si ninyi ndiyo mliotuibia? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanazungumza vitu bila kuvifanyia utafiti. Jana msomi mmoja akasema hatuwezi kuwa tunazungumzia bajeti ile ile kila siku, majibu yale yale, tunarudia pale pale! Nimekwenda kuchukua Kitabu cha Waziri Kivuli cha mwaka jana, mambo ni yale yale yanafanana na kitabu cha mwaka huu. (*Makof*)

Sasa kwa nini mnawadanganya Watanzania? Chukua usome kitabu cha mwaka jana, ukurasa wa 11, Mheshimiwa Kabwe Zitto anasema: "Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa linaonekana kuongezeka kwa kasi ya ajabu sana na hivyo kupelekea Taifa kuwa na mzigo mkubwa. Deni la Taifa limefikia asilimia 38." Mwaka huu hiki hapa cha Mheshimiwa Kabwe Zitto, Waziri Kivuli wa Kambi ya Upinzani anazungumza tena anasema: "Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaonesha kuwa Deni la Taifa linaongezeka kwa asilimia 38." Halafu akaja kwenye mapendekezo, mwaka jana anasema anapendekeza tuunde Bunge likague na mwaka huu anasema anapendekeza Bunge likague; hakuna jipya. Kwa hiyo, kama tuna Upinzani wa namna hii ni dhahiri kwamba, hata ufanyaji vizuri wa Serikali utakuwa siyo sawa.

Mheshimiwa Spika, Bunge liliopita Wabunge wote tuliungana kwa pamoja tukasema baadhi ya Mawaziri wawajibishwe, Serikali ikawawajibisha. Tusipokuwa na Upinzani imara, msitegemee Serikali ifanye vizuri. Leo tunao Upinzani ambao ni *zilongwa mbali, zitendwa mbali*; kinachosemwa

kingine, kinachofanywa kingine. Tumeambiwa hapa jana kuwa, Kiongozi wa Upinzani alikataa gari hadharani, lakini kalichukua. Anakataa elfu themanini ya posho anachukua milioni mbili kila mwezi maana yake nini? (*Makofi*)

Maana yake ni kwamba, kinachosema kingine, yaani hawa jamaa usimung'anye wala usiteme ndiyo zao hao. Kwa hiyo, nataka tuanzie hapo. Kama wenzetu wanachokisema ingekuwa ni Waziri wa Serikali ndiyo kakosea, wangekomaa mpaka ajiuzulu. Komaeni Mbowe ajiuzulu kuwa Kiongozi wa Upinzani kwa makosa aliyoyafanya ya kuchukua gari ambalo alilikataa hadharani. Unajua Mwislamu safi ni yule anayesema hali nguruwe, lakini ukimwona anayesema sili nguruwe isipokuwa nakula maini ujue huyo hafai kwenye Uislamu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu lazima tuviseme. Leo hapa kuna watu wanashauri wanasesma nchi yetu imekwama labda watu wakiokoka; wakiokoka si wataiombea nchi sasa ndiyo kilimo kitakua? Kwa hiyo, pandisha ili waokoke waiombee nchi ifunguke, maana watu wakiokoka ndiyo nchi inabarikiwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kuwa sasa hivi uchumi uelekezwe kwenye maeneo yaliyoachwa. Hebu tuachane na hawa wapiga ngenga, maana watu wanataka kutumia Bunge kuwa jukwaa la propaganda. Unawezaje kusimama ukasema eti ooh, kikataeni Chama hiki, ikataeni Serikali hii; hapa hatupigi kampeni na ndiyo maana na sisi inabidi tutoe majibu sasa kwamba kikubalini Chama hiki, wale wengine wakataeni waendelee kusema maneno hayo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niishauri Serikali, kwenye suala la kuondoa VAT kwa viwanda vya ndani, hapa msifanye mzaha, hatutaki tena mama zetu na dada zetu wavae vitengeta vya mitumba; hilo hatulitaki. Kwa hiyo, ondoeni na sisi

tunawajua Serikali ni sikivu mtafanya. Leo hii kuna Wabunge wanafanya vitu vingine ni vichekesho, unazungumza halafu unasema siungi mkono. Bajeti hii imepangwa kwa kuzingatia mambo makubwa mawili, ndugu zangu niwakumbushe; imepangwa kwa kuzingatia mpango ambao Bunge hili liliupitisha, bajeti hii imepangwa kwa kuzingatia llani ya Uchaguzi wa Chama kinachotawala. (*Makofi*)

Itazame Bajeti ya Upinzani, haizingatii hata llani ya CHADEMA, hakuna sehemu wanayozungumzia elimu bure wakati walikuwa wananaadi kwenye majukwaa elimu bure, uwongo mtupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna sehemu bajeti yao inaakisi; mnatupiga changa la macho na wenzenu tunaangalia bwana? Hakuna sehemu ambayo bajeti yao...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde sijakusikia vizuri, hebu weka vizuri sijakupata.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu imepangwa kulingana na Mpango. Bunge hili limepitisha, inazingatia llani ya Uchaguzi ya CCM; leo Bajeti ya *Opposition*, haizingatii hata llani ya Uchaguzi ya Chama chao. Walipokuwa wakinadi walikuwa wanasema elimu watatoa bure, soma humu kama ipo, halafu wanachuo ooh, hawa makamanda, makamanda gani hawa hamna kitu. Suala hapa siyo kuvua gamba na kuvaah gwanda, suala ni kuvua gamba na kuvaah uzalendo, ndiyo suala la msingi ili nchi iweze kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Umeongea nini sasa kwa muda ...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyo anaitwa Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mbunge wa Mtera. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Mansoor; Mheshimiwa Shekifu? Mheshimiwa Mansoor? Wote wawili siwaoni, Mheshimiwa Ritta Mlaki atafuatia na Mheshimiwa Mohamed Mnyaa na Mheshimiwa Mabumba ajiandae.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Serikali yake kwa ujumla, kwa bajeti nzuri sana ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hali ngumu ya maisha, ukame na matatizo ya umeme, lakini bajeti imekuwa nzuri, imezingatia mambo yote ya msingi na kweli tunashukuru sana na tuko pamoja na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti hii, Serikali imetueleza hali halisi ya uchumi katika Mpango wake na vilevile jinsi ya kuboresha hali hiyo; tunaipongeza kwa hilo.

Tunapoongelea hali ya uchumi, tunatamka zaidi kuhusu Pato la Taifa (*GDP*), pato la wastani kwa mwananchi, mfumko wa bei, thamani ya shilingi yetu, mapato, matumizi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naupongeza sana Mpango wa Maendeleo uliowasilishwa; ni mzuri na ukitekelezeka, hakika hali yetu itabadilika. Nitajikita sana katika mfumko wa bei ambao umepanda na thamani ya shilingi na Pato la Taifa vimeshuka. Serikali imetueleza hali ya hiyo na mkakati wa kukabiliana nao. Nakubaliana sana na Serikali na hasa mkakati wa kuboresha miundombinu. Nina hakika nchi yetu na Watanzania wote watakulaliana na mimi kwamba, nchi yetu imefunguka, barabara zinapitika na maendeleo yanapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa uzalishaji umeme ambao tumeuona na wa reli umetufurahisha sana. Tunaomba Mungu, Serikali iweze kufanikisha. Napenda niishauri Serikali kidogo juu ya mkakati huu wa kupunguza mfumko wa bei. Tuongeze nguvu na msisitizo kwenye bidhaa tunazouza nje ya nchi yetu; ni kwa kuuza bidhaa zetu tu kwa wingi ndipo thamani ya shilingi yetu itaweza kuongezeka. Kwa sasa tunauza tumbaku, kahawa, korosho na bidhaa zingine za *cash crops*, lakini tunauza zikiwa ghafi; tungeomba Serikali isisitize kwamba tuuze bidhaa hizi zikiwa zimeshaongezwa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010/2011 nilichangia ninayoyasema sasa na ninahisi kama sijaeleweka, nitarudia mpaka nieleweke. Serikali tuwasaidie wakulima wetu na wenyewe viwanda, siyo kwa kufanya mazingira yawe bora tu ila tuwasaidie waweze kufanya kazi, tuwasaidie waweze kujenga viwanda, tuwapatie wataalamu, masoko, pesa na mikopo ambapo Serikali i-guarantee mikopo mbalimbali. Tusione kama Serikali itakuwa imefanya biashara ni Sekta Binafsi na haiwezi kufanikiwa bila Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulinde viwanda vyetu vya ndani, tushukuru sana viwanda vya nguo vilivyoko hapa nchini, tuna pamba, tunaomba sana kodi ya ongezeko la thamani iondolewe katika viwanda hivi vya nguo. Nitalifuatilia hilo kwa kuwa ni mdau ambaye napenda viwanda na nimesimamia kwa miaka mingi, naomba sana hilo lizingatiwe, *zero rated* katika viwanda vya nguo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwamba, miaka ya 70 Serikali ilianzisha viwanda kila sekta; dawa, kilimo, nguo, chuma, sabuni, *margarine*, mpaka na nyembe, tulikuwa tuna viwanda vyake tukabinafsisha vikafa. Vingi ya hivyo viwanda vimekufa. Sisemi tufuate mfumo huo kwa sababu Serikali haifanyi biashara, lakini angalau tuwasaidie hawa

wafanyabiashara, tuwasaidie *Private Sector* waweze kuanza, bila *economic base* ya viwanda, uchumi utakua taratibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kuwa, Serikali ikiona vitu havibadiliki au vinakwenda kwa kiwango ambacho hakiridhishi, kuwardhisha wao wenyewe, hebu tufikirie kubadili huo mfumo wa kufanya kazi. Ninaamini kabisa Mawaziri wetu, Watendaji wetu na Wataalamu wetu, wana akili na wanafanya kazi kwa bidii sana. Wote mnaowaona hapa ni wenzetu, wana akili sana, lakini bado lawama zinakuja nyingi sana mpaka tunawaondoa wengine. Wananchi wanachotaka ni maisha bora na maendeleo. Hawajali inafanyika namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninawaomba Mawaziri na Serikali kwa ujumla, hebu tazamani huu Mpango; Tume ya Mipango ikishaweka Mipango madhubuti kama ilivyotutolea kwenye hiki kitabu hapa, basi wamwachie Waziri *free hand* na Wizara yake watekeleze. Mfano, viwanda; nitarudia hapa kwa sababu ndiyo sekta ninayoifahamu sana. Msimpangie Waziri kwamba jenga Engaruka au fanya hivi; hiyo unafanya kutokana na bajeti. Apewe *free hand* uzalishaji uongezeké, aisaidie *private sector*; kwa mfano, viwanda kama viko 1,600 nchi nzima, viongezeke mpaka 3,000 imsaidie yeye aweze kuwasaidia wafanyabiashara kwa *ku-guarantee* mikopo, kuweka mazingira vizuri na Waziri atapimwa kwa utendaji wake. Wizara zote za kiuchumi mfano, Uchumi, Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Utalii, ziachiwe angalau basi kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nawasikitikia sana Mawaziri; kwa mfumo wa sasa, Waziri anaweza akaamka hapa anataka kwa mfano kuanzisha kiwanda fulani, *paper atakayoandika*; vikao vitaanza, itapitishwa *Cabinet Secretariat*, itakwenda *MTC*, ikifika kwenye *Cabinet*, imetobolewa na inaweza hata ikakataliwa. Kumbe angepewa Waziri mkono wake, mimi nimeongea na Mawaziri wengine hapa ndani, hata Mheshimiwa Profesa Tibaijuka pale, wanaweza

wakafanya mambo makubwa sana kwa nchi hii. Mheshimiwa Kigoda ni mtu mwenye akili nyingi sana, mwachieni afanye kazi; yaani nikiwa na maana kwamba, aungwe mkono. Mtu akileta wazo lake, atajua pesa atapata wapi; kwenye mikopo au kokote na atajua atawezekuifanya namna gani. Mfumo wa sasa kusema kweli, umewafunga mikono Mawaziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee suala la usafiri Dar es Salaam. Naipongeza sana Serikali, katika mpango wake wa kupunguza msongamano wa magari Dar es Salaam, barabara nyingi zimeondolewa Manispaa zimepelekwa kwa Mkoa sasa ili Serikali Kuu iweze kufungua. Watu tunaona, wananchi wanaona kule Goba, Madale, kutafunguliwa; tunaunga barabara kuu ili kuweza kusaidia.

Ninaomba sana kuwapongeza na wananchi, wanasubiri na wamefurahi kwa mpango ambao umeshasemwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninafanya kazi Dar es Salaam na Mkoa niliozaliwa ni Kilimanjaro. Wananchi wa Hai wanasema wanaishukuru Serikali; ukitaka kwenda kule mlimani, ukipita kila njia inakwenda mlimani sasa. Ukipita Sanya Juu kule, Boma Ng'ombe lami, ukipita kwa Sadala mpaka utokee kule Bwami lami, ukienda huku Marangu lami, wanafurahi sana. Ukienda kule Marangu, mpaka pale Mtoni, ukipita pale Himo lami. Serikali imefanya kazi, wanaomba pale Kiraracha napo pashughulikiwe, lakini kwa sasa kazi wamefurahia sana na wanashukuru mno. Wanaomba vilevile ile Barabara ya Shirimatunda kama unakwenda Bonite kule iwekewe lami. Pale Himo mpaka Makuyuni ndiyo hiyo wamenituma. Kule Vunjo naitwa mwali, mwali hii Barabara ya Himo – Makuyuni ije na lami na kule Hai ninaitwa mtoto wao. Naambiwa Shirimatunda iwekewe lami. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba vilevile niongelee wakulima wadogowadogo ambao wanalima mazao yao,

lakini wanakosa mahali pa kuuza au yanaoza baada ya muda mrefu. Mpango unaonesha hapa Serikali itajenga maghala, itaanzisha tena wauze korosho, mahindi na vitu kama hivyo kwenye Vyama vya Ushirika. Tungeomba iharakishwe ili iweze kuwasaidia. Wananchi wadogowadogo wanaolima mahindi kule Kilimanjaro, wanaomba sana waweze kusaidiwa na Mikoa ya Kusini kule kama korosho, wasaidiwe ili hili zao liweze kuendelea. Mama yangu pale ana shamba, analima mahindi yanaungana miaka mitatu bado yako ndani, wanakula watu wawili tu pale. Kwa hiyo, unakuta hawezikufaidika kwa zao lake ambalo analima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninapenda sana kuishukuru Serikali, ninapenda sana haya mawazo ambayo tumeyatoa tuyazingatie ili tuweze kuhakikisha kwamba pato linakua, shilingi inaongezeka kwa ajili ya *export* na vilevile mfumuko wa bei ambao kwa sasa kusema ukweli unaenda vibaya, uweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii na mimi kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mawazo yangu juu ya bajeti iliyowasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilidhani kwanza tuangalie mambo ya msingi ambayo tungeweza kuyachangia katika bajeti hii. Nilifikiria kwamba, bajeti yetu itazingatia ni namna gani itakavyowasaidia Watanzania wetu; ni namna gani itawasaidia wafugaji na ni namna gani bajeti yetu itazingatia kuwasaidia wavuvi wetu. Vilevile nilifikiria kwamba, bajeti yetu itawaangalia pia wafanyabiashara wadogowadogo, itaboresha vipi viwanda vyetu, itaboresha vipi reli zetu, itaboresha vipi barabara zetu, itaboresha vipi elimu katika nchi

yetu, itaboresha vipi afya na itazingatia vipi ule Mkakati wa Milenia ambao umetajwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kuangalia bajeti ya mwaka 2011 na ya mwaka 2012/2013, bajeti ya mwaka 2011 ililenga kuangalia hali ya kutaka kuboresha maisha ya Watanzania, lakini bajeti ya mwaka 2012/2013 imekuja katika mkakati huo huo. Tuangalie mfumko wa bei; katika bajeti iliyopita ilikuwa asilimia 19, leo kuanzia 2011 mpaka Aprili 2012 mfumko wa bei ulifiki asilimia 20 na sasa ni asilimia 18. Hadi kufiki mwishoni mwa mwaka 2011, upatikanaji wa chakula ulikuwa ni kati ya asilimia 12 hadi asilimia 26 na sasa ni asilimia 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wanatumia asilimia 50 kwa ajili ya chakula, lakini Sekta ya Kilimo imebakia kama msamiati na wakati ilikuwa Serikali ipeleke kipaumbele katika Sekta ya Kilimo. Leo tuna Sera ya Kilimo ni Utii wa Mgongo wa Taifa, lakini sasa tuna Sera ya KILIMO KWANZA; tuangalie kwenye Jedwali la 26 katika kitabu kinachoelezea hali ya uchumi mwaka 2010/2011 kilimo kilitengewa asilimia 9.2 wakati makubaliano ya nchi zote za SADC walikubaliana kwamba, kilimo kipewe angalau asilimia kumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maelewano yale hayakuzingatiwa na ndipo nikasema kwamba, Watanzania ni wazuri kwa kutoa maelezo katika vitabu. Vilevile takwimu zinaonesha kwamba, Watanzania 675,000 tu ndiyo wanaolipa kodi kati ya 40,000,000. Tuangalie tutaweza vipi kukusanya mapato kama watu wanaolipa kodi ni hao tu na hao ni Wafanyakazi wa Serikali. Wafanyakazi wa Serikali hawa ndiyo wanaolipa kodi kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie wafanyabiashara na wawekezaji hawalipi kodi, tuambiane ukweli. Kwa nini tukubali Tanzania kufanya dampo? Leo watu wanakusanya mali Tanzania wanapeleka kwao, Serikali haiko makini katika

ukusanyaji wa mapato. Serikali makini popote duniani, inasimamia ufanisi wa ukusanyaji wa kodi. Leo tumefutiwa kodi ya *cigar*; ni Waziri gani anayevuta *cigar* hapa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kujenga Taifa la jamii ya wachuuzaji bila uzalishaji.

Vijana wetu wengi wa Tanzania, wanatumiwa kuchuuza bidhaa kutoka nje ndani ya nchi yetu. Twendeni pale Kariakoo, twende Manzese, twende hata hapa Dodoma, twende Mwanza, mwone vijana wetu wanatumiwa katika hilo. Tungeweza kuwawezesha vijana wetu katika Sekta ya Kilimo tu, basi ninahakikisha kwamba, nchi hii ingeweza kukusanya mapato kwa kiasi kikubwa sana. Tulitegemea KILIMO KWANZA itakuwa chachu ya vijana kuzalisha, badala ya kufanya vijana hawa kuwa wachuuzi. Leo KILIMO KWANZA kinaendeleza ufsadi kwa kiasi kikubwa kwa kuwanufaisha wachache. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje Dodoma na Dar es Salaam, tuna matrekta pale yamekaa mithili ya bustani ya maua. Laiti kama matrekta yale vijana wangepewa elimu wakaweza kuyatumia na yakapunguzwa angalau ushuru, basi vijana wangeweza kuijendeleza kwa kiasi kikubwa na nina uhakika kama matrekta yale yangekuwa yanatumiwa na vijana wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje katika suala zima la umeme; Tanzania bado ni maskini wa nishati ya umeme. Kwa ufahamu wangu, katika Kitabu cha Hotuba ya mwaka jana, zilizungumzwa *mega watt* 60 kutoka Mwanza na bajeti ya mwaka huu zimezungumzwa *mega watt* 60 kutoka Mwanza, lakini mpaka leo upatikanaji wake hauonekani. Sasa ningeomba tunapozungumza jambo, basi lile jambo tulikamilishe ili liweze kuleta mema kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye Sensa ya Wafanyakazi. Mwaka 2011/2012, Serikali ilifanya sensa ya wafanyakazi hewa na iligundua kwamba, kuna wafanyakazi hewa ambao wamelipwa mishahara kwa kipindi cha muda mrefu. Sasa niulize; hivi waliohusika na malipo hewa hawajulikani? Kama wanajulikana Serikali ilichukua hatua gani juu ya watu hawa ambao walikuwa wakilipa mishahara hewa? Je, Serikali itatupa jibu gani kuhusu fedha za wananchi zilizotolewa kinyume cha Sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la mfumo wa Bajeti. Mwaka 2011/2012, Serikali ilitenga shilingi trillioni 4.9... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kombo. Mheshimiwa Sylvester Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, ajiandae.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja ambazo ziko mbele yetu. Naipongeza Serikali yetu kwa hotuba nzuri ambazo imeziwasilisha mbele yetu hapa na ndiyo maana leo kila mmoja ameweza kuwa na uelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ipo makini sana kwa sababu ina jukumu la kutekeleza kwa Watanzania. Ni ukweli usiopingika kwamba, kama mtu hana dhamana ya kufanya lolote, ataleta hoja yoyote ile kwa sababu anajua mwisho wa siku hakuna atakayemwuliza. Bajeti yetu inasimamia utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. Wenzetu wa upande wa pili, hawana jukumu ambalo baadaye tutakuja kuwa uliza hapa kwa sababu hawakupata *mandate* hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yetu imejielekeza katika mambo makuu yafuatayo:-

Kwanza, inatekeleza Dira ya Taifa ya 2025, inatekeleza Mpango wa Kupunguza Umaskini na inatekeleza Mpango wa Miaka Mitano tuliozindua *St. Gasper*. Kwa sababu hiyo, imejielekeza kuhakikisha kwamba, Watanzania wanakuwa na maisha bora. Hili linawezekana kwa kupitia Sera yetu ya KILIMO KWANZA, ambako tunaamini asilimia 70 ya Watanzania wako vijijini. Kwa hiyo, Serikali imelenga kuhakikisha kwamba, kilimo kinanyanya maisha yao na hivyo kutoa ajira kwa asilimia 70 ya Watanzania ili waishi katika maisha ya furaha na amani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile bajeti yetu inalenga kuhakikisha kwamba nchi hii inakuwa ya Utawala wa Kisheria. Tukifanya hivyo, wananchi watakuwa na heshima ya kulipa kodi kwa wale wenye viwanda, lakini pia wale ambaa ni wafanyakazi na wafanyabiashara watahakikisha wanalipa kodi ili Serikali iweze kutimiza majukumu yake. Bila ya Utawala wa Kisheria, hii nchi haiwezi kwenda. Kwa hiyo, naipongeza Serikali yetu kuona kwamba, lengo la kuwa na Utawala wa Kisheria ndani ya nchi hii, linasimamiwa kupitia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Bajeti yetu imelenga kujenga uchumi wenye ushindani. Hili linawezekana kwa sababu leo hii Serikali yetu imesema kwamba, itaweka kodi kwa bidhaa zinazotoka nje ili kuhakikisha viwanda vya ndani vinajengwa na kuweza kutoa ajira na hatimaye vijana wetu wengi kupata mapato. Sekta Binafsi ambayo tutaifutia kodi, itaweza kuongeza Pato la Taifa na vilevile kuweza kupata fedha za kigeni baada ya kuuza nje. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa maamuzi hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa wanaposema bajeti hii haina mashiko; mashiko ni yepi ambayo tunataka tuyaoone hapa kama Serikali imeamua kuvifutia kodi viwanda vya ndani ili viweze kuzalisha na kuweza kuhimili ushindani? (*Makofii*)

Mwenye macho haambiwi tazama, tumeona kila sehemu Serikali yetu imefungua Vyuo vya VETA, lengo lake ni kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata *skills* na hivyo kupata ajira katika Sekta Binafsi. Serikali haiwezi kumwajili kila mmoja, lakini kupitia Vyuo vya VETA, Watanzania wengi wataweza kujiajiri wenyewe. (*Makofii*)

Bajeti hii itahakikisha kwamba, vijana hawa wanapatiwa vifaa ambavyo baada ya kumaliza katika Vyuo vya VETA wataweza kuanzisha shughuli za uzalishaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowaomba Wabunge wote humu ndani, tuisaidie Serikali kuishauri kwa makini, kupiga makelele hakusaidii, tutoe hoja za msingi ambazo Serikali yetu itaweza kuzizingatia. Sisi kazi yetu ni kuisaidia Serikali yetu, kuionesha mahali gani panahitaji kuangaliwa siyo kuja na kelele ambazo mwisho wa siku Serikali itakuwa hajafahamu nini imekusudia ifanye. (*Makofii*)

Serikali yetu imeweka wazi kwamba, miundombinu ya barabara, reli na bandari, lazima iendelezwe na hivi ni vichocheo vya ukuzaji uchumi. Tunajua tuna fursa kubwa, tukiimarisha reli zetu, bandari zetu na barabara zetu hasa kwa sababu kuna nchi majirani ambao wametuzunguka wako *land locked*, hawana *access* ya bahari, kwa kujenga reli zetu; Reli ya Kati na Reli ya TAZARA na barabara zetu na Bandari ya Dar es Salaam, tutaweza kuhimili ushindani wa majirani zetu na hivyo kuimarisha uchumi wetu. Kwa hiyo, bajeti hii naomba sana tuiunge mkono ili Serikali iweze kutimiza azma yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwamba, tuliomo humu ndani timesomeshwa kupitia Serikali ya CCM na ndiyo maana kwa sababu bahati nzuri sana hajatokezea Chama tofauti na CCM toka mwaka 1961, ingelikuwa sumu inaonjwa tungejaribu kuwapa hawa wenye bajeti ambayo

haitekelezeki, yenyе kuwafurahisha Watanzania, tukiwapa jukumu watakuja na *excuse* nyingi sana kwamba unajua ilikuwa Watanzania hawataki maneno hayo. (*Makofi*)

Watanzania wanataka utekelezaji na Bajeti hii ya CCM, ndiyo ambayo ina majibu kwa shida za Watanzania. (*Makofi*)

Leo hii sehemu ya Tanzania kuna Chuo Kikuu, maana yake nini? Ukiangalia *Open University* imeanzisha matawi yake kila mkoa na Watanzania wengi wame-access elimu hii na tukiangalia humu ndani Wabunge wengi ni *graduate* wa *Open University*.

**WABUNGE:** Ahaa, ndiyo imewawezesha kuwa na uono wa macho kwamba bajeti iko vipi. Kwa hiyo, tuishukuru sana Serikali ya CCM kwa kutusomesha Watanzania. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Na wewe shukuru.

Sehemu ya Sekta ya Afya, Serikali yetu iko macho inajua umuhimu wa Watanzania wenye afya njema ili waweze kushiriki katika shughuli za kiuchumi; ndiyo maana imekizingatia sana kilio cha madaktari. Nawaomba sana tuache kupeleka maneno ya kuchochea madaktari wetu wafanye migomo. (*Makofi*)

Naomba pia tuwasaidie sana walimu wetu, tusiwape matumaini ambayo yako hewani. Fanya bajeti yenyе kutekelezeka, usije na bajeti ambayo mwisho wa siku utakuja na sababu za kuomba radhi. Sisi tuko makini kuhakikisha kwamba bajeti yetu inatekeleza mahitaji ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie kuhusu mgawanyo wa bajeti yetu kwamba, bajeti ya matumizi iko juu kuliko ya maendeleo. Bajeti yote imepangwa kiutaalam kwa sababu leo hii wanaosema kwamba bajeti ya matumizi iko

juu kuliko ya maendeleo, yote imepangwa kiutaalam kwa sababu leo hii wanaosema kwamba bajeti ya matumizi ni kubwa na hawa hawa tusipowalipa mishahara mizuri watakuja. Kwa hiyo, bajeti inahakikisha kwamba, tunawapa *morale* wafanyakazi wetu kwa kuwapa mishahara mizuri, itakayokidhi maisha yao na familia zao ili *waji-engage* vizuri kwenye uzalishaji. Kwa hiyo, hili ni jambo la kuungwa mkono na kila mmoja wetu hapa. Tungelikuja na bajeti kubwa ya maendeleo peke yake tukasahau mishahara na mahitaji mengine, hawa wangepiga kelele; unaona mishahara iko chini! Leo wamekuja na *budget proposal* ya mshahara ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sylvester Mabumba.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Ya ngapi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Sasa ni Mheshimiwa ...

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Mnyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Nyangwine.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote, kwa kuwa sipo Dar es Salaam na kuna msiba wa Mhariri wa Gazeti la Jambo Leo, ningeomba kuungana na Wanahabari popote walipo kwenye msiba huu mzito na ninawapa pole. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tangu awali kwamba siungi mkono hoja iliyoko mbele yetu na naunga mkono mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Siungi mkono si kwa sababu ni Mbunge wa Upinzani bali kwa sababu Wabunge wote kwa pamoja tulikaa hapa Bungeni tukapitisha

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Serikali kupitia Bajeti hii, haijatekeleza huo Mpango kama nitakavyoelezea. Kwa hiyo, sina sababu ya kuunga mkono Bajeti iliyoko mbele yetu. (*Makofi*)

Kuna mambo mengi yamesemwa na yakanikumbusha kisa kimoja kule Manzese kijiweni; kule Uswahlilini kuna bafu fulani mtu akiwa anaoga anaweza akaja mtu akachukua taulo akakimbia nalo. Sasa ukitoka kumkimbiza yeze anaweza akawa ni chizi halafu wewe unayemkimbiza ukaonekana chizi zaidi. (*Makofi*)

Sasa nilikuwa nasikiliza majadiliano, kuanzia jana kuna hoja zilikuwa zinatolewa kwa kweli nikianza kuzungumza moja baada ya nyingine nitageuka kuwa chizi. Kwa hiyo, ningedhani kwamba, niache machizi waendelee na uchizi wao ili niweze kuzungumza mambo ya msingi yanayohusu maendeleo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, nakuomba sana, una uhuru wa kuchangia, lakini si haki kabisa kumwita Mbunge mwenzio mwengine yeyote yule mwenye mawazo tofauti na ya kwako kuwa ni chizi. Kwa hiyo, naomba ultoe neno hilo halafu uendelee kuchangia.

Vilevile nitoe onyo kwa mara nyingine, namsikia Mheshimiwa Mchungaji Msigwa na wengine, ninapotoa mwongozo hapa ni kwa ajili ya uendeshaji bora wa Kikao cha Bunge wala si kumwonea mtu yeyote yule.

**WABUNGE FULANI:** Endelea, Mheshimiwa Lusinde, ameongelea upuuzi hapa hujasema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa John Mnyika endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, ulikuwa na zamu ya kuongea lakini kabla hujaendelea, ninaomba nichukue Kanuni yangu nikae nayo hapa karibu, kwa kutoa onyo kwa mara nyingine tena na mara ya mwisho na kwa uhakika kabisa na nawaomba Wananchi wa Iringa Mjini kupitia Mbunge wao, Mheshimiwa Mchungaji Msigwa; ni vizuri kuwa na nidhamu katika Vikao vya Bunge. (*Makofi*)

Hiki ni kikao kikubwa, lazima tuheshimiane, sisiti hata kidogo kuchukua hatua sasa hivi. Kwa hiyo, nakuonya kwa mara ya mwisho, habari ya kuropoka kwa wakati ambao hujapewa nafasi ya kuzungumza siyo sawa.

Kama una jambo simama nitakupa nafasi utazungumza, anayezungumza ni Mheshimiwa Mnyika; nimemkataza kumwita Mbunge mwingine yejote yule chizi na hiyo nafuata utaratibu siyo ya kupanga mimi. Mheshimiwa Mnyika toa hilo neno halafu endelea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba nieleze maana ya nililoeleza maana jana wengine tuliiitwa tuna vichaa hapa.

**NAIBU SPIKA:** Hatubishani, naomba utoe hilo neno halafu tuendelee kwa sababu jana sikuwepo hapa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba nielezee maana ya neno chizi nilikuwa naamanisha nini halafu niendelee kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, ama unatoa hilo neno unaendelea kuchangia au basi haina maana ya kuendelea kuchangia, hayo ndiyo maelekezo ya kitu.

**WABUNGE FULANI:** Toa tu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya hizi dakika zangu nitaomba nitoe hilo neno ili niweze kuendelea kuchangia.

**NAIBU SPIKA:** Sawa sawa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naendelea kusema kwamba, kuna mambo yamesemwa kwamba bajeti hii inatekelezeka. Nimesoma llani ya CCM na Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano kwa kina kabisa na kwa niaba ya Wananchi wa Ubungo walionitura kuwawakilisha hapa, wenyewe matatizo makubwa ya maji, pamoja na kuwa nimekwenda Mtwara na kwingineko nimekuta wenyewe shida ya maji kuliko Ubungo, lakini nimefungua kabrasha hili la bajeti nimeangalia ukurasa wa 93, Miradi ya Maji imetengewa shilingi bilioni 187 wakati naelewa mpango uliopitishwa na Baraza la Mawaziri ulikuwa ni wa shilingi bilioni 600 na naelewa nini kilichopo kwenye llani ya CCM. Bajeti hii haitekelezi llani ya CCM wala haitekelezi Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. (*Makof*)

Nimepitia makabrasha ya Bajeti yanayosema kwamba, inatekeleza llani ya CCM, sijui kuhusu barabara kuna Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. Kuna msemo unasema mzimu uko kwenye maelezo, yaani ukichambua maelezo humu ndiyo unaweza ukajua mzimu uliopo kwenye hii bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utaona hilo ni neno gumu, niliseme kwa Kiingereza ili lieleweke; *the devil is in the details*, yaani mzimu umo humu kwenye maelezo. Ukisikiliza maelezo ya hotuba unaweza ukadhani kwamba, zile barabara za kupunguza foleni Dar es Salaam sasa zitajengwa, orodha imetajwa. Ukija kwenye Vitabu vya Bajeti, barabara zote za kupunguza foleni, kifungu kinachoitwa *Decongestion Dar es Salaam*, kwa ajili ya muda sitasoma kifungu kwa kifungu, zimetengewa bilioni kumi peke yake, kinyume na llani ya CCM na kinyume na Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano. (*Makof*)

Kwa hiyo, lugha zote zinazozungumza sijui llani za CCM, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano, ndiyo maana tunafikia kusema maneno mengine inakuwa kama ya uchizi uchizi hivi kwa namna yanavyozungumzwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo yamezungumzwa kuhusu Hotuba ya Kambi ya Upinzani kwamba; kwanza, ina mambo yasiyotekelvezeka; pili, Kambi ya Upinzani haitekelezi hata mambo yake na ikasemwa haina maana na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme mambo kadhaa ya msingi; limezungumzwa suala la pensheni ya wazee, sisi tumezungumza kwenye bajeti iliyopita, ndiyo maana nawashangaa wanaosema tumerudia, tumezungumza kwenye bajeti iliyopita, Serikali haikusikia tukazungumza inatekelezeza namna gani. (*Makofi*)

Bahati mbaya Wabunge wa CCM, sijui hata mnasahau kauli za Viongozi mnasema suala la pensheni ya wazee halitekelezeki, halafu Waziri Mkuu Mizengo Pinda, mwaka 2010 pale Morogoro, aliwaambia Wazee wa Tanzania kwenye Siku ya Wazee kwamba, tunakwenda kutoa pensheni ya wazee halafu mnasema haitekelezeki. (*Makofi*)

Tukisema kwamba watu wanazungumza mambo ya kiuchizi tunaamanisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, humu inasemwa kuhusiana na kima cha mishahara, kwa sababu ya muda sitaingia kwenye takwimu. Serikali ina wafanyakazi wangapi? Hoja hii ilishakuja Bunge liliopita, tuliposema kima cha chini ni shilingi laki tatu na kumi na tano ikasemwa haitekelezeki, tukaeleza kwa mifano na takwimu namna gani inavyotekelvezeka. Tunashangaa wapofu wa kumbukumbu leo wamesahau mambo ambayo yako kwenye Kumbukumbu za Bunge. Wakasome watekeleze

tuliyoamua, tumeyarudia kwa sababu hayajatekelezwa tunataka Serikali itekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitishwa na jambo moja kubwa sana na tumefika hapa tulipo kwa sababu ya udhaifu wa Rais Kikwete na nasema hivi; udhaifu wa Rais, tumefika hapa tulipo, kwa sababu ya uzembe wa Wabunge na Bunge. (*Makofi*)

Nayasema haya nikimaanisha tumefika hapa tulipo kwa sababu ya upuuzi wa CCM. Nikitakiwa kuleta ushahidi nitaelezea kwa nini nasema hivyo. Tunahangaika sasa hivi kuhusu Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano kwamba hauzingatiwi! Mtakumbuka kwamba, kwenye Bunge hili hili nilisema kwamba kwa mujibu wa Kanuni zetu za Bunge, Kanuni ya 94 inasema kwamba, kwenye Bunge la mwezi Februari, ndiyo Bunge linatakiwa kukaa kama Kamati ya Mipango kuhusu Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na kuhusu Mpango wa Mwaka wa Serikali. (*Makofi*)

Tukalumbana hapa tujadilini Mipango, tuweke vipaumbele, tufanyeje, ikaonekana kama mambo haya hayana umuhimu, badala yake tukaenda kuyajadili kwenye semina. Leo tunaletewa Mpango tunasema haufai, Mpango haujazingatiwa na kila kitu, lakini tulikuwa na wakati wa kufanya hivyo na ndiyo maana nasema kwamba, Mheshimiwa Naibu Spika, natumia maneno makali lakini naamini kuna hitaji la kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa mujibu wa Katiba yetu hii mbovu... (*Makofi*)

## KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumkumbusha Mheshimiwa Mnyika na Wabunge wengine wa aina hiyo, kila mara nimekuwa nasema kuwa, Kanuni ya 64 inakataza kabisa; siyo suala la hiari wala mtu kuamua, ukishafika humu ndani kuna mchezo wa humu ndani na mchezo wa magengeni, hapa ni Bungeni. Kanuni ya 64(d) inasema; Mbunge yejote hatatumia Jina la Rais kwa dhihaka. (*Makof!*)

Katika mjadala, Mbunge yejote hatatumia Jina la Rais tena kwa kutaja na jina lake ndiyo mbaya zaidi. Hatatumia Jina la Rais kwa dhihaka katika mjadala au kwa madhumuni ya kutaka kulishawishi Bunge kuamua jambo lolote kwa namna fulani. Ukienda zaidi ya hapo, hatatumia lugha ya kuudhi; yako mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ya kwamba, Rais Kikwete kwa jina lake, maana yake tunajua Rais ni *institution*, Rais ana Serikali, Rais Kikwete ni dhaifu, CCM ni upuuzi! Sasa naomba Mheshimiwa Mnyika, katika watu ambao nawaheshimu sana siyo kwa dhihaka, kwa ukweli kabisa wanaozungumza kwa kufikiri ni pamoja na Mnyika, nadhani hili umepotoka mdogo wangu. Kwamba, kwa kutokuangalia hii Kanuni ningombaa afute maneno yake haya, siyo kwa hiari yangu mlimi kwa hiari ya Kanuni ya 64, kifungu cha (d), kwanza kumtaja jina lakini kwa kutumia jina lake kwa dhihaka.

**NAIBU SPIKA:** Ni kweli ambacho anakisema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Kanuni hiyo ya 64(d) inajieleza vizuri na siyo tu kwamba katika maneno amemsema vibaya Mheshimiwa Rais isivyotakiwa, lakini pia amelisema vibaya Bunge hili katika lugha isiyopaswa. Kwa hili ambalo amesimama Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nakuomba Mheshimiwa Mnyika ili uendelee kuchangia, ufute na ultoe neno hilo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ungenisikiliza au Bunge lingenisikiliza kwanza niliposema udhaifu wa Rais namaanisha nini.

**NAIBU SPIKA:** Nimesema ultoe neno hilo ili uendelee kuchangia kama unataka kuendelea kuchangia.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili neno udhaifu wa Rais sitalitoa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendeshwa kwa taratibu na kwa kuwa mimi ni Naibu Spika wa uhakika, lazima nihakikishe kwamba taratibu zinafuatwa. Kanuni ya 73(2) inasema ifuatavyo:-

“Endapo Mbunge au Waziri atatumia maneno au lugha isiyotakiwa Bungeni, yaani lugha ya matusi, lugha ya uchokozи au lugha ya maudhi na akitakiwa na Spika ajirekebishe kwa kufuta maneno au lugha hiyo akakataa kufanya hivyo, Spika anaweza kumwamuru Mbunge huyo atoke mara moja nje ya Ukumbi wa Bunge na abaki huko nje kwa muda wote uliosalia wa kikao cha siku hiyo.”

Kanuni ya 73(3) inasema: “Endapo Mbunge yejote atatakiwa kuthibitisha ukwelli wa maneno aliyojasema na hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa amekataa au ameshindwa kutoa uthibitisho huo, Spika anaweza kumsimamisha Mbunge huyo asihudhurie Vikao vya Bunge visivyozidi vitano. (*Makofi*)

Kwa hiyo sasa, hiki kifungu cha tatu nakiacha, lakini kifungu cha pili; kwa kuwa nimekutaka ufute kauli hiyo na hujataka kuifuta, uamuzi ninaotaka kuuchukua sasa na kumwambia *Sergeant at Arms*, yaani Askari wangu mliomo humu ndani, mara moja mhakikishe kwamba Mheshimiwa John Mnyika anatolewa nje ya Ukumbi wa Bunge na abaki huko

hadi kesho saa tatu asubuhi. Naomba jambo hilo litekelezwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mnyika *out!*

(*Hapa Mheshimiwa John J. Mnyika Alitolewa Nje ya Ukumbi wa Bunge*)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na uchangiaji, anayefuata ni Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika kikao hiki cha bajeti kinachoendelea.

Kwanza kabisa, nasikitika kuona watu wazima wenye akili timamu, tunafanya mambo ya ajabu kutukana Viongozi wa Serikali, ni upuuzi ambao hauwezi kuvumilika. Tunachotakiwa kukifanya ni kufahamu kwamba, hii nchi yetu ni ya Tanzania, tumezaliwa Tanzania na kila mtu ana haki lakini siyo kuwadanganya Watanzania kwamba mkinipatia hiki nitafanya hiki na kile. Ndugu zangu, mmeshindwa kunadi Sera zenu ndiyo maana mlishindwa. Haiwezekani msomi mzima aliyesomea uchumi anasema kwamba, ataongeza mshahara wa wafanyakazi kima cha chini kiwe shilingi 315,000; kwa bajeti ipi ya trilloni 15? Acha kuwadanganya Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Naomba nisisitize; *Sergeant At Arms*, nilipomtoa Mheshimiwa Mnyika, mnatakiwa kuhakikisha anatoka mpaka nje ya Geti la Bunge. (*Makofi*)

Narudia tena, *Sergeant At Arms*, hakikisheni mnamsindikiza mpaka nje ya Geti la Bunge.

Mheshimiwa Nyangwine endelea.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, umekula dakika zangu kama tatu hivi.

Mimi naamini kabisa kwamba, ndugu zangu, tukiendeleza uzalendo wa kuitetea nchi yetu, basi Watanzania tutafika lakini tukikaa na kuwalaghai Watanzania kwa kudandia hoja ambazo zimeshajadiliwa na Chama cha Mapinduzi unakuja kuzileta huku hadharani kusema haisaidii kitu, ni unafiki na jambo kama hili haliwezi kuvumilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, mimi naamini Wananchi wa Tarime na Watanzania wenzangu wanafahamu; nina ushahidi, Wananchi wa Tarime walitoa karibu mihula miwili kwa chama hiki kuongoza kule Halmashauri na Jimbo, hakuna kilichofanyika hata kidogo zaidi ya kupigana na matusi kila siku; unafiki mkubwa huo.

Baada ya kusema hayo, naomba niingie kwenye kuchangia Bajeti ya Serikali. Naamini kabisa kwamba, hata kama mtasema kwamba mtakuja lakini Wananchi wa Tarime wanafahamu hamtaambulia chochote kile, mtaambulia sifuri tu na wala msihangaike. Ninaamini kabisa kwamba, Sera zenu haziuziki ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha ongea na mimi.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Baada ya kuyasema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye Bajeti. Mimi nafahamu kwamba, tunachokipigania sisi Watanzania na wanaotusikiliza kokote kule ni namna gani tutatumia rasilimali tulizonazo ili kuiendeleza nchi yetu.

Kwa kweli tuna changamoto kubwa sana ambazo tunashindwa kuzielewa; ni kwa nini sisi Watanzania hadi hapa

tulipo ni maskini; naumaskini wetu unasababishwa na nini? Haya ni mambo ambayo tunahitaji mjadala wa Kitaifa bila hamaki, bila itikadi ya chama chochote kile, kwa kila Mtanzania mwenye uzalendo. Kuna mambo kama yale kwamba; je, Sekta ya Madini katika nchi yetu inalinufaishaje Taifa? Tuna hifadhi, mbuga na vitu vingi kama mito, maziwa na mabonde ya kila aina, tunatumia rasilimali hizi kulinufaishaje Taifa letu? Hayo ndiyo mambo ya msingi ambayo nafikiri kila Mbunge aliyepo hapa akija na hoja kama hiyo na kuielekeza Serikali ifanye nini tutaweza kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni kwamba, Serikali isitegemee kuongeza mapato kwa kutumia pombe na sigara. Kwa kweli hilo mimi siliungi mkono, tuachane nalo lakini tuangalie ni namna gani tutatafuta vyanzo vyta kuongeza mapato ya Taifa kwa kutumia rasilimali tulizojaliwa nazo. Tuna Sekta ya Madini ambayo ni muhimu sana tukaitumia na ikawakomboa Watanzania wanaoishi katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kabisa kwamba, katika nchi yetu ya Tanzania, aidha matumizi yanakuwa makubwa sana kuliko Mipango ya Maendeleo, ndiyo maana tunashindwa kuendelea. Mimi napendekeza kwamba, ikiwezekana tutumie rasilimali tulizonazo lakini pamoja na hayo tubane matumizi. Tunatumia mashangingi makubwa sana Serikalini, unaweza ukakuta Wizara moja ina mashangingi zaidi ya mia moja na yamenunuliwa kwa zaidi ya shilingi milioni 200 na wakati huo huo gharama ya kuyaendesha kwa mwezi inaweza ikafikia shilingi milioni kumi. Kwa hiyo, inawezekana kabisa kwamba, Serikali tuna nia nzuri ya kuwasaidia Watanzania, lakini tupunguze matumizi ya Serikali, tutumie magari ambayo yanaweza kutumia mafuta kidogo kama Prado kuliko kutumia mashangingi. Hilo nafikiri linawezekana.

Jambo lingine ambalo tunaweza kulitumia ni kwa wahujumu uchumi wa nchi, bila kuangalia itikadi, kabilia wala dini, napendekeza kwamba tuamue kama nchi au hata Bunge

hili tutunge sheria kwa wanaohujumu uchumi wa nchi, yaani wanaoiba fedha za Serikali tuwafanye nini, hata ikiwezekana tuwanyonge ilimradi tutunge sheria, hilo linawezekana kabisa tukafanikisha. Hilo ni jambo ambalo tunaweza kulitumia tukafanikisha kuliko kuacha baadhi ya watu wananaufaika lakini wengine wanaendelea kukaa katika lindi la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba kuisemea Bandari ya Dar es Salaam. Katika Bajeti hii sijaona sehemu ambayo kuna mkakati mahususi wa kuiboresha Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kuliingizia Taifa pato kubwa sana, badala yake Bandari ya Dar es Salaam inatumiwa na watu wajanjawanja tu kama Wahindi wananaufaika lakini Watanzania wanaumia. Hilo jambo lina ubaguzi katika nchi yetu na hatuwezi kulivumilia.

Kwa mfano, unachukua mizigo inayokuja bandarini inapelekwa kwenye bandari ya nchi kavu ambapo Wahindi wana magodauni yao wanatunza mizigo. Ukifika kule Mhindi anachukua *exchange rate* ya dola 1,800 badala ya shilingi 1,560; kwa hiyo, huo ni ubaguzi ambao katika nchi hii hatutaweza kuuvumilia na sanasana tuangalie ni namna gani tutawawezesha wazalendo kuwaonesha kwamba wanamiliki uchumi wa nchi.

**MBUNGE FULANI:** Hiyo ni lugha ya kibaguzi.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Siyo lugha ya kibaguzi, nimesema tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumaliza hapo, naomba kujadili kuhusu fedha za rada. Hizi fedha za rada zimerudishwa na tulipanga ndani ya Bunge hili, tena Mheshimiwa Mkuchika wakati huo akiwa Waziri wa TAMISEMI alisema kwamba, hizo fedha zitakwenda kununua madawati katika Halmashauri zetu nchi nzima. Sasa hivi kuna mambo ya ujanjaujanja tu yanafanyika; mara ziende kwenye vitabu bilioni

55, mara bilioni 27 ziende kununua madawati katika Halmashauri tisa! Sasa jambo la kuuliza Watanzania kama kweli tupo *serious* na kuwatetea Watanzania na kuwaletea maendeleo, kama Waziri alisimama akasema kwamba hizo fedha zitakwenda kununua madawati lakini matokeo yake zinatakiwa kwenda katika Halmashauri tisa; hilo jambo hatulikubali bali tunataka huo mgawo ugawanywe kwa watu wote katika Halmashauri zote za Tanzania na hata Zanzibar kwa sababu Wizara ya Ulinzi ni ya Muungano na zile fedha zimetokana na rada, hakuna sehemu katika mgawo ule Zanzibar imeoneshwa. Mimi nawashauri mjipange upya na Zanzibar ipate mgawo kutokana na zile fedha za rada. (Makof)

Suala la MKURABITA, MKUKUTA na Mpango wa Maendeleo, namwomba Waziri anayehusika aje na hoja ya kujibu kwamba vinawanufaishaje Wananchi wa Tanzania au ni katika maandishi tu? Kitu kama hicho tutakuwa hatuwatendei haki watu wetu wa Tanzania.

Mwisho, ni namna gani ya kuboresha utalii katika nchi yetu ya Tanzania. Naomba hili suala tulizingatie kwa sababu tuna Mashirika kama TANAPA, TTB na Mamlaka ya Ngorongoro, matokeo yake tumeachia TTB ndiyo inatangaza utalii na wigo wa TTB kutangaza utalii katika nchi ya Tanzania ni mdogo mno. Tunaomba utaratibu, kila taasisi iliyopo katika Wizara ya Maliasili na Utalii iruhusiwe kutangaza utalii yenyewe, TANAPA itangaze ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nyangwine Chacha Mariba, ahsante sana. Sasa ni Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Said Jaffo. Mheshimiwa Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Yapo mambo nitakayoyasema yatakayonifanya nichelewe kuunga mkono hoja hii.

La kwanza, kuna kazi za maendeleo ambazo zipo Vunjo kama barabara ya lami ambayo Serikali imeahidi tangu mwaka 2010 kuanzia Marangu Mtoni kwenda Kilema Kaskazini kwenda Kiruavunjo Magharibi mpaka Kawawa. Pili, kuna suala la usambazaji wa maji safi ya kunywa Mji wa Himo. Tatu, kuna ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Himo. Nne, kuna Barabara ya Kilema Pofo - Kilema Hospitali Uchira mpaka kwa Ralia.

Nimemua kuyataja haya kwa sababu tumekuwa tunagombana na Serikali kuhusu maendeleo ya Jimbo la Vunjo, Miradi inasuasua tatizo fedha hakuna. Tulipokuwa tunakagua hesabu za Serikali za Mitaa tumegundua mambo yafuatayo:-

Kwanza, hata fedha zinazoidhinishwa na Bunge hili kwa mfano mwaka 2011, Halmashauri zilizopo ni 134; fedha ambazo zilipaswa kupelekwa ambazo ziliidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 164 lakini zilizopelekwa ni shilingi bilioni 130, kasoro shilingi bilioni 30 kwa Halmashauri 18. Maana ni kwamba, hata fedha tunazoidhinisha hapa haziendi ni kama tunaidhinisha fedha hewa. Sasa nikiunga mkono nitakuwa na uhakika gani kwamba hizi tunazoldhinisha safari hii zitakwenda zote? Maana mwaka 2010/2011 fedha zilikwenda kasoro asilimia 20, kwa hiyo, wakinihakikishia kwamba fedha zitakazoidhinishwa na Bunge hili zitakwenda zote kwenye Halmashauri za Wilaya kutengeneza barabara, kusambaza maji na kujenga shule, pengine nitafikiria upya.

La pili, hata zile fedha ambazo zinatakiwa ziende wanazichelewesha mpaka *quarter* ya mwisho. Kwa mfano, mwaka 2010/2011 kufikia Juni 30, 2011 zilitakiwa ziende shilingi bilioni 545 lakini fedha zilizokwenda kwa wakati mwafaka ni shilingi illioni 342. Kwa hiyo, fedha ambazo hazikwenda, yaani

hazikutumika ni shilingi bilioni 174.5. Sasa, nitaunga mkono kama fedha tutakazoidhinisha hapa zikapangwa kwenda kwenye Halmashauri zitakwenda kweli na hii ni *trend* ambayo nimeiona kwenye Serikali. Mwaka 2007/2008 kiasi cha asilimia 20 ya fedha hazikwenda kwa wakati mwafaka na hazikutumika, mwaka 2008/2009 na mwaka 2009/2010 hazikwenda kwa wakati mwafaka. Kwa hiyo, Miradi iliyopangwa kwenye Halmashauri haikutekelezwa na kama imetekelizwa basi haikutekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa.

La tatu, nitaunga mkono kama nitathibitishiwa kwamba fedha tutakazoidhinisha hapa hazitaporwa na wezi na mafisadi kwenye Halmashauri. Mwaka 2010/2011, tulitoa mfano ya Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, fedha zilizopelekwa ni shilingi bilioni 6.7 lakini zilizotumika hakuna, karibu fedha zote zimekwenda kwenye Mifuko ya Wafanyabiashara wa Kishapu, Watumishi wa Benki ya Kishapu na Watumishi wa Halmashauri. Sasa tutakuwa na uhakika gani sisi Wabunge kweli tukiidhinisha fedha hizi Serikali ina mkakati gani wa kuondoa huo wizi kwenye Halmashauri zetu; na wale wanaoiba hizi fedha au wananchi walioibiwa kwa mfano wa Kishapu na kule Vunjo nani atawafidia?

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwafidia kwa fedha zilizopelekwa lakini zikaibiwa, zikaliwa na zikatumika? Pale Vunjo kuna mfereji wa Ndekombeka na Faru, tulikwenda kukagua, kweli fedha zile zimetafunwa lakini wale watu hawajakamatwa mpaka hivi sasa, yule mkandarasi hajakamatwa na kushtakiwa na wala wale viongozi walioiba zile fedha kwenye kile Kijiji hawajakamatwa wala hawajashtakiwa ingawa kuna *report* ya CAG kwamba watu wale wakamatwe na washtakiwe.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, hakuna mtu anayekataa hii bajeti, lakini yapo mambo mengi ambayo lazima Serikali ituhakikishie sisi ambao tupo hapa kwa niaba ya

wananchi walio tuchagua kwamba, tukiidhinisha hizi fedha kwa mfano ile barabara yangu ya Kiruavunjo kuja Marangu Mtoni itajengwa. Maana haikujengwa tangu mwaka 2010 mpaka leo tatizo tuna ambiwa fedha hazitoshi, bajeti haitoshelezi; itatosheleza lini? Je, Barabara ya Kilema Pofu kwenda Kilema Hospitali itajengwa? Mkini hakikishia mimi sina mgogoro, ninachotaka wale watu wangu walionitura waone kazi zao walizoniagiza ninazitekeleza. Ile Barabara ya Uchira kwenda Kaloleni mpaka kwa Laria je fedha zipo? Nionesheni zipo wapi hapa kwani sina mgogoro na ninyi.

Je, ule usambazaji wa maji tena Rais mwenyewe aliagiza kwamba tukimchagua atasambaza maji safi ya kunywa Himo; tangmwaka 2010, 2011 na sasa ni mwaka 2012 kama hizo fedha sizioni nitaidhinisha nini jamani? Nitaunga mkono bajeti ipi?

Rafiki yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi sasa kuna kazi nzuri hamtaki kunifanyia pale ya Soko la Kimataifa ambalo ni la kununua nafaka kutoka Mbeya. Ninyi ndugu zangu ambao mahindi yenu hayana soko mlete pale kwangu Njia Panda, yaani Himo ili watu wa Sudani, Kenya, Uganda na Somalia, wafike pale wanunue mahindi yale kwa bei nzuri, yaani bei za Kimataifa ili tuweze kupata soko zuri. Je, fedha za lile soko zipo kwenye hii bajeti ili nikuunge mkono rafiki yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwani mimi sina mgogoro na wewe lakini kama zile fedha hazipo nitakwenda kuwaambia nini watu wa Moshi na Vunjo?

Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, sisi tunapiga kelele hapa siyo kwamba tuna roho mbaya, sisi ni Watanzania na ni Wazalendo lakini tunachoogopa ni kupidisha bajeti ambayo haina uhusiano na maeneo yetu na nchi yetu. Kwa hiyo, ndiyo hilo la kwanza.

La pili, mmezungumzia KILIMO KWANZA, ni jambo zuri sana. Kule Vunjo nina Masista wa *Holy Spirit Sister*, ni wakulima

wazuri sana wa mahindi na ni wafugaji wazuri sana wa ng'ombe wa maziwa na mbuzi. Masista hawa wanasaidia sana masuala ya jamii kwani wamejenga shule ya sekondari nzuri sana, ambayo hata Rais Jakaya Kikwete ilikuwa aje aifungue katika eneo la Siha. Pia wamejenga kituo kizuri sana cha afya na sasa hivi wana makontena wamepata kutoka Marekani wanataka kujenga kituo kikubwa cha kulelea wazee.

Sisi hatuna kituo cha kulelea Wazee Mkoa wa Kilimanjaro na siyo Mkoa wa Kilimanjaro tu ni karibu nchi nzima. Sasa tatizo lilitojiteza ni kwamba, watu wamevamia shamba lile, kwa miaka mingi wale Masista wanahangaika, wanatukanwa, wanakashfiwa na hao watu waliovamia pale (*intruders*), Viongozi walioko ndani ya Serikali wameshindwa kuwasaidia. Wameshindwa kusuluhiha mgogoro ule na wameshindwa kuleta amani, wale Masista wameamua kwenda Mahakama Kuu. Wamehangangaika sana wale akina mama, Mahakama Kuu wamejaribu kuita pande mbili zinazohusika na mgogoro ule imeshindikana. Wale waliovamia wanapewa kichwa kwamba ninyi kaeni hakuna mtu atakayewang'oa hapa. Mahakama Kuu imetoa uamuzi na ninasema kama tutafika mahali hatuheshimu hata amri za Mahakama tena Mahakama Kuu, hii nchi tunaelekea kubaya. Tunakuwa na *double standards*.

Mahakama Kuu ikiamua mambo yake maeneo mengine amri zile zinasimamiwa, lakini nashangaa; naliomba Bunge hill, namwomba Waziri Mkuu na naiomba Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, hawa Masista wa *Holy Spirit Sisters* wa Marangu Moshi walishinda kesi yao Mahakama Kuu tangu mwaka 2008 na hiyo amri ya Mahakama Kuu ninayo hapa, amri ile inawapa haki ya mwanzo kwamba watu wote waliovamia shamba lile tangu mwaka 2004 ambao sasa hivi wanaauza shamba lile la Masista, zaidi ya hapo wanazika hata watu wao kwenye shamba lile, wameamriwa waondoke lakini hawajaondoka mpaka leo. Naomba Serikali mtekeleze.

Katika mazingira haya nitaungaje hoja mkono kama hamjatekeleza hiyo na hamjawaondoa wale wavamizi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrema.

**MHE. SELEMANI SAID JAFO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, binafsi napenda kukushukuru sana. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye mchana huu wa leo nami nimekuwa mionganini mwa washiriki wa kujadili katika hoja hii ya bajeti ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kutoa pole kwa Watanzania wote kutoka ndani ya moyo wangu, kwa sababu Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumechaguliwa kwa ajili ya Watanzania. Najua leo hii tumekuja katika mchakato wa bajeti, lakini bajeti hii ilianza kutengenezwa katika maeneo mbalimbali. Matusi yaliyotokea hapa maana yake ni kwamba, Watendaji wote wa Serikali hawana akili na wapumbavu. Hii ndiyo maana ya matusi yaliyotokea hapa! (*Makof!*)

Ina maana Wizara zote zilizofanya mchakato huu mpaka sisi Wabunge hapa tunakuja kuangalia nini kimefanyika tuweze kuishauri Serikali kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 (2), kazi ya Bunge ni kuismamia na kuishauri Serikali. Lengo tuseme ni upungufu upi upo katika bajeti na yepi yaweze kuongezwa ili iweze kutoka bajeti nzuri kwa ajili ya mustakabali wa Watanzania. Tumefikia hatua mpaka tunamtukana Rais katika Bunge hili; ndugu zangu nasema ni aibu kubwa sana ambayo tumeipata! (*Makof!*)

Rafiki yangu Mheshimiwa Lusinde alitoa *reference* ya Kizaramo ‘*zilongwa mbali zitwendwa mbali*’ kwamba tunayozungumza tofauti na tunayotekeleza tofauti. Mimi naomba kuongea katika lugha nyingine ya Kizaramo inasema: “Shokola”, yaani pori ambalo halijawahi kufanyiwa kazi kabisa.

Nataka nzungumzie suala zima la matumizi mengineyo, tukiachia bajeti ya maendeleo. Bahati mbaya tuna vitabu hivi tumekaa navyo toka katika Kamati, lakini watu hatujasoma. Bahati mbaya Wabunge hawajajua kuna vifungu gani ambavyo mwaka huu ni vipya. Kuna *Vote Namba Nane* ambayo inasema *Constitutional Review*, inabeba karibu shilingi bilioni 39. Hiyo ni sehemu ambayo ina fedha nyingi sana, ingejenga barabara yangu ya Kisarawe hadi Maneromango pale, lakini kwa vile Katiba ni jambo muhimu na kila mtu anapiga kelele kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama kuna kitu kipyga kimekuja lazima matumizi mengineyo yataongezeka katika bajeti ya mwaka huo.

Jamani mnaona hata katika migogoro tunayoingia hapa Tanzania kila mtu anazungumza katika vyombo vyahabari ni kwa ajili ya Katiba tu. Nini maana yake? Maana yake ni kwamba, kumbe Tanzania mwaka huu hata bajeti yetu ingetengwa kwa ajili ya kuangalia Katiba tutaifanyaaje kwa sababu lilikuwa ni jambo muhimu katika hilo. Fedha zake zinaenda katika matumizi ya kawaida, huwezi kuzikuta kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala zima la Sensa. Mwaka huu mnajua tarehe 26 Septemba tunaenda kufanya Sensa ya Taifa. Sensa hii inahitaji fedha ili iweze kufanyika na fedha yake huwezi kuikuta kwenye Miradi ya Maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu; hapa Wabunge tumezungumza kwamba, mielongoni mwa sehemu ambazo Tanzania tunapata hasara ni katika suala zima la Mikataba. Ofisi ya *Attorney General*, mwaka huu imeweka kifungu maalum kwenye suala zima la kusimamia Mikataba, fungu ambalo kipindi cha nyuma halikuwepo. Watu hawajasoma na hawajaona, zote zinakwenda katika matumizi ya kawaida. (*Makofii*)

Kuna matatizo watumishi wote wanalamika kwamba maslahi yao hayazingatiwi, hata Waheshimiwa Wabunge tumelalamika humu ndani, imeundwa Bodi Maalum ya kushughulikia jinsi gani haki ya kila mfanyakazi itapatikana mwaka huu kwa kuunda Bodi Maalum. Bodi ile iiliyoundwa maana yake inaingiza tena bajeti ya matumizi ya kawaida, lakini watu hatujasoma tunalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna Kitengo kinaitwa *Financial Intelligent Unit*, kwa mara ya kwanza kimeanzishwa kwa ajili ya kuangalia hizi fedha chafu. Tumesema miongoni mwa jambo kubwa lenye athari Tanzania ni Kitengo hicho na Serikali imeleta kifungu hicho ni kipyta, someni vitabu mtakiona.

Kuna Kitengo kipyta kinaitwa *Public Private Partnership* katika Idara ya Fedha kwa ajili ya *PPP* ilimradi hata fedha ndogo ziende Wizara ya Kilimo, waje wawekezaji wengine kuhakikisha kwamba wanatumia miundombinu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Kilimo kinaenda mbele. Watu hatujasoma, hayo ni maeneo mapya. (*Makofii*)

Kuna fedha za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ambazo mwaka huu nazo zimeingizwa katika matumizi mengineyo. Naomba niwaambie ndugu zangu, katika *Subvote* ya *Crop Development Bank* katika Wizara ya Kilimo kuna suala zima la ununuaji wa pembejeo, ambalo lina karibu shillingi billioni 75. Kununua dawa na pembejeo, zote zipo katika matumizi ya kawaida. Hizi zote ukiziangatia lazima zinaleta uzito katika matumizi ya kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema Mheshimiwa Lusinde ali-quote reference ya Kizaramo "zilongwa mbali zitwendwa mbali", naomba Wabunge tusionekane ni wanafiki kwa Wafanyakazi wa Serikali. Tumesema Wafanyakazi wa Serikali hawalipwi posho mpaka Madaktari waliandamana hapa na watu tulishabikia kwelikweli. Utakapomwongezea Daktari posho, utakaposema

posho kwa ajili ya wafanyakazi walioko katika mazingira magumu, lazima itaongeza uzito katika matumizi ya kawaida. Ndugu zangu tusiseme, lazima tuwajali na hawa watu ambao wanaenda kuifanyia kazi Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Jambo kubwa la kutakafari kwa kina hapa ni njia za kufanya kukabiliana na matatizo yanayotukabili. Kwa hiyo, ina maana ukija kuangalia uzito wake kuna fedha nyingi nyingine zinaenda katika *investment*.

Mheshimiwa Mwigulu, jana alisema kwamba, hata hili suala zima la kuendeleza elimu lote linaingia huko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nimesema kazi ya Wabunge sisi ni kuishauri Serikali wapi kuna upungufu tuweze kujazia ili bajeti iweze kwenda vizuri. Kwa hiyo, yale matusi ndugu zangu nilinyong'onyea sana kwamba siyo vizuri mpaka kumdhilisha Rais katika Bunge hili huku Watanzania wote wanaona. Kwangu mimi kijana ni kitu ambacho naona kwamba siyo kizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya watu hawa, ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu wamepewa fursa kubwa sana. Wenzetu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuna bomba kubwa kutoka Ruvu Chini linalotengenezwa. Sisi Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, tulikwenda kukukagua kule, hilvi sasa watu wapo kazini wanafanya kazi na bajeti hii inaonesha kuna kitu gani kinafanyika lakini watu hawazungumzi! Tuzungumze mazuri yaliyopo na yepi tuweze kuongeza kujaza nyama. Haiwezekani kila kitu unakashifu mpaka unawatukana watu wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Ndugu zangu sisi tumeumia sana na hii inaonekana kwamba tuna watu wengine humu ndani hawako makini. Mimi nimelisema hili kwa uchungu kwa sababu kumbe tuna watu wengine umakini umepungua na umakini ukipungua maana yake ni kwamba, kazi yako ni kuwajaza watu hasira wakukubali ilimradi kwa vile umewajaza hasira tu siyo kwamba una hoja kweli kwa ajili ya kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali katika maeneo yafuatayo:-

La kwanza, vijana wetu wa bodaboda. Naomba kodi zote za bodaboda zifutwe, mtu akinunua pikipiki yake ana licence yake anaweza kufanya kazi kwa sababu ni sehemu kubwa ya ajira kwa vijana wetu. Mimi nina vijana wangu pale Kisarawe sasa hivi wanantazama wanaomba niwaombee hili na ninaomba nililetie. Serikali ninaomba siku ya kuhitimisha hapa mseme bodaboda wote kodi zote zimefutwa, mtu akiwa na leseni yake aingie kwenye biashara. (*Makofi*)

La pili, naomba tufute kodi katika viwanda vya ndani hasa vya korosho, pamba na viwanda vya kutengeneza mafuta ya kura. Tukifanya hivi maana yake tutakuwa tumekuza uchumi wa nchi yetu na tutakuwa tumekuza ajira ya wananchi wetu wa Tanzania. Hili sitakubali mpaka nimsikie Waziri hapa anatamka ni nini kinafanyika katika eneo hilo. (*Makofi*)

Sehemu ya tatu ambayo sijaridhika nayo na ninaomba Wabunge wenzangu msiridhike ni kupandisha gharama za simu kama ilivyopendekezwa. Tupeleke gharama hizi kwa makampuni ya simu. Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha, naomba utueleze kwamba, gharama za simu zimebaki palepale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa kufanyiwa marekebisho hayo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Jafo. Nawaomba na Waheshimiwa wanaofuata, tujitahidi kuangalia lugha zetu.

Mheshimiwa Chiku Abwao, atafuatiwa na Mheshimiwa Kange Lugola.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Bajeti. Kwanza, naomba nimpongeze kaka yangu Mheshimiwa Mgimwa, kwa kuchaguliwa na Mheshimiwa Rais, kushika wadhifa huu kwa kuwa Waziri wetu wa Fedha. (*Makof*)

Pia nampongeza kwa mwanzo mzuri alioanza nao, maana pamoja na upungufu uliopo katika Bajeti ye ye ameonesha ubunifu wa kuweza kuangalia kodi mpya ambayo itagusa matajiri ambao wana hiari kutumia fedha zao kama watasajili magari yao kwa majina, kwa fahari zao wanaweza wakafanya hivyo, wakati huo huo Taifa litakuwa limeongeza kipato. Nakupongeza sana Mheshimiwa Mgimwa kwa hilo; ni matumaini yangu kwa ubunifu huu umeanza vizuri, utaendelea kubuni kodi nyingi. (*Makof*)

Kwa dhana ya Watanzania, mpaka sasa watu maskini wamekuwa wakitozwa kodi sana lakini tunashindwa kutumia fursa ya matajiri ambao wana fedha nyingi za kumwaga ambao wakiwekewa mambo mengi ya ufahari ili kuonesha fahari zao, umaarufu na uwezo wao kiuchumi, wangeweza kulipa kodi hii kwa mapenzi na furaha kiasi kwamba tungeweza kujikwamua katika umaskini unaotukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, naomba nami pia nitoe mchango wangu, lakini pia nina maskitiko kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge katika Bunge hili la Jamhuri wote tuna haki sawa na hakika kwa yale maovu ambayo hayatakiwi kufanyika ndani ya Bunge hili yanatakiwa yatuguse pande zote mbili. Inapofikia suala la kukataa lugha chafu, lugha ya maudhi, iangaliwe kwa Wabunge wote na wote watendewe haki sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika, jana hapa Wapinzani walitukanwa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chiku, samahani, naomba ukae kidogo. Meza ikishatoa uamuzi siyo ruhusa kujadili uamuzi ule. Endapo unaenda huko ni nia yangu tu kukutahadharisha usije ukatumbukia tena kwenye tatizo ambalo hatulihitaji. Endelea kuchangia bajeti.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ungenisubiri tu sina maana ya kujadili uamuzi uliotoka sasa hivi, ndiyo maana nimeanza kwa kusema jana. Nimenukuu jana kuonesha mfano; juu ya suala la leo mimi sitaliingilia wala kulizungumzia, isipokuwa nasema jana.

Jana kuna Waheshimiwa Wabunge hapa wametoa lugha za kuudhi, wametukana Wapinzani, wameaita vichaa, wameambiwa wakapimwe akili ni wanazi.

Haya mengine ya leo yamekuwa ni nyongeza na pengine yametokana na hasira za kuona kwa nini sisi tunyanyasike namna hii wakati wenzetu hata wakitumia lugha mbaya ambazo hazipendezi hawachukuliwi hatua yoyote; ndiyo maana nimeona nizungumze hili! (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana hukuhusika wewe, hukuwa kwenye Meza, lakini ni Bunge hili. Tukitendewa haki, Bunge litakuwa na heshima. Lugha chafu kutumika kwa Mbunge haipendezi na mimi pia sitaki kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, acha nirudi kwenye mchango, maana dakika kumi ni chache. Mimi naomba nichangie kuhusu Deni la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa linazidi kutisha. Mwaka jana lilikuwa asilimia 10.9, lakini mpaka hivi sasa limefikia asilimia 19. Deni linazidi kukua, maisha ya Watanzania

yanazidi kuwa ya dhiki. Mfumko wa bei unazidi kupindukia. Tunajiuliza hili Deni la Taifa linakua kwa kiasi hiki; fedha hizi zinatumika kwa kazi gani? Maana ingekuwa ni faraja sana kama Deni hili la Taifa linakua lakini kunakua na unafuu upande mwingine kwamba, Watanzania wananaufaika zaidi, maisha angalau yanakuwa na hali ya kuridhisha, matatizo yanapungua, lakini nchi hii matatizo kila kona.

Madaktari wako mbioni kugoma tena, Walimu mishahara haitoshi wanalia, Watumishi wote kwa ujumla, maisha yamekuwa ni magumu kwa kila sekta, lakini Deni hili la Taifa linakua. Hii hali ni ya kutisha sana, inaonesha Serikali iliyopo madarakani inaangalia wakati tulionao tu, haiangalii baada ya wao kuondoka tutaiendesha vipi nchi hii. (*Makofii*)

Ninaposema kuondoka siyo kwa maana tu ya kuondoka madarakani, maana tatizo la Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, ukigusa suala la utawala, hata yale mambo mazuri ambayo wangeweza kuyapokea hawayapi nafasi kabisa. Tukizungumza kuondoka, kuna kuondoka kwa kuzeeka, kung'atuka Serikalini na kuna kuondoka kwa kila aina, ambapo kwa ujumla wake bado athari inabaki kwa Watanzania walio wengi.

Ndipo hapo sisi tunajiuliza hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina mtazamo gani?

Unapotaka kuchambua mtazamo ndiyo utakuta ile ile lugha ya kuudhi, lakini siyo lengo letu Wapinzani kukaa kila siku kuwatolea maneno mabaya.

Tunasikitishwa na mwenendo wa Serikali, pale ambapo unakuta matarajio ya Watanzania kuja kuishi maisha yenye neema yanapotea kabisa. Tuna hali ngumu sana sasa hivi Tanzania, lakini ukiangalia hata mtazamo wa bajeti unavyokwenda, hata kwa suala hilo la Kilimo ambalo tunasema labda kwa Mpango wa Kilimo Kwanza labda

tungeweza kujikwamua katika uchumi wetu, lakini bajeti kiasi gani inapangwa katika kuhakikisha kwamba, Kilimo kinakuwa na tija.

Afadhalii tungekubaliana hata na uamuzi wa nchi za SADC kwamba, angalau asilimia kumi iwe inatengwa kwenye Kilimo ili tuangalie kuanzia hapo kuboresha kilimo chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ina mkakati gani wa kuboresha soko la ndani? Sasa hivi Tanzania kila kitu tunategemea nje tu. Tunazibeba Sera ambazo zinazidi kutuangusha. Hivi tukijiuliza hasa *logic* ya ubinafsishaji ni nini? Hivi unategemea nini; kila kitu utegemee kufanyiwa na watu wengine upate faida? Tunategemea hivyo kweli? Tunabinafsisha madini yetu tunachukua asilimia ndogo sana tunategemea eti tutafanyiwa kazi na wenzetu watutajirishe; inawezekana hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ufile wakati hata hizo Sera kama mlizipanga, kila kitu huwa kinakuwa na upungufu wake. Upungufu wa Sera ya Ubinafsishaji umeshaonekana waziwazi, ni mahali ambapo tulikosea, tukubali makosa ambayo tuliyaufanya pengine kwa matarajio makubwa. Inawezekana kabisa Viongozi wetu wakati huo walikuwa na mawazo mazuri kabisa, wakafikiri kwamba ingetusaidia, lakini imefika mahali sasa tumeona wazi kuwa haitusaidii.

Kwa nini tuendelee kung'ang'ania tu kitu ambacho kinazidi kutuletea umaskini katika Taifa letu eti kwa sababu tu Viongozi waliotangulia waliona hiyo Sera ni nzuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona hatutendi haki. Ufile wakati wa kuziangalia upya sera zetu, zile ambazo zimetuletea tija ziendelee, ambazo zinatuletea umaskini tuziache. Tuzuie sasa hivi ubinafsishaji mpya ambao bado hatujaufanya. Kwa mfano, hivi sasa tumeshagundua gesi nyiningine.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile dakika zangu naomba uzikumbuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumegundua tena gesi, lakini mpaka leo hii ninavyoongea, sijui kama kuna sera ya gesi. Naomba Serikali ituambie: Je, kuna sera ya gesi? Sera ya gesi ipo? Kwa hiyo, tutaendelea kubinafsisha kuweka wawekezaji wengine katika kitu ambacho hatujakiwekea utaratibu mzuri, hatuna sera ya kuendesha biashara ya gesi, matokeo yake tunazidi kuwanufaisha wageni tunaowabinafsishia kazi hiyo, tunabaki sisi kuwa maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufile wakati wa kufuta itikadi ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano. Tunapojadili mambo ya msingi, tuachane na mambo ya vyama, tuangalie maslahi ya Watanzania. Nchi yetu inakwenda vibaya! Umaskini unaokuja sasa hivi, amani haitakuwepo. Amani itavurugika. Amani haipo mahali penye shida! Amani inakuwepo mahali watu akili zao zimetulia, wana uhakika kesho wataishi vipi. Watanzania wa sasa hawajui kesho wataisha vipi, tunang'ang'ana tu mambo ya itikadi. Bunge linageuzwa kama ukumbi wa wasanii, kila mtu anaonyesha umahiri wa kutoa lugha za maudhi. Haipendezi!

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tukuballane wote tuwe kitu kimoja, tushikamane kwa mambo ya msingi ya kulinusuru Taifa letu ili vizazi vyetu vije kupata manufaa katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo ambacho kinafanyika sasa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, kuweka ushabiki wa Vyama vya Siasa na kutupa mbali hoja za msingi ambazo ndizo zilizotuleta ndani ya Bunge hili hatuwatendei haki Watanzania. Mimi siko tayari kushabikia ushabiki wa kiitikadi wakati Taifa hili linakwenda vibaya. Umetoa onyo, wakati nikianza kusimama ulifikiri nitatoa maneno ya maudhi. Mimi

sitaki maneno ya maudhi, nataka tulijenge Taifa hili kwa maslahi ya nchi yetu na vizazi vyetu vije vitutaje kwamba walikuwepo Wabunge fulani walijenga hiki na hiki na ndiyo maana leo tumefika hapa. Mambo yote mazuri yanapotea katika Taifa hili, tunashikilia ushabiki. Mtu anasimama hapa kama yuko kwenye jukwaa la usanii wakati anaimba nyimbo huko! Haifai! Tunatakiwa sasa watu tuangalie maslahi ya nchi yetu tunapokuwa, hasa katika suala kubwa hili la bajeti, itikadi tuachane nazo wote bila kujali vyama vyetu, tuangalie tunafanya nini kuwasaidia Watanzania ambao sasa hivi wana hali ngumu sana kiuchumi, hawajui kesho wataishi vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii itapita, lakini ukweli ni kwamba inapita kwa sababu ya uwingi tu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Lakini kama ingekuwa Wabunge wa Upinzani ni wengi, bajeti hii isingepita. Lakini Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanasmama wanaunga mkono mia kwa mia wakati huo huo wanachambua kila...

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Abwao namwona Mheshimiwa Nkumba amesimama ameomba mwongozo.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 64 kifungu cha (g). "Mheshimiwa Mbunge anapochangia amekuwa akitoa mfano..."

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukisome.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Kinasomeka kwamba: "Bila ya kuathiri masharti ya ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge yeoyote hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine."

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anapochangia hapa ametoa lugha ya kuwadhalilisha na kuwaudhi wasanii wa Tanzania ambao kwa kweli tunawaheshimu sana nchini hapa. (*Makof*)

Maelezo anayoyatoa Mheshimiwa Mbunge kwamba Bunge hili haliwezi likageuka kuwa kama eneo la wasanii wanaotoa maneno yasiyofaa, ni maelezo yanayowaudhi, ya kuwadhalilisha na kuwakejeli wasanii wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mheshimiwa Mbunge atoe maelezo ambayo yanaweza yakarudisha heshima ya wasanii walioko nchini. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge *ruling* yangu katika mwongozo huu nina- refer kwenye Bunge la Tisa, alipokuwa Mheshimiwa Mzee Samuel Sitta ni Spika hapa, aliwaomba Waheshimiwa Wabunge kuwa na ngozi ngumu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane, tustahimiliane, lakini ambacho nakichunga zaidi hapa, tusiende kwenye kutukanana na kuvunjiana heshima. Lakini haya makombora madogo madogo tuvumiliane. Mheshimiwa Chiku Abwao malizia. (*Makof*)

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nina hakika mimi nafahamu Kiswahili, nimezaliwa mjini, lakini mwenzangu sijui amezaliwa wapi, lakini ukweli ni kwamba nilikuwa nina maana ya kwamba tusigeuze hili Bunge sehemu ya usanii. Kwa sababu najua usanii ni muhimu sana katika Taifa letu, lakini una maeneo yake. Hata hao wasanii wanategemea tuwafanyie kazi nzuri ndani ya Bunge humu ili na wao pia waanze kunufaika. Hiyo ndiyo ilikuwa maana yangu. Sio maana ya kudharau sekta ya usanii. Nawaheshimu sana wasanii na wana mchango mkubwa sana katika Taifa letu na nawaombea waendelee kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, hoja zangu za msingi ziliikuwa ni hizo, kuhakikisha kwamba tunataka deni hili la Taifa lisizidi kukua kupita kiasi. Kwa kumalizia, kuhusu deni hili la Taifa, ni vizuri ikaundwa Tume ili tuweze kuchunguza na kujua fedha zinatumika vipi, hizi zinazokopwa kila siku, wakati maisha ya Watanzania yanazidi kuwa duni. Zinanufaisha sekta gani? Maana hazionekani! Tunapewa madeni makubwa, lakini hatuelewi yanafanya nini na kikubwa zaidi pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Ohoo!!!!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chiku Abwao. Sasa mchangiaji wangu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola wa asubuhi ya leo.

Utaratibu itakuwa mwisho.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Naomba nianze na kitu kilicholetwa humu ndani kinaitwa Bajeti Kivuli, Bajeti Mbadala. Mwanzoni nilidhani kweli kuna kitu kinaitwa Bajeti Kivuli kimeletwa humu ndani, lakini baada ya kusoma nikagundua si kivuli tena ila ni giza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wabunge wenzangu mnielewe na ninaomba rafiki zangu Wapinzani mnielewe na kila mmoja achukue kitabu chake cha hotuba ya Mheshimiwa Zitto Kabwe afunue ukurasa wa 34 na 35. Hatuwezi kukubali kuwadanganya Watanzania, kwamba sisi tunaweza kunusuru maisha yao wakati hatuna uwezo wa kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma mapato ya ndani kwenye bajeti, giza; mapato ya ndani *TRA* ni sifuri, mapato ya

sio ya kodi ni sifuri na mapato ya Halmashauri ni sifuri. Hii bajeti ya namna hii ambayo bajeti ya ndani ni sifuri, anapohubiri kutenga asilimia 35 mapato ya ndani atayatenga kutoka fedha gani? Anaposema ataongeza mishahara ya wafanyakazi, ataongeza mishahara kutoka kwenye fedha gani wakati mapato ya ndani ni sifuri kwa mujibu wa hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunawadanganya Watanzania kiasi hiki? Namshukuru Mheshimiwa Nchemba Madelu aliita *rubbish* na akaitupa. Ila nilimshangaa kwa nini hakuisigina.

**NAIBU SPIKA:** Nitakupa nafasi Mheshimiwa. Mheshimiwa Kangi Lugola, malizia.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ambaye anasema uongo na hasa uongo mkubwa wa kudanganya watu zaidi ya milioni 45, sisi waumini wa dini huwa tunamfanyia huduma, ili akiokoka aweze kusema ukweli kwa ajili ya kuokoa Taifa, na hatuna lugha nyingine Kikanisa, huwa ni kumkemea na kusema kwa Jina la Yesu ashindwa na alegee. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuisome vizuri bajeti ya Serikali. Bajeti ya Serikali imeainisha maeneo yote ambayo Watanzania wa leo wangependa yafanyiwe kazi kwa ajili ya maisha yao. Maeneo gani ni maeneo ya kupambana na umaskini, maeneo ya kupambana na mfumuko wa bei, maeneo ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na kilimo, afya, uvuvi, mifugo na ufugaji. Lakini naomba niishauri Serikali, tuweke vyama vyetu pemberi tuongozwe na uzalendo. Katika mazingira ambayo tuna nia njema ya kuhakikisha kwamba tuatekeleza yale ambayo tumekubaliana kwenye bajeti hii bajeti ya Serikali katika hotuba yake ukurasa wa 35, wanasema, kuna changamoto na vikwazo vinavyosababisha

bajeti hata wakati mwingine ikiwa nzuri kiasi gani, inakuwa na matatizo katika utekelezaji. Naomba nishauri katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wamezungumzia kuhusu misaada na mikopo kwamba imekuwa haipatikani kwa wakati kutokana na urasimu na masharti magumu. Hivi Serikali yetu mnayo dawa ya masharti magumu? Mnayo dawa ya urasimu juu ya jambo hili? Eneo hilo tulitazame vizuri. Tutafute namna ambavyo tutapata fedha ili tuondokane na utegemezi huu ambao tumeshaona kuna kikwazo ambacho ni sugu, ambacho kina tatiza nchi nyingi za Kiafrika. Kuna kikwazo kingine sugu mmekionyesha kwamba kumekuwa na ongezeko la malimbikizo ya deni la ndani kwa maana ya wakandarasi, wazabuni pamoja na watumishi na hasa walimu, wanadai zaidi ya Shilingi bilioni 14. Hiki nacho ni kikwazo ambacho kama tutaendelea na mtindo huu, badala ya kutafuta maeneo yenye fedha, vikwazo hivi ambavyo ni sugu, kwa kweli mipango yetu mizuri, mipango yenye nia njema kwa Watanzania itakuwa ni vigumu sana kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mwibara wananchi wangependa badala ya kuendelea kuagiza chakula kutoka Rukwa Sumbawanga tutumie maji ya Ziwa Victoria kulima maeneo ya Karukekele, Kabainja, Muranda, Nansio na maeneo mengine. Lazima tupanue wigo kwenye kilimo, lazima tuhakikishe kwamba fedha za kutosha zinakwenda kwenye kilimo, vinginevyo tutatwanga maji kwenye kinu. Fedha zitatoka wapi, naomba sasa Wabunge mnielewe na naomba Watanzania mnisikilize. Kodi ya mapato kwenye upande wa madini nchi hii inaibiwa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge nchi hii inafilisiwa. Ninasikitika Bunge lilitotunga sheria hii, hawakuona maeneo hayo vizuri. Inawezekanaje tunatunga sheria ya kulinda Kampuni za ndani zitakazotoa *technical services* ndani ya migodi, tunazilinda kwa kodi ya zuio ya asilimia tano kwa maana ni wakazi na Makampuni ya nje yametungiwa Sheria ya Kodi ya zuio asilimia 15. Lakini makampuni haya ambayo ni ya kigeni yamefurika ndani ya

migodi kwa ajili ya kutoa *technical services* yamekuwa yakikwepa kulipa asilimia 15 na yenyewe yanalipa asilimia tano, huu ni wizi mkubwa katika nchi hii.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono turekebishe sheria hii. Wamekuwa wakija, wakashaka wanapata ile *Permanent Establishment* wanaonekana na wao ni Makampuni ya ndani, wanakwepa sasa kulipa 15%, wanlipa asilimia 5% kama Makampuni ya Watanzania. Huu ni wizi mkubwa ndani ya mgodi. Nawaambia Watanzania, kwa vile wanakwepa, 10% ni nyingi sana, tuwabane kwamba wao wataendelea kuwa ni *non resident* ili waweze kulipa 15%. Nawaambieni bajeti hii itatekelezeka kwa fedha hizo, na hakuna Mtanzania atakayelalamika tena katika nchi hii. Nchi hii ni ya asali kwenye madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuliwatungia sheria ya kuwatetea, wao ndio waweze kutoa huduma ndani ya migodi, asilimia zaidi ya 70 ya matumizi ndani ya migodi hapa Tanzania, ni manunuzi. Lakini manunuzi ndugu zangu ndani ya migodi hata kupeleka kuku ni *South Africa*, hata kupeleka mchicha ni *South Africa*, wazawa wa Tanzania wanashindwa kufanya manunuzi ndani ya migodi. Nchi hii tunaipeleka wapi? Wakati umefika sasa Waheshimiwa Wabunge badala ya kuilaumu Serikali, wakati sisi ndio tunaotunga sheria mbaya, na ndiyo inatuibia rasilimali za madini, turudi ndani Waheshimiwa Wabunge na mniunge mkono. Nami nawaambieni Waheshimiwa Wabunge, kama hamtaniunga mkono kurekebisha sheria hii inayotuobia, na Serikali msiponiunga mkono kwa kusimama juu ya hoja yangu, sitakubali kuitisha bajeti yenu kwa sababu ni wizi mtupu ndani ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie viwanda vya kuchambua Pamba. Kama hatutafuta kodi za *VAT*, wakulima wa Pamba wataendelea kutafunwa na mchwa anayeitwa Soko la Dunia. Lazima turudi, Watanzania tujenge *capacity* ya viwanda hivi, watengeneze mnyororo wa thamani kwa maana

ya kuongeza ajira, viwanda vya nguo ndugu zangu ndiyo mwajiri mkubwa katika nchi hii, wanaajiri zaidi ya watumishi 30,000 na hili nalo msipofuta kodi hizi hakutaeleweka hapa ndani. Hatuwezi kukubali mnasamehe Makampuni ya nje, inapokuja kwenye Makampuni ya ndani ya wazawa, mnakataa kufuta kodi hizi ambazo zinatu haribia hayo mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wapinzani hawa ni wenzetu, nami nawashauri jambo moja muhimu sana mchana wa leo. Serikali ya CCM imewajengea majengo haya, leo mnazunguka kwenye viyoyozi; Serikali ya CCM imewajengea barabara mnazopita na mashangingi yenu barabarani; na Serikali ya CCM inawapa mishahara kutokana na kodi inazokusanya kwa Watanzania. Naomba tuheshimiane, tusitukanane, tuhakikishe tunaboresha bajeti ya Serikali kwa kuitafutia fedha. Hapo ndipo tutakapoheshimiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kangi Lugola, nakushukuru sana.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Kuna Waheshimiwa wawili walismama. Tuanze pale nyuma.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 kuhusu utaratibu, na naomba utaratibu kuhusiana na Kanuni ya 73(2).

**NAIBU SPIKA:** Subiri kidogo. Kanuni ya 68 inayohusu utaratibu, halafu umekwenda Kanuni ya 73(2), naomba uisome.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** "Endapo Mbunge au Waziri atatumia maneno au lugha isiyotakiwa Bungeni, yaani lugha

ya matusi, usafihii, uchokozi au lugha ya maudhi na atatakiwa na Spika ajirekebishe kwa kufuta maneno au lugha hiyo, akakataa kufanya hivyo, Spika anaweza kumwamuru Mbunge huyo atoke mara moja nje ya Ukumbi wa Bunge na abaki huko nje kwa muda wote uliosalia wa kikao cha siku hiyo."

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kanuni hii inasema kwamba mtu anapotolewa nje na *Sergeant At Arms* anatolewa nje ya Ukumbi wa Bunge, sio nje ya viwanja vya Bunge.

Sasa mwaka jana alipotolewa Mheshimiwa Msigwa, Tundu Lissu na Lema ukawapa *Sergeant At Arms* kuwapeleka mpaka nje.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje naomba ukae chini kwanza. Ninachokiona, unachofanya ni kujadili maamuzi yangu, kitu ambacho unazidi kuzivunja Kanuni.

Kwa Kanuni hizi, kwanza nitoe tangazo moja, Mheshimiwa Sara Msafiri ni Katibu wa Wabunge wa Morogoro, anawaomba Wabunge wa Morogoro mtakapotoka hapa mkutane ukumbi wa Msekwa.

Kwa mujibu wa kanuni hizi tunapokutoa nje ya ukumbi, maana yake ni nje ya ukumbi wowote katika kumbi zillizoko hapa. Ninapofafanua mnapaswa kunisikiliza vizuri. Siwezi kukutoa hapa halafu ukaenda kwenye kikao cha Sara Msafiri cha Ukumbi wa Msekwa ukasema ultolewa katika Ukumbi. Huo ndiyo ufanuzi. Ukitolewa nje ya Ukumbi wa Bunge maana yake huwezi kushiriki shughuli za ndani ya ukumbi na wala shughuli za Kamati za Bunge popote katika eneo la Bunge kwa siku hiyo mpaka kesho yake.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijaridhika na jibu unalonipa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wenje kaa chini.

Mheshimiwa Silinde kama huna lolote, muda wangu umekwisha.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, *this is quite unfair.*

## TAARIFA

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninatoa taarifa, Kanuni ya 68 (8). Wakati mzungumzaji wa mwisho anazungumza, kuna mambo mawili alizungumza ambayo alijaribu kuyagusia katika Hotuba ya Kambi ya Upinzani.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 68 (8), inasema nini?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Inasema: "Vilevile Mbunge yejote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na ruhusa ya Spika itatolewa...", na kuendelea. Uliniambia nisubiri, na sasa umenipatia nafasi. Ni kwamba mzungumzaji wa mwisho alijaribu kuzungumzia hotuba ya Kambi na alitaja ukurasa wa 34 na akaainisha kwamba hakuna mapato. Lakini katika hotuba hiyo, ukurasa wa 34 imeonyesha kwamba mapato ya ndani ni Shillingi trilloni 11.889. Kwa hiyo, Watanzanla wajue ipo hiyo ndani. Kwa hiyo hilo anaweza akalifanya kwa wakati wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, tunataka tuweke sawa kwamba mishahara tunayolipwa, hatulipwi na CCM, tunalipwa kwa kodi za wananchi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Niliwaona Waheshimiwa Wabunge wawili wengine kwa haraka. Mheshimiwa Mbatia halafu Mheshimiwa Sendeka atakuwa wa mwisho.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuhusu mwongozo wako, Kanuni ya 68(7).

**NAIBU SPIKA:** Naomba uisome.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 inasema, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema maneno kuhusu utaratibu ambapo Mbunge yejote ambaye wakati huo atakuwa anasema atanyamaza na kukaa chini na Spika atamtaka Mbunge aliyedai utaratibu ataje Kanuni au sehemu ya Kanuni iliyokiukwa. Sasa kifungu cha saba kuhusu Mwongozo wa Spika, inasema: Kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatorewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiti chako kimetoa maelekezo kuhusu namna ya kuvumiliana na namna bora ya kutumia muda wa Bunge kwa ajili ya maslahi ya walioleta ndani ya ukumbi huu au kwa maslahi ya walipa kodi wa Tanzania. Sasa imekuwa ikijirudiarudia, na msemaji wa mwisho amediriki kusema kwamba tunalipwa mishahara au posho hapa kwa kodi ambazo ni za Chama cha Mapinduzi. *Democratic Principle* inasema: "No... (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, samahi na nafikiri Mheshimiwa Silinde ameliweka vizuri. Sidhani kama kuna haja tena ya kuendelea na mjadala wa jambo hilo kwa maana hiyo. Naheshimu sana ulichokizungumza na nakubaliana na wewe. Nafikiri limekaa vizuri.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa ajili ya taarifa ili kuwafanya wenzetu warejee kwamba kulikuwa na Mheshimiwa Mbunge amejaribu kupotosha hoja ya Mheshimiwa Kangi Lugola pale alipotoa mfano wa hotuba ya Kambi ya Upinzani ukurasa wa 34

kwamba (a) mkiangalia kuna trillioni 11.889, lakini mapato ya kodi ya *TRA* ni zero, kuhusu mapato yasiyo ya kodi ni zero. (*Kicheko/Mayowe*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wazima hawapigi yowe, watu wazima wanajenga hoja. (*Kicheko/Mayowe*)

**NAIBU SPIKA:** *Order please.* Naomba asikilizwe.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa natoa taarifa kwamba kitabu cha Mheshimiwa Zitto Kabwe ni hiki hapa. Katika sehemu ya mapato ya kodi ya *TRA* ni sifuri, sehemu ya mapato yasiyo ya kodi ni sifuri, lakini sifuri zote mbili ukizijumlisha unapata trillioni 11.889. Mahesabu haya ya Zitto Kabwe hayapo. Huwezi kujumlisha sifuri na sifuri ukapata Shilingi trillioni 11.889.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Siyo hivyo tu, angetakiwa arejee ukurasa wa 85 wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mgimwa ambayo imebainishwa pale kwamba mapato ya kodi ni Shilingi trillioni nane na mapato yasiyo ya kodi ni Shilingi bilioni 644. Lakini ukizijumlisha ndiyo unapata Shilingi trillioni nane, pale juu ya mapato ya ndani. Kwa maana hiyo, ni vizuri wakaangalia kurasa zote mbili na ukiziangalia utaacha kuwadanganya Watanzania, na la mwisho kauli ya Spika ndiyo ya mwisho na Waheshimiwa Wabunge wajifunze. Unapotoa *ruling* kama mtu ana haja ya kupinga, aende kwenye kanuni inayoruhusu kuandika barua kwa Spika badala ya kuendelea kusimama wakati umetoa *ruling* yako. Ni hilo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimewaahidi kwamba nitampa nafasi ya Mheshimiwa Lukuvi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Naomba mkae Waheshimiwa Wabunge wote wenye taarifa. Mheshimiwa Lukuvi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kutumia kifungu hiki cha 68 ambacho wengi tunakitumia na hasa nilipomsikia dada yangu Mbunge mwenzangu wa Iringa. Nataka kurudia maneno yake kwamba hapa ndani ni Bunge na lazima tutekeleze majukumu ya wananchi kwa mujibu wa matakwa na uungwana na Kanuni zinazotawala Bunge. Sasa kwa faida ya Watanzania, nataka niwaambie, maana naona maelekezo mnayaelekeza kwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu wa Mabunge, kuna utaratibu wa kujichunga wenyewe. Sasa msimlaumu Spika kwamba jana kuna mtu alitukana halafu hakuchukuliwa hatua. Ndiyo maana tumeweka viti hivi vya mbele, kuna watu wa kuchunga nidhamu. Sasa inapofikia unamwona mtu wa *front bench* ambaye ndiye mtu wa kuchunga nidhamu ndiye anayetoa matusi, ndiyo tatizo linalotupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hutrajii Waziri Mkuu hapa asimame atoe matusi, vinginevyo hakuna sababu ya utamaduni wa Mabunge kukaa na uongozi. Tuna *caucus*, viongozi tusiwe watu wa mbele kuongoza mashambulizi ya matusi. Haiwezekani! Kwa hiyo, naomba kila kambi na kila kundi lihakikishe uongozi uliowekwa kihalali kupitia vyama. Haiwezekani Katibu wa Wabunge wa *Caucus* ndio akaongoza matusi! Haiwezekani *Chief Whip* akawa ndiye anaongoza matusi, haiwezekani Waziri Mkuu akawa anaongoza matusi au Kiongozi wa Upinzani akawa ndiye anaongoza matusi. Vinginevyo utamaduni wa Mabunge wa dunia hii tunauvuruga. (*Makof!*)

Nilikuwa natetea kiti kwamba utaratibu wa Mabunge sisi wenyewe tujichunge. Kama kuna upande fulani, wengine waliopewa dhamana hiyo ya kusahihisha wasimame. Mis-assume kwamba kila jambo Spika atakuwa analiona. Sisi tulipewa dhamana hiyo, tushirikiane kwa pamoja kuwahakikishia kila Wabunge katika Kambi yao, wanaendesha Bunge kwa mujibu wa utamaduni na ustaarabu wa kibunge.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge. Nawaona wote na mko wengi. Mkitazama saa yetu, mtaona kabisa kwamba haituruhusu kabisa kuendelea hata kwa sekunde moja. Nimalizie *session* hii ya mchana kwa kuwataja watakaoanza kuchangia leo jioni. Atakayeanza kuchangia leo jioni atakuwa Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Waheshimiwa wengine walioomba waendelee kuijandaa.

Katika kumalizia, naomba nisitize tena, *Chief Whip* kwa upande wa chama tawala, Mheshimiwa Lukuvi kwamba walioko mbele pande zote mbili tunasaidiana na mimi katika kuendesha kikao hiki.

Kwa hiyo, tusaidiane, tushikiane, mtaona mambo yanakwenda vizuri. Katika kumalizia, najua Mheshimiwa Mbunge ukisimama unaweza ukawa una jazba fulani, lakini jitahidi kutofautisha hotuba za kwenye majukwa tunapokuwa kule nje na hapa ndani. Kwa sababu kwenye majukwaa kule, hakuna kanuni tulizanazo hapa. Hapa tuna kanuni, lazima tuzifuate. Kwa hiyo, tukiheshimu kanuni na tukichunga kanuni, zetu hatutaishia mahali pa matatizo kama haya ambayo yanajaribu kuendelea kutokea.

Mwisho, kanuni ile ya 64, na nafanya hivyo kwa kuwakumbusha Waheshimiwa hasa wale ambao hawapendi kuvikumbuka vitabu hivi vya Kanuni.

Kanuni ya 64 (e) na (f) inasema: "Mbunge ye yote hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge, (yaani haikubaliki hata ninyi kushambuliana Mbunge kwa Mbunge. Mbunge kuwaita wenzake machizi, haikubaliki hapa). Hairuhusiwi kumsema Jaji katika lugha inayokubalika au mtu ye yote anayeshughulikia utoaji wa haki, isipokuwa tu kama kumetolewa hoja mahususi kuhusu jambo hilo." Hiyo ni (e). (f) "Hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine ye yote." Inaendelea kusisitiza. Hii yote ni kuleta utengamano na ushirikiano." Vinginevyo, tukiruhusu mambo ya kurusha maneno, Wabunge kwa Wabunge mtapigana na siyo malengo yetu mfikie mahali hapo.

Kwa hiyo, Kiti hiki kipo hapa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mnachangia, mnapata nafasi, mnazungumza kwa uhuru kabisa na niwahakikishie kwamba kila Mbunge ana uhuru asilimia 100 ya kutumia nafasi yake ya Ubunge hapa kama ambavyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano inavyomruhusu. Kwa maelezo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo ambapo Mheshimiwa Zungu ataingia kuongoza Bunge hili. Ahsanteni.

*(Saa 7.11 mchana Bunge lillahirishwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu. Leo ni kikao changu cha kwanza, lakini kwa rehema zake na baraka zenu na heshima zenu, zitanisaidia kuniwezesha kuongoza kikao hiki.

Nilikuwa naomba kusema jambo moja, sisi ni Wawakilishi wa watu na kazi yetu ni kutetea maslahi ya watu. Serikali imetoa bajeti yake, ni wajibu wetu sisi kuishauri Serikali pale ambapo tumeona pana mapungufu ili Serikali waweze kutizama umuhimu au hoja za Wabunge. Tunapoanza kupigana vijembe humu ndani, hatuwatendei haki wananchi wetu.

Kwa kweli mimi naomba na ninawasihi tujadili, na mawazo mengi sana mazuri ya upinzani ambayo Serikali wanayachukua na kuyafanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu, na kuna mawazo mazuri kutoka Chama Tawala ambayo Serikali inayachukua kwa maslahi ya nchi yetu. Naomba tuwe na subira, tuwe na busara, tujiheshimu na tuheshimu nyumba hii ambayo kwa kweli ndiyo inayoleta taa na mwongozo wa Taifa letu. Ahsante. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa kwanza jioni hii ni Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia, na wewe ni mara yako ya kwanza kukalia Kiti hicho, naomba nikupongeze kwa moyo wangu wa dhati kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Mwenyezi Mungu akujalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimpongeze Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri, lakini pia niwapongeze Manaibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao wanaokupatia hatimaye ukaweza kuanda hotuba nzuri ambayo mmeileta ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nitaomba kujielekeza kuhusu reli. Ili kukuza uchumi wan chi hii,

Serikali ni lazima ihakikishe inaimarisha miundombinu ya barabara pamoja na miundombinu ya reli. Ikishaimarisha miundombinu hiyo, nina uhakika kabisa uchumi ambao tunautarajia utaweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, Reli ya Kati ameipa kipaumbele. Naomba nimshukuru kwa kuweza kuliangalia hili, lakini naomba nitoe mchango wangu kwa kusema kwamba, kwa vile kati ya vipaumbele ambavyo amevipanga ni pamoja na Reli ya Kati, naomba basi ahahakikishe pesa zitakazokuwa zimetengwa kupelekwa kuimarisha Reli ya Kati zisiondolewe kule. Pesa zikipatikana, zikipelekwa, zisitolewe kule, zibaki kule kule zikafanye kazi ambayo imepangwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Ukanda wa Magharibi, Mwanza Kigoma, Kagera na Mara pamoja na Rukwa wanapata taabu sana. Wamekuwa ni maskini kutokana na reli kutokufanya kazi kwa muda mrefu. Kwa vile Serikali imepanga kwamba reli itakuwa ni kipaumbele, tunaomba reli iimarishe sambamba na injini pamoja na mabehewa ili vitu hivyo vitakapokamilika wananchi waweze kusafirisha mizigo yao, waweze kupata usafiri wa nafuu ili waweze kuinua uchumi wao na kujongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutokuwa na reli ya uhakika, bidhaa zinazosafirishwa kwenda katika Mikoa hiyo, zikifika kwenye Mikoa ile, zinakuwa ni bidhaa za bei aghali sana kwa sababu viwanda viro Dar es Salaam, bidhaa nyingine kama sukari inasafirishwa kutoka nchi za nje ikifika Dar es Salaam ndipo inaposafirishwa kuja katika Mikoa hii. Sasa utaangalia ni jinsi gani bei zinavyoongezeka kutokana na usafiri wa kusafirisha mizigo kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, Kigoma, Kagera, Mara na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mfuko wa sementi Dar es Salaam ni Sh. 18,500/=, Kigoma ni Sh. 22,000/=. Angalia

tofauti iliyopo hapo. Mfuko ukiutoa Dar es Salaam ukaupeleka Kigoma, unafika kwa Sh. 22,000/=, utaangalia gharama za usafiri ni kama Sh. 6,500/= kama nitakuwa nimepiga hesabu zangu sawasawa. Lakini sukari kilo 50 ikifika Kigoma na Mikoa mingine ninayoisema ni Sh. 93,000/=.

Si hivyo tu, nauli ya treni kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa bei ya kawaida ni Sh.19,000/=, lakini kwa bei ya kuruka ni lazima niseme kwamba kutokana na shida iliyopo ya usafiri wa treni, wananchi siku zote hawanunui tiketi kwa bei halali, wanunua kwa bei ya kuruka. Badala ya Sh. 19,100/= wanunua tiketi kwa Sh. 30,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kutokuwa na usafiri wa uhakika, wananchi wenyewe kipato cha chini wakitaka kusafiri kutoka Kigoma kuelekea Dar es Salaam nauli wanayotoa kwa mabasi ni Sh. 55,000/=. Angalia tofauti iliyopo. Sh. 55,000/= na Sh. 19,000/=! Wananchi wanapoteza pesa nyingi kwa kutokuwa na usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali kwa kuwa imeamua na kwa kuwa ni Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, ikiamua inaweza kutekeleza. Kwa hiyo, naomba kabisa haya yote ambayo naomba yafanyike, Serikali iyachukue kwa moyo wa dhati kwa kuwasaidia wananchi hawa ambao wanapata shida kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni lango kuu la uchumi. Mwenyezi Mungu ametujalia fursa hiyo, lakini sisi wenyewe bado hatujaweza kuitumia fursa hiyo. Ukiangalia mizigo ambayo inasafirishwa kwenda *DRC*, mizigo inayosafirishwa kwenda Burundi, Zambia, kama kweli tungkuwa tumeimarisha reli yetu ya kat, mizigo yote ingeweza kusafiri kwa njia ya treni, ingeweza kufikishwa katika bandari ya Kigoma, ingeweza kuvushwa kwenda Burundi, *DRC* na sehemu nyingine kwa bei ambayo ni nzuri na tungeweza kuinua uchumi wetu na tungeweza kuongeza kipato chetu kwa kutumia reli yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa reli, kunachangia sana kuharibika kwa miundombinu ya barabara. Leo hii ukiondoka hapa kuelekea Kahama, ukifika Sekenke kuelekea Igunga, barabara imeharibika sana kwa sababu malori makubwa yanapita yenye uzito mkubwa. Kwa hiyo, barabara imeharibika kabisa. Kwa hiyo, tukiimarisha reli yetu, tuna uhakika tutazitunza barabara zetu, tutaendelea kuimaisha uchumi wetu, lakini kama hatutaimarisha reli, tujue kabisa kwamba barabara tutakazokuwa tunazitengeneza kila baada ya mwaka mmoja au miwili zitakuwa zinaharibika.

Kwa hiyo, badala ya kusonga mbele, tutakuwa tunarudi nyuma kuendelea kutengeneza barabara. Pesa ile ambayo tungeweza kuichukua kuipeleka kuhudumia katika vituo vya afya, kuhudumia Shule za Sekondari zitakuwa zinarudi kwenda kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itusikie sana wananchi tunaotokea Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipoisemea barabara ya Kigoma - Nyakanazi, kwa kweli mimi mwenyewe nitakuwa nimejipunja. Mwaka jana tulitengewa pesa, Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya barabara ya Kigoma - Nyakanazi, lakini mpaka sasa hili mimi napita barabara ile kila siku sijaona kitu kinachoendelea. Ninaomba sasa kupitia Bunge hili, barabara ile ya Kigoma - Nyakanazi iweze kutengenezwa, kwa sababu barabara ile ndiyo inayounganisha Wilaya zote za Mkoa wa Kigoma, na kwa sababu kila siku tunaimba Kilimo Kwanza, barabara ile ndiyo inayosafirisha pembejeo na mazao kupeleka sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba barabara hiyo itengenezwe ikamilike kusudi wananchi wa Mkoa wa Kigoma waweze kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, imeufungua Mkoa wa Kigoma. Barabara ya Kigoma - Mwandiga imekamilika, barabara kutoka Mwandiga kuelekea Uvinza - Tabora nayo inatengenezwa, daraja la mto Malagarasi ambalo lilipewa jina la Mheshimiwa Kikwete nalo linaendelea kujengwa. Kwa hiyo, nina imani na barabara hii ya Kigoma - Nyakanazi nayo itaweza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie maji. Ziwa Tanganyika lipo katika Mkoa wetu wa Kigoma, lakini pamoja na kuwa na Ziwa katika Mkoa wetu, Wilaya ya Kigoma hakuna maji, Kasulu hakuna maji na Kibondo hakuna maji. Naomba basi tuweze kutengewa pesa kwa ajili ya kwenda kutoa maji Ziwa Tanganyika na kwenda kusambaza katika Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado Kigoma tuna vyanzo vikuu vya mito, tuna mto Malagarasi. Kwa kutumia mito hiyo, bado tunaweza tukapata fursa ya kupata maji kwa wingi. Vile vile kwa kutumia vyanzo hivyo, tulivyonyavyo, tunaweza hata tukaimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia vyanzo vya maji vilivymo ndani ya Mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itusaidie watu wa Kigoma kuelekeza miundombinu ya maji katika Mkoa wa Kigoma ili tuweze kunufaika kwa kutumia Ziwa Tanganyika na Mto Malagarasi kwa ajili ya kupata maji na kwa ajili ya kupata kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia vyanzo vyetu vya maji tulivyonyavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri kwamba Serikali imepanga kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya Wami, Ruvu, Kilombero na Malagarasi. Naomba Serikali kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi, isiwasahau wakulima wadogo wadogo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza msemaji wetu wa pili ajiandae, na Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo watafuatia.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kujadili bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kutoa masahihisho kwa wachangiaji ambao walikuwa wanasema kwamba bajeti ya CHADEMA ilikuwa haionyeshi tarakimu ya matumizi ya bajeti. Ninachotaka kusema katika Bunge hili na wananchi wanatusikia ni kwamba kulikuwa na *typing error* ambayo haikuonyesha, lakini tarakimu zimeonyeshwa, inaonyesha mapato ya kodi *TRA* ni Shilingi trilioni 10.2, mapato yasiyo ya kodi Shilingi trilioni 1.168, mapato ya Halmashauri Shilingi bilioni 4.9 ambayo inaonyesha jumla yake ni Sh.11,889,078,000,000/=. Kwa hiyo, hizo ni *typing error* ambazo hata wakati mwingine zinatokea hata katika vitabu vya Serikali. Wananchi wanaskia na tunasahihisha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kuna baadhi ya wachangiaji au mchangiaji ambaye alisema na hasa alitulenga sisi Wabunge wa Kambi ya Upinzani kwamba Serikali imetujengea Bunge, imetujengea jumba safi lenye viyoyozi na tunajiviringisha hapa katika viti. Napenda kusema hivi, wakati tupo ndani ya jengo hili, ukitoka hapa kilomita mbili utakutana na nyumba za tembe. Kwa hiyo, hatuwezi kujisifu na kujivuna kwamba tupo

katika nyumba hii ambayo ina viti na viyoyozi wakati Watanzania kilomita mbili kutoka hapa wapo kwenye nyumba ambazo zimeezekwa na udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo imetokana na mfumo mbovu wa kiutawala pamoja na mfumo mbaya wa kibajeti ambao leo hii ndiyo tunajadili kuona ni jinsi gani bajeti hii inaweza kuleta maisha mazuri ili tujivune kwamba tupo ndani ya Bunge kwenye viyoyozi, lakini Watanzania wenzetu nao wanaweza kuwa na makazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga bajeti hii mkono kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, bajeti hii ukiangalia katika matumizi ya Serikali ambayo yamekuwa ni kilio cha muda mrefu katika nchi yetu ambayo *NGOs* zimesema, waandishi wa habari wamesema, watu mbalimbali wamechangia bajeti ya mwaka jana na zile za nyuma hatu kabla hatujaja kwenye Bunge sisi watu wengine zimekuwa ni bajeti zinazoonyesha kutumbua tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoandaa hii bajeti na hasa bajeti ya matumizi inalenga baadhi ya watu fulani. Ukitazama katika kitabu cha bajeti ya matumizi, utashangaa sana. Utaangalia jinsi watu wanavyoomba kutengeneza *furniture* kila mwaka. Mimi najiuliza, tumekaa hapa kwenye viti hivi mwaka mzima, mbona havijachakaa? Ina maana wale watu wengine wanaokalia viti katika ofisi, makalio yao yana misumeno! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi kama haya watu wanunua *furniture* kila mwaka, watu wanaomba kula vitafunio, chapati, maandazi, chai ndiyo imejaa kwenye kitabu cha bajeti hii. Naomba Serikali ya CCM ijiondoe katika anasa. Magari ya kifahari, matumizi yasiyokuwa ya lazima ambayo mimi naungana kabisa na mchangiaji mmoja ambaye alisema tunaweza kukata *OCs* nusu tukapeleka katika bajeti ya

maendeleo ambayo kwa kweli haitekelezeki. Siwezi kusema *data* kwa sababu tunaposema uchumi wa wananchi, tuangalie hizi *data* ambazo mama yangu kijiji na ndugu zangu hawawezi kusoma *GDP*, hawawezi kutuambia kwamba gharama ya Dola imekuwa hivi sijui nini, hawaelewi! Wanachotaka kuona ni maisha yao ya kila siku. Je, umeamkaje asubuhi, umeweza kupata chai, umeweza kufua, umeweza kupata chumvi, mafuta ya taa? Huo ndiyo uchumi wa watu wa kawaida na hiyo haitaki digrii.

Mimi nasema huo ndiyo uchumi wangu. Uchumi wangu mimi hauhitaji kwenda shule, kwa sababu watu waliokwenda shule, ndiyo hawa walikuwa wanatuambia walikuwa kwenye mabenki, lakini pamoja na kwamba waandamizi wa mabenki wapo humu, bado Shilingi yetu inateremka kila siku na bado mfumko wa bei unakuwepo. Kwa hiyo, hatuwezi kujadili kwamba eti kwa vile mtu ana digrii kumi za uchumi, ndiyo anaweza kupanga haya. Tunachotaka ni bajeti ilenge watu walio chini, tutoe matumizi makubwa ya Serikali ambayo hayana ulazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema na Waziri Mkuu wetu amewahi kutamka hapa na hata katika Mikutano kwamba jamani tupunguze matumizi ya magari, haya mashangingi, Waziri Mkuu naona wenzako walikuzidi kete. Naona walikuzidi nguvu, *otherwise* wangeweza kuondoa matumizi makubwa ya magari yasiyokuwa na lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika randama, watu wanaomba kununua betri milioni ishirini, wewe unaonunua betri kwa bei gani? Kwa hiyo, utaona matumizi ni mengi. Ukisoma randama hizi, utaona mambo ya kushangaza. Mimi kwa kweli kwa hilo nasema Serikali ya CCM acha kutumbua, acha anasa, Serikali ni mali ya watu, Viongozi tuishi maisha ya kawaida ili tuweze kusaidia watu wetu wa ngazi ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme juu ya reli ambapo mwenzangu ambaye ameguswa na reli amesema. Nimekuwa nikiangalia katika Mpango wa Maendeleo ukurasa wa 23 na ukurasa wa 24, hakuna dhamira na utashi wa kisiasa wa kutengeneza Reli ya Kati mpaka Mwanza. Ni kwa sababu gani? Kwa sababu watu, Maofisa, Viongozi Wakuu wamenunua magari wakaweka barabarani, nani atakubali gari lake likae chini kutengeneza reli? Hamwezi kutengeneza reli kwa sababu ya mambo ya kibinafsi.

Tunaomba mtutengenezee reli, watu wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa, watu wa Kagera ili tuweze kuondokana na gharama kubwa za maisha za kununua vifaa vyta ujenzi na vyakula kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka jana, 2011 wakati nachangia Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, nimejitahidi nikasema mpaka nikadai meli yetu ya umoja iko wapi? Mliipeleka wapi? Hakuna majibu! Sijui mliuza! Maana yake ilikuwa inatusaidia kubeba mabehewa kutoka Mwanza mpaka Bukoba. Sasa hivi meli hiyo illingia mitini, hatuioni. Mheshimiwa Waziri atujibu, hata wakati wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi, kama sitapata nafasi, mtujibu hiyo meli mmeipeleka wapi kwa manufaa ya watu wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee deni la Taifa. Kupitia Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alituonyesha kwamba wakati Serikali ya Awamu ya Nne inaingia madarakani, nchi hii ilikuwa inadaiwa Shilingi trillioni saba tu. Sasa tunaambiwa tunadaiwa zaidi ya Shilingi trillioni 20. Ina maana katika miaka 40 ndani ya Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, na Awamu ya Tatu tulikuwa na deni la Shilingi trillioni saba? Sasa inakuwaje ni mara mbili yake na wala hailingani kabisa na maendeleo yaliyopo? Awamu ya Kwanza ilijenga viwanda, vyuo na miundombinu mbalimbali. Lakini sisi hizi fedha zinatumikaje? Ndio hoja ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri iundwe Kamati ya kuangalia deni hili linakopwa kweli, maana yake ukiangalia Sheria ya Usimamizi wa Madeni, yaani *Loan Guarantee and Grant Act* ya mwaka 1972 kweli inamwelekeza Waziri wa Fedha kukopa lakini kwa kupitia Kamati ya Usimamizi ya Deni la Taifa. Lakini kwa taarifa zilizopo ni kwamba, Waziri amekuwa akikopa peke yake bila kwenda kupitia katika Kamati hiyo na Kamati haifanyi kazi. Kwa hiyo, matokeo yake hili deni linakua. Nawaambia kwamba huko mbele kama hatuangalii, hii itatuweka katika *crisis* za madeni kama nchi nyingine kama Ugiriki, na kama tulivyoona mambo yanakuwa mabaya. Kwa hiyo, naona kuna haja ya kuunda Tume, kuangalia hili deni linakua kwa sababu gani? Linakua kwa *percentage* katika miaka saba. Huko nyuma nimeiambia Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni watumbuaji, acheni kutumbua, tengeneza miradi ya maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bajeti hii ni bajeti ambayo haiwezi kusaidia watu ambao wanalala kwenye nyumba za tembe. Sisi tunajivuna hapa na viyoyozi, watu wanakula mhogo na maji kila siku. Sisi hapa tunajivuna kwamba tumejenga nyumba, nyumba inaweza kuwa ya ufalme hapa tukakaa, lakini huko nje hatujui kwamba watu wanakosa mkate. Kwa hiyo, tuangalie mambo hayo, turudishe bajeti hii, tuichanechane Waziri wa Fedha aiangalie apunguze matumizi, hizi OC's hapa ndiyo kuna dilli za kuwaibla Watanzania. (*Makofii*)

Hata ukiangalia mfumo wenyewe wa matumizi haya, unagusa baadhi ya watu tu. Hauwezi ukagusa wafanyakazi, kwa mfano, wahudumu, wafagiaji hawaguswi; wale hawapati chai. Mimi nina ofisi yangu pale Mkoani, najua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika matumizi mabaya, haraka haraka niguse Mkoa wangu wa Kagera. Kuna mradi wa Kabango B, Serikali ilitoa Shilingi bilioni 1.8 wamekwenda kule Shilingi bilioni 1.8 wamekwenda kujenga kichuguu. Ndugu

yangu hata Kamati ya *PAC* imekwenda pale mpaka *RAS* amekubali, sasa mmewatengea huku kwenye kitabu Shilingi milioni 75, kufanya nini? Warudishe kama *RAS* amekubali. Kwa nini wasirejeshe hizo fedha ndani ya matumizi? Yamekuwa ni matumizi katika nchi nzima kuanzia Halmashauri, huko kwa *RAS* halafu tunajidai tunatengeneza bajeti. Bajeti ambayo haisimamiwi, bajeti ambayo matumizi yake ni holela holela, yaani kila mtu anasema. Yaani hii Serikali ya CCM ni nyumba ya kambare ndugu yangu. Maana yake hata kama mtu anaiba hatuchukui hatua. Kwa hiyo, sasa tusemeje? Hakuna sababu. Ahsante. (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji amerekebisha kwenye matumizi, lakini kile alichorekebisha sicho sisi tulichoongelea kwenye matumizi. Kwenye mapato, ndiyo tulisema wameweka 000 lakini kwenye matumizi kitu walichorekebishi, a sisi tulisema kiuchumi na kiutalaam popote pale hauwezi ukawa na matumizi yenye 000 mwishoni hii ni *forgery*, ni namba ya kubandika, haina *addition* ya aina yoyote. Hauwezi ukapanga matumizi ya nchi nzima halafu ukapata *exactly figure* yenye tisa sifuri sifuri mwishoni. Hii imebandikwa tu kama ya vitumbua vile. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, tumekuelewa.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kwa kupata nafasi na naomba nikupongeze kwa kushika Kiti hicho leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kama Mheshimiwa Mcemba alivyosema kwamba huwezi kungojea mpaka dakika ya mwisho watu wamesema, halafu ndio unasema kuna *error, error*, ambayo hukuiona kabisa huku mpaka unasoma umemaliza hilo pemberi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kusema, naunga mkono hoja. Lakini pia nampongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake pamoja na Watendaji kwa bajeti hii nzuri ambayo wametulea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nisisimame hapa bila kusema masikitiko yangu kwa jinsi kijana mdogo anapoweza kumtukana mtu mkubwa na hasa akiwa ni kiongozi wa nchi. Maadili yetu ya Kitanzania hayaruhusu hilo. Mimi nafikiri kama kweli ni kijana wa Kitanzania, basi atajiliza, atajitafakari na ataomba radhi kwa hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nitoe marekebisho ya kupotoshwa kwa maneno hapa. Mimi ni mmoja katika Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Nilisikitika sana na nilishangaa nilimpomsikia Mheshimiwa Mbunge akisema eti Kamati imekataa bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, kitu ambacho siyo kweli, ni uongo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Wizara ya Afya na Elimu pamoja na kuwa Wizara ya Afya na Elimu, lakini pia TAMISEMI inashughulika na Afya na Elimu. Kama iliagiza ikawaambie kwamba tunataka kuona takwimu za TAMISEMI ili kusudi tupate kuona uhakika wa kiasi gani cha fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya afya na elimu. Kwa hiyo, kwa sababu ilikuwa Dar es Salaam, TAMISEMI ilibidi wakusanye takwimu, ikabidi lazima tuje Dodoma na tulikaa chini. Mimi nasema mtu mzima anaposema uongo anakuwa na maslahi yake binafsi. Lakini kama hilo siyo, tulipokuwa Dar es Salaam, Mheshimiwa Mbunge huyo huyo alikuwa anajaribu kupita kwa wenzie na kuwashawishi kwamba tukatae bajeti nzima na wala tusishiriki. Alipoona wenzie wamemkatalia, ikabidi na yeye akae asikilize. Kwa hiyo, akaona aje kuwapotosha wananchi wa Tanzania. Mimi nawaambia Watanzania, siyo kweli. (*Makof*)

Kwa nini tulitaka tupate uhakika wa bajeti hiyo ya TAMISEMI? Kwa sababu kulikuwa na vitu muhimu sana. Pamoja na hivyo, fedha zilizotengwa kwa ajili ya madawa tulitaka tujue Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unazungumzia kujenga VETA, tulitaka tuone fedha za VETA ziko wapi. Kuna matatizo ya mafao ya Madaktari na Sekta nzima ya Afya tulitaka tuone viko wapi na baada ya kuviona na mimi nasema Serikali yetu ni sikivu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni msikivu sana. Tulimwendea na alipoombwa kwamba hii inaweza isikidhi, alisikiliza na alifanya marekebisho. Mheshimiwa Waziri endelea na hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mchango ufuatao kwenye bajeti hii. Ni kweli kabisa kwamba bajeti yetu upande wa maendeleo tulikuwa tumeegemea sana kwenye fedha za nje. Mimi nashukuru katika Wizara ambazo tulizishughulikia na ndiyo kazi ya Kamati, nashangaa watu wanakuja kupiga kelele hapa badala ya kuzisaidia kama tulivyoambiwa kuvisimamia Serikali na kuishauri kwenye Kamati, kwenye Kamati ndio tulikuwa tunatakiwa tuwashauri. Tuliwashauri kwamba yale maendeleo nyeti wayatoe katika fedha za nje na wayapeleke katika fedha za ndani na walifanya hivyo. Kama hiyo siyo Serikali sikivu ni kitu gani? Kwa hiyo, nilikuwa nina mawazo kwamba, pamoja na yote, Serikali ni lazima iongeze makusanyo ya fedha. Katika makusanyo ya fedha, kuna vyanzo vingine vingi pamoja na kuangalia hizi fedha ambazo zinapatikana kutoka sehemu mbalimbali pamoja na kutaka Serikali iangalie kodi kama za migodi, Makampuni ya Simu. Lakini na sisi wenyewe kila mwananchi ambaye anaweza kuchangia maendeleo achangie. Sasa najiuliza, hizi hela za kodi za majengo zinakusanywa? Hazikusanywi. Ni kwa nini basi Serikali za Mitaa tusiwape kazi hiyo? Siyo ya kukusanya, ya kuratibu, ili kuhakikisha wale wa Serikali za Mitaa wanajua kila mahali nyumba gani ipo na kama inalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri alichukue hilo na waliangalie jinsi gani wanaweza kulifanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nakubaliana kabisa na suala la kupunguza kodi ya boda boda, lakini ninauliza: Hizi boda boda ni za hawa vijana au vijana hawa ni madereva wa hizi boda boda? Maana yake ziko za hawa vijana, lakini ziko nyingine siyo za vijana hawa. Je, wale wamiliki wengine wa boda boda ambaye mtu mmoja ana boda boda kumi anakodisha kwa kupata Sh. 15,000/= kwa boda boda moja, tunaacha bila kuchukua kodi hapo? (*Makofi*)

Lingine, ni Wamachinga ambao wako wengi sana, wafanyabiashara ndogo ndogo. Hivi mmachinga gani ambaye ameshafunga safari kwenda China kwenda kuingiza makontena ya vitu ambavyo wanauzu? Siyo kwamba wanapewa, sisi Dar es Salaam kuna kitu kinaitwa mali kauli, unakwenda, unapewa mzigo, unakwenda kuuza. Ukishauza, unapeleka hela za tajiri. Yule tajiri sisi tuna hakika gani kwamba hawatumii machinga kukwepa kodi? Naomba Serikali illiangalie hilo. Kuna wafanyabiashara wengi sana wanakwepa kodi kwa kutumia hilo. Kwa hiyo, wanawatumia wamachinga kwa ajili ya kujinufaisha wao wenyewe. Hilo naomba tuliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma bajeti kivuli, lakini linanipa taabu sana neno kivuli. Sisi tunapokaa kwenye Kamati, tunakaa wote pamoja, tunatoa mawazo yetu, na kama Kamati yetu imesheheni wasomi Madaktari, Mafamasia, Manesi, Walimu wamo mle. Mtu anasikiliza tokea mwanzo mpaka mwisho halafu anakwenda kuandika, anasema hiyo ni *speech* ya Waziri Kivuli. Hivi ni ya kwake kweli? Wakati kakaa mle ndani na mwingine anatoka hata katika Kamati nyingine anakuja kwenye ile Kamati anakuja kukaa anasikiliza halafu anasema hiyo ndio bajeti ya Waziri Kivuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wazo. Kwa nini isiundwe Kamati nyingine ya Mawaziri Vivuli ili kusudi wakae wajadili kama ilivyokuwa *cabinet* yetu? Basi kuweko na *cabinet* nyingine ya Waziri Kivuli ambayo watacaa wawe na *idea* zao ili wasiwadanganye Watanzania kwamba ni *idea* zao, kumbe ni *idea* za wana-CCM ambaa ndio tunazungumza. (*Makofi*)

Mimi sikubaliani kabisa kwamba zile *idea* ni zao kwa sababu tunaona wanayoyaandika. Wanayoyaandika ni yale ambayo tumeyajadili kwenye Kamati. Tena mwingine hata Kamati siyo ya kwake, lakini anakuja na anadiriki kujitambulisha mimi Waziri Kivuli wa mahali fulani, wa Wizara fulani. Unakuja kutusikiliza sisi, unasikiliza hoja zetu, unachuma akili zetu, unakwenda kuandika. Sana sana unaongeza na mengine yaliyokuwa kwenye mtandao baada ya kuwaauliza kwenye *twitter* pamoja na *forum*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiwaongopee Watanzania, bajeti ni nzuri, imeangalia mambo mengi, imeangalia makusanyo, imeangalia jinsi ya kupunguza makali ya maisha. Tunachokizungumza humu ndani, wengine wanatoa maneno ambayo siyo ukweli, siyo ya kwao, yanasemwa na mengine ninadiriki kusema ni uongo mtupu. Kwa sababu amezungumza akasema bajeti hizo hazikupitishwa wakati sisi tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Afya, tumepitisha Bajeti ya Wizara ya Elimu baada ya kwenda kuifanya marekebisho. (*Makofi*)

Meshimiwa Waziri, narudia tena kukushukuru kwa jinsi ulivyokuwa na upeo mpana na jinsi unavyokubali ushauri na unavyokubali kusaidia pale mahali ambapo pamekwama. Kamati yetu umetusaidia sana na kuhakikisha kwamba tunakwenda kuwatendea wananchi yale ambayo walikuwa wanayatarajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema tena, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

## TAARIFA

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (8), nikiomba kumpa taarifa mzungumzaji ambaye amekaa chini muda mfupi uliopita anapaswa kuelewa kwamba ni haki ya kila Mbunge kuweza kwenda kwenye Kamati yoyote kusikiliza na kupata taarifa na kuweza kuzitumia kwa maslahi ya Bunge letu na kwa maslahi ya wananchi. Kwa hiyo, asilalamike kwa namna yoyote ile kwamba Mheshimiwa Mbunge fulani alikwenda kwenye Kamati fulani na kuchukua taarifa kwamba alikuwa kwenye *wrong position*. Hata masuala ya kutumia mitandao kwa lengo la kuweza kupata taarifa ambazo ni sahihi, siyo kosa kwa mujibu wa Sheria zinazoongoza nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hiyo aichukue, na kama alikuwa hajui, basi afike, tutamfundisha. Ahsante.

*(Hapa Mheshimiwa Zarina S. Madabida alisimama  
kutaka kusema kitu)*

**MWENYEKITI:** Kaa chini Mheshimiwa Madabida. Tunaendelea na Mheshimiwa Felix Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchambua bajeti hii ya Shilingi trilioni 15. Nianze kwa kueleza kabisa kwamba wananchi wa Kibondo kule Kigoma waliniagiza kwamba nisiunge mkono bajeti ambayo hailengi kuwaletaa maendeleo, bajeti ambayo kila siku mnaongeza Mikoa. Tunawaambia, tubadilishe mifumo ya uongozi. Hii ya kuongeza Mikoa, mnaongeza matumizi ya nchi. Watu hawajawaambia wanahitaji Wakuu wa Wilaya. Badala ya kupeleka Zahanati, mnanunua Ma-V8 ya kuwanunulia Wakuu wa Wilaya wapya. Wananchi hawahitaji hayo mambo. Hawajawaambia wanataka Wakuu wa Mikoa mipya, hayo ni namna ya kutafuta

jamaa zenu muwape nafasi za kisiasa. Wananchi wanataka Zahanati na elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo tuna ushahidi, hatuwezi tukaunga mkono bajeti hii kwa sababu bajeti iliyopita kwanza imewashinda kutekeleza. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu unisikilize vizuri, kwa sababu tulikubaliana na Spika hapa kwamba hakuna Mbunge kuzungumza na wewe tunapokuwa tunazungumza. Naona hatoki sasa! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Endelea, anakusikiliza.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Nataka asikilize maoni ya wananchi wa Kibondo kwa umakini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali kaa chini. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mzoefu wa kila eneo na anakusikiliza.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, ngoja niendelee. Bajeti ya mwaka jana imewashinda kutekeleza na naomba Mheshimiwa Wasira wakati mnaandika bajeti hii siyo muanze kwa kusema kwamba ilikua kwa asilimia Fulani, ukilinganisha na asilimia fulani mwaka fulani wakati jambo limepungua. Naomba muwe mnaeleza kabisa kwamba Sekta ya Uvuvi imeshuka chini kwa kiwango hiki. Hiki ni kitabu chenu, ngoja tuwaonyeshe hapa mlivyoshindwa kuongoza nchi hii. Kilimo, Mifugo, Misitu na Uwindaji imeshuka kutoka asilimia 4.2 mwaka 2010 mpaka asilimia 3.6, mwaka 2011 mmeshindwa kuwakomboa wakulima, mifugo, misitu na uwindaji mmeshindwa. Uvuvi umeshuka kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 mpaka 1.2 mwaka 2011. Kwa hiyo, mmeshindwa tena kwenye uvuvi. Viwanda na ujenzi imeshuka mwaka 2010 ilikuwa 8.5 mwaka 2011 imekwenda 6.9. Kwa hiyo, mmeshindwa tena kwenye ujenzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa viwandani pia Chama cha Mapinduzi mmendelea kushindwa kutoka asilimia 7.9 mpaka 7.8. Kwa hiyo, mmeendelea kushindwa. Kwenye umeme na Sekta Ndogo ya Gesi ilikuwa 10.2 mwaka 2010, mwaka 2011 ni 1.6, kwa hiyo, mmeendelea kushindwa kwenye kila sekta. Sekta Ndogo ya Ujenzi nayo ni hivyo hivyo; usambazaji huduma za kijamii hivyo hivyo. Kwa hiyo, mwandike mwonyeshe namna gani mnashindwa kuongoza Taifa, siyo kuanza kwa kueleza kwamba imekua kwa asilimia *something* wakati imepungua. Wakati imepungua, elezeni hali halisi kwamba tumeshindwa kwenye kilimo, tumeshindwa kwenye ujenzi, tumeshindwa kwenye nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii watu wameshindwa kukusanya kodi na hatuwezi tukavumilia haya mambo hata kidogo. Haiwezekani Waheshimiwa Wabunge tuwe tunazungumza haya mambo. Kuhusu mitandao ya simu, kwa nini haujaleta *amendment* ya mitandao ya simu kama mlivyoleta kwenye *amendment* ya mitandao mingine. *Vodacom* peke yake kwenye huduma ya M - PESA wamepitisha Shilingi trilioni 6.6 ambazo hizo fedha hawajalipia kodi, mnawatoza *corporate tax* peke yake, huduma nyingine wanazofanya hamwatozi.

Kama *Vodacom* peke yake wanaweza kufanya *transaction* ya Shilingi trilioni 6.6, acha *Tigo*, acha *Airtel*, acha Z - Pesa na vitu vingine mmeshindwa kukusanya kodi. Leo Halmashauri zetu zimeshindwa, siyo kwamba wameshindwa huku, hii Serikali imeshindwa kukusanya kodi kuanzia vijijini mpaka juu. Mnaweza kukusanya kodi kwa kuwakata wafanyakazi pekee yake. Mgeanzia chini, kuanzia vijijini mpaka juu mmeshindwa kukusanya kodi. Mnaweza kukusanya kodi kwa kuwakata wafanyakazi pekee yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye sehemu nyingine ambayo ni ajira kwa vijana. Ukisoma hiki

kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa, unaona takwimu zenu ni za mwaka 2006. Soma ukurasa wa 111 na ukurasa wa 112 utaona kabisa takwimu za ajira nchi hii haina. Hajui watu wangapi wamemaliza shule, watu wangapi wameajiriwa, wakulima wangapi wana mashamba nchi hii, hawafahamu. Wanatuletea mambo ya kubabaisha babaisha hapa. Hii Serikali ime-*paralyse*, tunatakiwa tubadilike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuja unazungumza kwamba utatatua tatizo la ajira kwa takwimu ambazo mmekuwa mnazirudia mwaka jana, mmetuletea takwimu hizi hizi za mwaka 2006, sasa hivi mmetuletea takwimu hizi hizi, vijana hawatakubali. Tumechachamaa, tumeanza kuja Bungeni na mwaka 2015 tutaongezeka kwa kasi kuja kukomboa Taifa letu. Hatutawavumilia hata kidogo mwendelee kufanya mambo ya namna hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie eneo lingine. Nchi hii sasa hivi imekuwa na tatizo kubwa, ujisadi umezidi kila sehemu, wazee wastaa fu mnasema hamwezi kuwaongezea pensheni. Hivi mnazungumza vitu gani? Leo hata hii pensheni ambayo wanaipata haiwafikii, watu wanakaa zaidi ya miezi sita, wazee hamwapelekei pensheni! *PSPF* sijui wapi, mnafanya nini? Pesa hizi mnaziingiza kwenye ma-fixed accounts huko, mnashindwa kuwapelekea wazee, wanakaa zaidi ya miezi sita, huu ni ujisadi kwenye Taifa hili. Hatuwezi kuvumilia. Mmeshindwa kuongoza Taifa, Sekta za Uchumi zinashuka, mnatupangia Shilingi bilioni 300 uchukuzi, mnategemea nini? Reli ndiyo itaboresheka hii? Nnazidiwa na Wajerumani toka mwaka 1905 mpaka leo, ninyi mmeshindwa! (*Makofii*)

Badilikeni jamani! Halafu tunapozungumza haya mambo, msione kama vile hawa watu wanakuja wametushukia. Mambo yamewashinda! Mmeshindwa kuongoza Taifa, sasa kwa nini tusiseme? Hali ya maisha inazidi kuwa ngumu, bidhaa zinapanda bei, hata mtu, chukua hata mtu yejote...

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Naona Waziri wa Nchi ana wasiwasi kidogo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapaswa kuangalia upya namna gani nchi yetu tuiongoze. Hawa watu nadhani imefika muda wa kupumzika. Nchi hii watu hawafuatilii, hawajui *data*, wameshindwa ku-*collect data* mipakani. Tunauliza maswali, sisi watu tunaotoka maeneo ya pembezoni, fungueni mipaka watu waingie wafanye biashara mpate kodi. Mmeshindwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza swali hapa mwaka 2010 tumeingia Bungeni hapa, Soko la Kibondo pale Mkarazi mtajenga lini ili ule mpaka ufunguke? Nimekwenda Burundi, navuka kwenye Jimbo langu kwenda Burundi nakuta bendera za Afrika Mashariki zinapepea pale mpakani, nyie huku mnashangaa. Gari kule inaingia *free*, huku mnawazuia kuingia wasifanye biashara. Mtapata kodi wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wabadilike, wamechoka! Leo ukiangalia kwenye makabrasha, bajeti za Mikoa zinatofautiana hata kwenye mishahara. Yaani wafanyakazi kwenye Mikoa ni tofauti, Mkoa huu *basic salaries and allowance* wanazidiwa na Mkoa mwingine. Kwa nini msiwe na mfumo unaoeleweka ambao kila Mkoa utakuwa na wafanyakazi 30, ma-*secretary* ni wale wale. Kwa hiyo, wameshindwa kila sehemu. *Message sent.* Najua mnakataa, lakini ndio hivyo. Bajeti ya *administration and management* ya Kilimanajaro na Kigoma ni tofauti wakati kazi ni zile zile na Mikoa ni ile ile. Kwa hiyo, lazima mfike sehemu muwe na uelewa wa haya mambo.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Oooh! Aaah!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uwazuie kuzomea, kwa sababu yamewagusa sasa wanaumia. (*Kicheko/Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa. *Order please!* Sasa namwita Mheshimiwa Kayombo, halafu Mheshimiwa Dkt. Shekifu na Mheshimiwa Mansoor Shanif mjiandae.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nafasi hii ya kufika kipindi hiki na kutupa amani hadi sasa. Lakini pia napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mgimwa kwa kazi nzuri aliyofanya; lakini pia na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Mahusiano na Uratibu) - Mheshimiwa Wasira. Lakini pia napenda kuwapongeza Watendaji wao waliowasaidia. Vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Mbanga na hasa wale viongozi waliosaidia sana kuanzisha mtandao wa wakulima wa kahawa na sasa hivi wanaendelea kuanzisha vikundi vyakulima wa mahindi na mazao mchanganyiko. Lakini pia niwapongeze vijana wale wanaoendesha bodaboda kwa utulivu na ukomavu waliouonyesha, na nampongeza sana Mkuu wa Wilaya kupitia *DAS* wake kwa mazungumzo waliofanya na kuleta amani katika Mji wa Mbanga na kwamba sasa tunaweka ombi hapa mbele ya Serikali, kodi katika boda boda ziondolewe ili wananchi wa Vijiji waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi ulio mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na ninazo sababu, lakini kabla sijafika hapa, nilipokea simu kutoka Mbanga ya kijana, anasema Mheshimiwa Mbunge, yule Mbunge kijana mwenzetu aliyetolewa kule Bungeni atalipwa posho yake ya leo? Ameongea kwa masikitiko makubwa sana. Kwa hiyo, rai yangu kama mtu mwenye umri mkubwa kidogo, nafurahi ninapoona vijana wanatoa hoja, wanachemka vizuri, lakini sifurahi wanapokosa mwelekeo katika kipindi fulani. Nilifikiri Taifa limepata vijana wazuri na ambao wananchi walikuwa wanawajengea matumaini. Lakini kwa lugha hizi za matusi, zinatupunguzia zile *marks* zetu. Ni ushauri tu, ningeomba muuchukue. Kwa sababu mimi napenda pia upinzani

uliokomaa, sitaki upinzani legelege ili nchi yetu iweze kuwa imara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho kitabu cha Mpango na kitabu cha bajeti. Bajeti hii ndiyo imetafsiri Mpango huu katika fedha. Sasa Mpango huu Mheshimiwa Wasira alieleza kabisa vigezo vinavyotumika kuchagua miradi ya kimkakati, misingi ya hiyo miradi na imeendelea kutaja miradi iliyoko na katika miradi humu. Kama utaniruhusu ninukuu baadhi. Kuna kituo cha biashara pale Kurasini, kwenye miundombinu kwenye usafirishaji kuna reli ya kati, kuna ukarabati wa reli yenyewe, lakini pia kuna reli ya Mtwara - *Mbamba Bay* halafu nyie mniambie niikatae bajeti hii? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Njombe hawajui reli. Sasa kwa mpango huu, reli inakuja, halafu wewe unaniambia mimi niikatae? Unataka nini? kuna Bandari ya Kigoma iko humu, kuna malipo ya EPZ Kigoma yako humu, halafu mtu anasimama anasema hakuna kitu. Kama tumesoma na tumekwenda shule, lazima tujifunze kuwa wakweli. (*Makofi*)

Hii bajeti siyo nzuri kwa asilimia 100, hata mimi naweza kusema hivyo. Siyo nzuri kwa asilimia 100, lakini ni nzuri. Ina-address masuala muhimu ambayo tumekubaliana. Sasa ni wazi haiwezi kwenda katika kila Jimbo, kila Wilaya kwa mwaka huu kwa sababu inao mpango wa miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yako mambo mazuri sana humu, kwa mfano, Bandari ya Tanga, reli ya Tanga. Mimi nafikiri hawa Waheshimiwa wanastahili pongezi na mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge tungueungana tuseme hivi, tunahitaji Tume ya Mipango iwe na nguvu, ipewe meno, i-supersede Wizara zote ili mipango yao inapopangwa Wizara zifuate. Wizara *translate*, siyo kila Wizara kuwa na mpango wake.

Mimi nafikiri tungesaidia hii Tume ya Mipango, iweze kuwa kweli Tume yenyeye nguvu, maana, mantiki, iwe na meno na ifanye *monitoring* ya haya mambo ambayo tumekubaliana yafanyike. Hatuwezi kuacha Wizara zinajifanyia mambo zinavyotaka. Nafikiri hii ndiyo hoja. Huku kwingine kote, hapa ni Bungeni, jamani siyo uwanja wa mukutano. (*Makofi*)

Mimi nilikuwa nawasihi Wabunge, tuungane, tumsaidie Dkt. Mpango apate nguvu zaidi, fedha zaidi, wataalamu walio bora wawewe kutupangia mipango. Yule mtaalamu ambaye sio wa Jimbo fulani, akae aangalie mawazo yote ya Wabunge na mawazo ya wananchi wengine, Madiwani huko wayakusanye, halafu wapange nchi hii katika kipindi hiki cha miaka 25 ambayo tunataka liwe Taifa ambalo limeendelea. Nafikiri hapo tungekuwa tunaitendea haki hii nchi. Kwa jinsi tunavyokwenda, hatuitendei haki. Tunatumia fedha ya Serikali kukaa hapa kutukana, hili siyo jambo liliro sahihi hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu unashangaa mtu aliyeshindwa kwenye kura za maoni CCM amekwenda Upinzani mara moja amekuwa mzuri sana. *In fact it is the same product. It is the same CCM.* Katibu Mkuu wa Chama ametoka huku huku. Ni nchi moja hii. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri niyaseme hayo. Mambo yaliyoelezwa humu ni mazuri, isipokuwa mimi nataka kukosoa sehemu chache. Moja, ni ile Bandari ya Mtwara. Zimetengwa fedha humu kwa ajili ya Bandari ya Mtwara, sasa unapozungumzia Bandari ya Mtwara bila kui-link na Bandari ya *Bamba Bay*, nafikiri hufanyi kitu kizuri sana. Nilifikiri hizi fedha ambazo zimepelekwa Mtwara, zitafutwe fedha za kuweza kuimarisha pia Bandari ya *Bamba Bay* ili iweze kuvusha mazao kwenda Malawi na nchi nyingine kule, hapo tutakuwa tumekamilisha. Hata ikiwezekana, kuna Bandari ya Bagamoyo hapa, hii Bandari ni mpya kabisa, hata kama tunaiahirisha kwa

mwaka huu ili tukamilishe ya *Bamba Bay*, nafikiri litakuwa jambo zuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni uwekezaji. Kuna mradi wa umeme. Pale Ngaga kuna mradi ambao uko pamoja na NBC, hausemwi katika hivi vitabu hata kidogo. Wale wawekezaji wameanza kuchimba makaa ya mawe, wanaauza hapa ndani na wanaauza nje ya nchi. Wanashindwa kujenga *power station* kwa sababu hakuna Gridi ya Taifa pale.

Kwa hiyo, fedha hizi zingeweza kutatua tatizo la umeme. Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri wa Fedha jambo hili analifahamu vizuri, atafanya haki. Pia, kuna kilio cha watu wa Pamba. Nguo zetu wanazosalisha ni ghali, ondoeni hiyo VAT ili hizi nguo waweze kutengeneza kwa wingi. Tulimtembelea Bwana mmoja anashindwa kuzalisha kwa sababu hazinunuliwi. Kwa hiyo, inabidi aanze kuagiza shuka kutoka nchi za nje badala ya kucaa nguo zetu wenyewe. Hili jambo ungeweza kulifiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu. Mishahara ya Watanzania ni midogo sana na badala yake sasa hata pensheni zinakuwa ndogo. Kwa hiyo, tufikirie katika miaka inayokuja kupandisha mishahara ya Watanzania iweze kuwa mizuri zaidi. Lakini pia malipo kwa wafanyakazi wetu wanaokaa vijijini. Siku hizi benki nyingi zina ATM. Kwa nini wasiweke ATM kule vijijini wale wafanyakazi wasipate taabu ya kuhangaika kuja mjini? Riba za mabenki ni kubwa na kitabu cha Mipango kinakiri, lakini hakijaweka dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo chechefu ni asilimia saba tu, *less than 10%*. Kwa hiyo, hakuna sababu kwa mabenki kuweka riba kubwa. Ziteremshe na ningeomba benki kuwa, hapa ichukue wajibu wake. Mshahara kwa ajili ya Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani kazi zao ni kubwa. Mimi sioni kwa nini Serikali ishindwe kumlipa Diwani mshahara. Tunampa posho, tushindwe kumlipa Mwenyekiti wa Kijiji mshahara, wakati

Mtendaji wa Kijiji anapata mshahara! Kwa hiyo, yeye anakuwa *super* kuliko Mwenyekiti. Maana yake mtu mwenye fedha ndiyo anakuwa na nguvu. Kwa hiyo, hii tungeibadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kulipa madeni ya ndani, hapa nina wakulima kule Mbinga. Mbiku hawajalipwa Shilingi milioni 400, kuna walimu pia wanadai. Katika kipindi hiki ambacho tumesheherekea Jubilee ya miaka 50, nchi hii haitakiwi kuwa inadaiwa na Watanzania wenzake. Walipeni watu hawa waache kunung'unika tupate baraka za Mwenyezi Mungu, tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote, ningependekeza zile fedha za mradi wa dharura kwenye umeme tungeziondoa, tungezipeleka katika mradi ule wa Ngaka tuweze kusaidia. Hatuwezi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependekeza kurekebisha *structure* ya ubia ule, badala ya kuwa na asilimia 70 wale *inter energy* na 30 *NDC*...

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ya mwisho? Tungerekebisha, mimi sioni kwa nini...

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Shekifu, na Mheshimiwa Mansoor, Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Kadenge na Mheshimiwa Naomi Kaihula wajiandae. Mheshimiwa Shekifu hayupo.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kandege nipo.

**MWENYEKITI:** Upo? *Okay.*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi ili niweze kusema yale ambayo wananchi wa Jimbo la Kalambo Kata 17 na Vijiji 126 walinituma kuja kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, naanza kwa kuunga mkono hoja na kwa matarajio makubwa kwamba Serikali itakwenda kufanya marekebisho haya ambayo walinituma nije niseme ili Serikali ipate kuyarekebisha. Ukitizama katika kitabu cha mpango, nimefarijika sana kwamba tumechukua hatua kuhakikisha kwamba tunakua na umeme wa uhakika na hasa kwa kuanzia Nyakanazi kwenda Kigoma, Mpanda, Sumbawanga, Tunduma, Makete na kuishia Iringa. Tumekuwa tukisema Waheshimiwa Wabunge kwamba, bila kuwa na chanzo cha uhakika cha umeme, nchi hii haiwezi kuendelea na bahati nzuri kwenye mpango limeingizwa hili na sasa hivi linakwenda kuanza kutekelezwa. Nadhani inabidi tujifariji na tuhakikishe kwamba tunasukuma hili ili liweze kufanyika, lakini pia ni vizuri tukabaini vyanzo vya uhakika vya umeme. Kwa Mkoa wa Rukwa, tuna chanzo kizuri sana cha makaa ya mawe ambacho Professor Waziri wa Nishati amesema katika vyanzo vya uhakika vya kutoa umeme wenyewe gharama nafuu, ni pamoja na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Rukwa tuna chanzo kizuri pale, ukienda Namwele na Nkomolo na ukionyesha pale kuna *prospect* ya kupata kiasi kingi sana cha makaa ya mawe na bahati nzuri kuna Mtanzania mzalendo ambaye tayari alishaanza kuchimba. Anachotaka ni kupata uhakika na *support* kutoka Serikalini. Kwanza, uhakika ni kwamba umeme utakaozalishwa utanunuliwa na Serikali na kuingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Nini maana yake? Ukishakuwa na umeme wa

uhakika, wawekezaji watakuwa wengi kwa Mikoa ya Rukwa, Katavi pamoja na Kigoma kwa ndugu zetu ambao wanasesma hawataki bajeti hii. Lakini naamini wanahitaji umeme. Ni vizuri wengine tukawasaidia kuwasemea kwa sababu wengine tumejaliwa kuwa wakweli. (*Makof*)

Tukiwa na umeme wa uhakika, ni imani yangu kubwa kwamba hata lile Soko la Kimataifa la samaki lililopo Kasanga ambalo bahati nzuri hata Mheshimiwa Makamu wa Rais alitutembelea pale, akafarijika na soko lile, lakini bila umeme hatuwezi kufika popote. Naamini tukiwa na umeme wa kutosha, wawekezaji wengi watafika kwa ajili ya kujenga viwanda, Mikoa ya Rukwa, Katavi pamoja na kwa hawa ndugu zangu Kigoma. Kwa hiyo, naamini Serikali iamue kwamba lini itatoa *support* kwa mwekezaji wa ndani mzalendo ambaye ameshaanza kuchimba makaa na wamhakikishie kwamba umeme unanunuliwa ili kazi hiyo nzuri iliyoanzishwa na mzalendo isije ikaingia nuksi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine nisemee kuhusiana na suala la barabara. Nina kila sababu ya kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuanza kuamua kwa nia ya dhati kufungua mawasiliano ya barabara kwa Mkoa wa Rukwa, Katavi na baadaye kwa ndugu zetu wa Kigoma. Itakuwa ni kweli ile kauli ya kwamba *sleeping giant* wameamua kusimama. Sasa naamini ile dhana kwamba wenzetu walitaka kuigawana nchi ya kaskazini kwa vile wao vipaumbele vilifika mapema haitakuwa na maana tena kwa sababu watajua na sisi tuko *potential*. Ni kwamba, tulifanya kucheleweshwa, tumeamka na sisi tulitaka tusikilizwe.

Kwa hiyo, bajeti hii niungane na mwenzangu mmoja aliyetangulia kusema sisi tunaoitwa Mikoa ya Pembezoni, hatupendezwi na lugha hiyo, tunataka na sisi tupewe upendeleo ili tuweze kuendelea na kazi kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na suala la kilimo. Kwetu sisi ni wakulima hodari, wala hatumsubiri mtu kutuambia twende tukalime. Unapofika msimu wa kilimo hatusubiri kusukumwa, tunachotaka ni kuwezeshwa, tumekuwa tukizalisha mahindi kwa kiasi kingi sana, lakini ukiuliza tunazalisha kwa njia zipi? Ni kwa kutumia wanyama kazi ambaao nao ikifikia kipindi wanachoka. Tunataka Serikali ielekeze nguvu kuhakikisha kwamba wakulima na hasa vikundi nya *SACCOS* na vikundi vingine wanawezeshwa kwa kukopeshwa matrekta na sisi tuna tabia ya kulipa hata kwenye bajeti ya mwaka jana nilisema, sisi tukikopa cha mtu, tunarejesha. Tunaomba Serikali ihakkishe kwamba katika pesa hii ambayo wametenga kwa ajili ya benki ya wakulima, kuwe na namna ya sisi kuweza ku-access mikopo hiyo kwa urahisi. Ninavyofahamu mimi, ukitaka kutoka Rukwa au Katavi kupata mkopo unaambiwa mpaka uende Mbeya. Tunataka urahisi wa wananchi kuweza kupata mikopo ili tuinue Kilimo Kwanza kiwe ni hasa chenye tija. Hatuwezi tukaendelea kwa kulima vilevile na ndio tukategemea kulilisha Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumekuwa na matatizo makubwa kuhusiana na suala la pembejeo, pembejeo zimekuwa zikifika kwa kuchelewa sana. Inakuwa kama vile takwimu sahihi kwamba mvua zinanyesha Rukwa na Katavi lini, hazijulikani. Naamini hii ni namna tu ya watu ambaao wangetaka Serikali ya Chama cha Mapinduzi Ionekane kwamba haifanyi kazi ili waje wapate maneno rahisi ya kuiondoa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, inajua mvua zinaanza kunyesha lini, pembejeo ziwahi ili wananchi waweze kununua na pia bei ya pembejeo ipunguzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimekuwa pia nikipata tabu pale tunapoambiwa kwamba, tumeondoa kodi kwenye matrekta, lakini pale unapoenda kununua tela unaambiwa eti hii unailipia kodi, haieleweki kabisa. Au unaenda kununua tairi, unaambiwa sasa tairi hili unalilipia kodi, lakini ukinunua trekta kwa ujumla wake, hamna kodi, hii itakuwa kama tunaigiza.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hakikisha kwamba kodi zinatolewa kwa zana za kilimo ili Kilimo Kwanza isiwe ni maneno iwe ni halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda niongelee kidogo kuhusiana na uvuvi. Uvuvi mara nyingi sana tumekuwa tukisahau na hasa uvuvi kwa Ziwa Tanganyika, ambalo liko mpaka Kigoma kule. Nikipitia kwenye mpango, inaelezwa vizuri sana, lakini inapokuja kwenye *implementation* silioni hili kwamba, wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanasaidiwaje? Wavuvi wa Ziwa Rukwa wanasaidiwaje? Naomba itafsiriwe, hii habari ya kwamba unaondoa kodi kwenye nyuzi, sio namna sahihi ya kuweza kumsaidia mvuvi; mvuvi anataka apate vifaa vya kisasa ili avue kisasa. Kuna samaki wengi sana ziwa Tanganyika, ambao tumeshindwa kuvua kwa sababu ya uwezo wetu mdogo wa zana duni. Naomba tafsiri hii iwe kivitendo ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo kuhusiana na huduma za jamii. Kwa sisi wa Mikoa ya Rukwa na Katavi pamoja na Kigoma, tumekuwa tukipata tabu sana katika suala la elimu. Walimu wakipangwa kwenda kufanya kazi kule, hawataki kukaa huko kwa sababu miundombinu ni hafifu. Ifike wakati Serikali ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba na wale wananchi wanafaidika na huduma zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika afya, katika sehemu ambazo tuna tabu ya afya kwa maana ya Zahanati zetu kukosa dawa na kukosa watumishi ni Mikoa hiyo hiyo ambayo ikitwa majina ya kejeli Mikoa ya Pembezoni. Ifike mahali Serikali iamu kwa makusudi kwamba, kule ambako kulikuwa kunaonekana kwamba ni pembezoni si pembezoni tena kwa sababu fursa zimefunguliwa na itakuwa ni rahisi na wananchi nao kufaidika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongee kidogo kuhusiana na suala la *TEHAMA*. Ni ukweli kwamba kwa dunia ya leo ya sayansi na teknolojia, tunataka *accessibility* ya *data* ifike kila mahali na kila Wilaya. Itoshe sasa kwamba na sisi wa Wilaya za Kalambo, Wilaya za Mlele na kule Kigoma kwa ndugu zetu, tuweze ku-access *data* hata tukiwa katika hizi Wilaya mpya na hasa tukiwa na uhakika baada ya kufikishiwa umeme, ili tuweze kutuma maombi kwa kutumia mitandao tukiwa vijijini na tunarudi tunaenda kufanya kazi za kilimo. Itapendeza sana nchi hii kama Taifa, tunaendelea kwa pamoja, tusije tukaachana, tulishaachana inatosha. Haifai tena wengine tukaendelea kuachwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, napenda kumpongeza jirani yangu Mbunge wa Ilala, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti. Naamini atatumia Kiti chake vizuri, kama alivyo mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ningependa kuchangia bajeti hii, kwanza tuelezane kwamba, ninaomba tu ndugu zangu tukiwa humu Bungeni, watu wetu, wananchi tunaowawakilisha kwa pamoja tuwe ni CHADEMA, tuwe ni CCM, tuwe ni NCCR, wanatuona kwamba ni watu wenye hekima; yaani wanatuona kwamba tumeinuliwa kuwasaidia kuwaongoza. Kwa hiyo, isingekuwa vizuri kuanza hapa kulumbana na kuwandanganya watu. Tuko hapa kusudi tuweze kupata ufumbuzi wa mambo mengi ambayo yanatukabili na hapa ni njia nzuri mojawapo ya kuweza kuwaonesha wananchi ni wapi tunashindwa ili tukirudi kule na wenyewe wakatusaidie kwa sababu siku hizi uongozi pia ni shirikishi, kule kuna viongozi. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mimi ninaomba niwakumbushe wenzetu wa CCM, sisi CCM ni lazima tuitaje na ninyi CHADEMA ni lazima muitaje; msikasirike kwa sababu sisi wajibu wetu tena Kikatiba kabiso, sisi ni *opposition* sio kwamba kupinga tu kila kitu lakini kazi yetu kubwa ambayo imetuleta hapa ni kuwasukuma ninyi, yaani ku-oversee kuona kwamba mnatekeleza yale mambo kama inavyopaswa. Sisi ni kama ma-*watchdog*, yaani ni macho na midomo ya wananchi humu ndani. Sasa mnachopaswa kufanya ni nyie kujibu tu kwa hoja wananchi wasikie na waone kwa sababu, kwa bahati nzuri kwa teknolojia hii mnaposema, tunaposema, wanatusikia wote na wale kule wanapima. Kwa hiyo, hakuna tatizo la kuanza kuzozana hapa, kuoneshana vidole, naomba sana tuelewe hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwasomea nukuu moja ya Baba wetu wa Taifa ambaye tunamheshimu sana, imetoka katika nukuu ya wiki ya Rai, ambayo inaeleza ni kwa nini Vyama vya Upinzani vilianzishwa. Naomba niwasomee, nukuu ya wiki ya Rai ya Alhamisi, Juni 14, 2012 inasema hivi:-

*"Ubovu wa uongozi ndani ya CCM ndio uliofanya nikapendekeza tuanzishe mfumo wa vyama vingi. Nilitumaini kuwa tunaweza kupata chama kingine kizuri ambacho kingeweza kuongoza nchi yetu badala ya CCM au ambacho kingekilazimisha CCM kusafisha uongozi wake kwa kuhofia kuwa, bila kufanya hivyo kitashindwa katika uchaguzi ujao."* Jamani eeh, hivi ndivyo ilivyo; nirudie tena? (*Makofi/Kicheko*)

**WABUNGE FULANI:** Ndio! Rudia tena. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inazungumzia kazi ya Upinzani na kwa nini vyama hivi vilianzishwa ni kwamba, Mwalimu huyu tunayemheshimu sana, tunayempenda sana, anasema hivi:-

*"Ubovu wa uongozi ndani ya CCM ndio ulifanya nipayendekeze tuanzishe mfumo wa vyama vingi."*

**WABUNGE FULANI:** Rudia tena. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea kusema:-

*"Nilitumaini kuwa tunaweza kupata chama kingine kizuri ambacho kingeweza kuingoza nchi yetu badala ya CCM au ambacho kingekilazimisha CCM kusafisha uongozi wake kwa kuhofia kuwa, bila kufanya hivyo, kitashindwa katika uchaguzi ujao."* Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri tumeelewa kwa nini sisi tunafanya kama tunavyofanya, msituchukie. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nichangie. Mimi napenda kuchangia hivi, mimi sio mnafiki. Huwa napenda kusema mambo ya ukweli na ambayo kwa kweli mtu yeyote alipo anayapima.

## TAARIFA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Kaihula, kuna Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa bado hatujaelewa vizuri yale maneno, angeyarudia tena ili tuyaelewe vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naomi, endelea!

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ambaye hakusikia aje, mimi nitamwelekeza na nitamgawia pia hili gazeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda niseme hivi, mimi hii bajeti siwezi kuikubali, siwezi kuiunga mkono kwa sababu, tumekuja tuiureka bishe. Ikienda kurekebishiwa ndio tutanza kufikiria tena jinsi gani tuiunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza kabisa ambacho napenda waende wakarekebishe kwa sababu sisi wote kwa pamoja katika bajeti iliyopita tulizindua mpango wa uchumi; katika huo tulikubaliana, ilikuwa kama ni ahadi kwamba, jamani tumezidi kuwa tegemezi, mpaka lini tunaendelea kuwa tegemezi, ombaomba? Tukakubaliana wote kwamba tuwe tunatenga kiasi cha 35%, sasa hiki kitu hakijaanza, hakijaoneshwa huku kwenye bajeti hii, badala yake kiko chini yake. Hili jambo kwa kweli limekiuka mapatano na makubaliano ya sisi sote Wabunge. Kwa hiyo, sisi hili litatufanya tukatae ndugu zetu, Serikali ya CCM, tunaomba mrudi hili mkalipange upya, kusudi tuweze kuja kuwaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili. Pia sisi sote hata huko kwenye Kamati, nafikiri mnajua kwamba kwenye Kamati, mfumo wa Kamati hautofautiani sana na mfumo wa hapa Bungeni; kwenye Kamati pia tunazidiwa na watu wa CCM na humu ndani tunazidiwa na watu wa CCM, ndio maana sisi tunataka tuwaambie hapa kusudi wananchi wajue kwamba, ingawa tunapitisha sio wote ambao tunapitisha hicho kitu, tumezidiwa jamani, tunaomba msamaha. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili suala jamani tunakubaliana sisi wote, tunaumia sisi wote, tukiwa nje tunazungumza sisi wote, jamani, kwa nini tunaendelea kutoa misamaha ya kodi? Sisi wote, mimi nashangaa, tunabadilikaje jamani? Tunapatwa na kitu gani mpaka tunaanza

kubadilikababadilika? Tumekubaliana sisi wote kwamba misamaha ya kodi tuseme hapana na ambaye atasema hapana ni kwa kupitia Serikali yetu, sasa sisi tukiwaambia, mnachukia. Sisi tunasema hivi na tunawaomba, misamaha ya kodi kama tulivyoelezwa kwa kirefu kwamba kwa kweli tumesema hapana tusiendelee kuwasamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuendelee kuwasamehe? Mimi nashangaa, eti kwa mfano wanasma tunaleta vivutio, unavutia nini? Mimi nakwambia nchi yetu yenewe ni kivutio. Kweli, yaani Tanzania yenewe ni kivutio na sasa hivi kwa mfano gesi yenewe kusema gesi ipo, ni kivutio. Kwa hiyo, watu wanajileta hapo, wanapambana huko nchi sijui Asia, Marekani, Uingereza, wanakuja hapa tena wanataka kututawala kiuchumi; mnasema mnawapa vivutio, unawapa vivutio vya nini? Hapanal! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunapendekeza hivi, wakija hapa twende kwenye mikataba inayoelewaka. Sisi tunawekeza ardhi yetu, tunawekeza mali yetu itakayopatikana hapa, wenyewe wanaleta utaalamu na vifaa kwa hiyo, tunapoanza tuanze *at equal*, halafu tukipata vile vitu tuongeze thamani. Haiwezekani! Sisi tumekwenda kutembea kule Nkakaa, eti sisi tunapata 30 halafu mwekezaji anapata 70; jamani, mimi nilitamani kulia, *actually* nililia nikakaa chini. Hiki kitu kitu gani, tunawapa vivutio gani? Halafu hukohuko tunazungumza jamani eeh, tunavipaumbele, tuweke vipaumbele. Kipaumbele chetu cha kwanza kikubwa kimojawapo ni kwa ajili ya kuweka umeme. Umeme tunajua kabisa hata kwa mtu mwenye akili kidogo ukimueleza anaelewa kwamba, umeme *uta-stimulate* vile vianzio vya uchimbaji wa makaa ya mawe, chuma, viwanda vilivyopo hivyo tunavyosema nguo sijui, pamba, vyote vinategemea umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha ajabu, sisi tumekuwa na ajizi kubwa sana hapa Tanzania, utafikiri yaani hatuna akili

kichwani, sijui taahira. Kuna kitu kinatuloga, tuombe, tunaomba watuombee, watuombee, kwa nini tunapata udhaifu sana wa kuweza kutengemaza hili suala la umeme ambapo kwa mfano sisi tulizungumza katika llani yetu, ndio Kamati ya Viwanda na Biashara, kuna wataalamu wetu kwenye *NDC*, wataalamu wale wanatuambia kwamba, tukipewa kiasi hiki, milioni hizi, tutaweza kuleta umeme, lakini sisi tumeshindwa, tuna tatizo gani? *TANESCO* yenyewe tumekaa tunaipandikizia tu mambo, jamani hiki ni kitu gani? Madeni ya *TANESCO* yasiyolipika ambayo sio ya kwake, mara sijui nini, jamani tunamwomba Mungu na tunaomba wananchi msamaha kwamba, watuombee. Ni lazima tupate ufumbuzi wa kipaumbele cha umeme, umeme upatikane kule Nkakaa, umeme upatikane kila mahali vijijini, upatikane umeme wa kweli. Uwe wa maji, uwe wa upepo, uwe wa nini, unawezekana, ila sisi ndio ambao tumefungwa; kuna kitu kimetufunga jamani, tukubali. Tukubali kuna kitu kimetufunga, tukubaliane kwa pamoja tuombe kitatuliwe. Inaweza ikawa ni pepo, mimi ni muumini, pepo; pepo la kutoelewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru, naomba niendelee. Pia jambo lingine nililotaka kulizungumzia ni suala la *succession*, yaani kuweka hawa wataalamu. Kila siku tunasema tu, tutasomesha wataalamu wetu, sasa sikilizeni, tutasomesha lini? Angalau Baba wa Taifa alianza akafanya; mnakumbuka kwamba, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, hakutaka madini yachimbwe wala kufanya kitu chochote mpaka tutakapokuwa na wataalamu wetu wenyewe, si ndio jamani? Tukasomeshwa tulio wengi kwa bei ya wafadhili kusudi tuweze kuja hapa, lakini kinachoendelea sasa hivi mimi sikielewi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuja marubani wanalia, eti wamewawekea mtu wa nje ndio ana-supervise kufundisha marubani. Marubani wetu wa ndani hawawapi nafasi ya kupata *milage* kusudi waweze ku-*qualify*. Sasa hapo unapata *succession* namna gani? Utaendelea kutawaliwa. Hili jambo

naomba Miundombinu, Uchukuzi, mlifanyie kazi, wataalamu wetu marubani, vijana wetu wako wanakata tamaa mpaka wanatamani kunywa sumu kwa sababu, hawasikilizwi. Naomba muende mkalifanyie kazi wapate nafasi ya kujifunza, wapate uzoefu waweze kuendesha ndege tunazotaka kuzinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba niseme hivi, ile bajeti ya mwaka jana ilishindwa kabisa, ilishindwa kabisa. Sasa tulipaswa kujifunza kwenye ile bajeti, hata kama ni chungu, tujifunze; chakula kinaweza kikawa biashara na kinaweza kikawa chakula, kwa nini tuliwa mashamba ya *NAFCO*, watu walikuwa wanazalisha chakula cha kutosha, tukayatupa huko. Badala yake mnataka kuwataifishia watu kuleta mambo ya Zimbabwe hapa na mambo ya *South Africa*, kama vile hatujui historia. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu, tujifunze. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nakupongeza wewe kuwa Mwenyekiti na kuanza kazi leo. Kama wenzangu walivyosema, tunategemea utamchukua farasi huyu kwa kasi inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze awali ya yote kwa kusema kwamba, mimi ninaungana na Kamati ya Fedha na Uchumi, ninaungana na Kambi ya Upinzani kwamba, tunachozungumza hapa sio kwamba, bajeti hii haina maana, hapana. Tunasema bajeti itazamwe, iangaliwe upya kwa sababu kuna maeneo yanatakiwa kurekeblishwa, hasa maeneo ya mipango ya maendeleo kwa kutizama mpango ulioletwa hapa na Serikali. Sasa hiyo mimi sielewi ni kwa nini watu wapate jazba kwa kurekebisha kitu ili kiweze kutufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya Upinzani kilicho jonesha ni kwamba, ilipunguzwa hela ya matumizi ya kawa ida ikaongezwa hela ya maendeleo. Mimi sioni ni kwa nini watu watoe mpaka mishipa, watoleane mishipa mikubwa, kwamba hii ni takataka itupwe, hayo ni mambo ya kawa ida kurekebisha, ni *adjustment*, kwa neno la kingereza. Waheshimiwa Wabunge, kujadili bajeti ni matakwa ya Katiba kwa hiyo, msilete mchezo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika mimi ninamhurumia Waziri wa Fedha na wasaidizi wake kwa sababu, Wabunge wengi hawajatumia kinachostahili, wengi wamezungumzia mambo ya Majimbo yao, hapa inatakiwa tujadili bajeti ili baadaye tujadili Wizara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaanza na la kwanza ambalo ni msumari unaouma kwamba, matumizi ya *recurrent* ni makubwa kwa sababu Serikali yetu ni kubwa sana kwa hiyo, kuiendesha inataka gharama kubwa. Sasa hiyo ndio imemeza sehemu ya maendeleo ambayo hii Waziri wa Fedha, hataiweza kwa sababu, bwana mkubwa aliyeiunda Serikali yeye haulizwi, Katiba inasema asiulizwe, kwa hiyo halitatusaidia lakini katika hii bajeti tuliyonayo ya shilingi triliuni kumi na tano, inawezekana tukafanya *adjustment* hapa kwamba bajeti ikawa *withdrawn* na Waziri wa Fedha akakaa na wataalam wake na sisi tumetoa mapendekezo siyo dawa ya asprini umeze hapa ni mapendekezo kama haifai basi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati wa bajeti mimi nilizungumzia vianzio vingine ambavyo Serikali haikuchukulia maanani, sasa ndio tatizo limekuja. Mimi mwaka jana nilizungumzia kwamba wigo wa kodi ni mfinyu sana, tukazungumzia *VAT*, wigo wa *VAT* (*Value Added Tax*) ukaongezwa na watu wengi wakachukulia hiyo itakuwa ishara kubwa ya kupata watu wa *income tax* kwa sababu walitajwa *income tax* wanakwepa kwa sababu hatuna kumbukumbu lakini kama kuna *VAT return* kutakuwa na taarifa ya awali

kwamba ni nani anayetakiwa alipe kodi. Sasa Serikali badala ya kufuatilia hilo kuweka hiyo VAT ambayo mimi nilipendekeza na kuzungumzia juu ya *real estate*, ambayo ni pesa nyingi sana, Serikali imeacha, imekimbilia vijana wa bodaboda ambao wanaendesha pikipiki kwa malapa hawana kitu chochote. Pikipiki siyo kitu ya kutegemea, simu hii ya mawasiliano ambayo katika vijiji na sehemu yote ndiyo mawasiliano ya watu wa chini Serikali inaona hapa iongeze asilimia 12 ya ushuru wa forodha hiyo sehemu siyo. Sasa ina maana wakiacha kupiga simu ndiyo sawa na yule mzungumzaji leo asubuhi aliyesema kwamba pombe watu wakiokoka itakuwaje na wengine leo wametangaza hawanywi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri *compliance*, kama Sheria ya Kodi, *compliance* ikisimamiwa vizuri, nchi hii ina kodi nyingi sana, nyingine imeshatamkwa leo, biashara ya madini *leakage* ni kubwa, sisi pesa tunazo nyingi tu, hatungekuwa tunakopa. Sasa tumeambiwa leo hapa deni la Serikali limekwenda *over 20 trillioni* na ni katika muda mfupi. Tuna wasiwasi hela hiyo imefanya kazi gani kama imefanya maendeleo, watu wamekopa kutengeneza barabara ni sahihi lakini kama wamekopa wakalipa mishahara *then* nchi imewekwa rehani, hiyo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona kwamba tunaweza tukaongeza pesa na tukarekebisha bajeti yetu, tutakuwa tumeokoa ule mpango wa miaka mitano kwa sababu inaelekea mpango wa miaka mitano katika mwaka wa kwanza tumeanza vibaya na huu mpango wa miaka mitano ni matakwa ya Katiba, kwa hiyo ikiwa kama bajeti yetu ya mara ya kwanza haijafuata mpango kama ulivyopangwa tumevunja Katiba. Jana alivyokuwa anawasilisha bajeti mbadala Msemaji wa upande wa Upinzani ni vile muda ulimbana pale mwisho angewasilisha vizuri, Kikatiba ilitakiwa ile bajeti ya Serikali isizungumzwe na tukapigia kura, ni sahihi

kisheria lakini kwa sababu muda ulimbana hiyo hoja haikutoka baadaye ikafuata hoja ya watu kuwa na jazba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue muda huu kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge *this is a noble House*, tuzungumze vitu vya heshima, kila mtu ana nyongo, sasa ukimwaga nyongo hapa, kila mtu akamwaga yake, hatutaweza kufika. Mimi nilitegemea Waheshimiwa Wabunge wanavaa suti vizuri lugha yao ingekuwa nzuri kama wao na mawazo yao ni mazuri sasa inakuwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu nje wanatutegemea, wanafunzi wa vyuo vikuu wanataka kuona mfano Mbunge anazungumzaje, wanafunzi wa shule za msingi na wengine wazee kama mimi na wajukuu zetu wanataka kuona tunazungumzaje. Kama ni kupigana ngumi tufanye mazoezi wengine mbona tutatoka mapema hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niende kama muda unaruhusu kwenye eneo la usimamizi. Pamoja na bajeti finyu, usimamizi wa pesa za Serikali ni wa hali ya chini kabisa hasa katika Halmashauri zetu, watu hawasimamii pesa, wamekuwa, sijui lugha sahihi, lakini wamekuwa wafujaji au wezi na hawachukuliwi hatua. Wananchi wanalia, Maafisa Watendaji wa Kata wenyewe ndiyo ma-*Professor* kabisa wa kula hizi pesa. Imetungwa sasa Sheria ya Kazi, ni mlolongo, mtu anakaa miaka mitano analipwa *full salary*, hafungwi jela, hafukuzwi kazi, Halmashauri zinapelekwa Mahakamani sijui tufungue tena Chuo Kikuu cha kutetea Halmashauri maana wao wameiba pesa na wameweka na Mawakili. Sasa sijui Halmashauri nayo itatetewa na nani? (*Makofi*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea ni kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize juu ya vijana hawa wa bodaboda. Vijana hawa wa bodaboda Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameleta *exemption tax*, anataka kuwameza, amewaondoa kwenye ile *band* ya chini na kuwavuta *band* ya juu ya 95. Mimi napendekeza kwanza hii *Presumptive Tax* iondolewe kabisa kwa sababu hapa ndiyo eneo la rushwa kwa sababu mtu ambaye hana kodi anaambiwa kodi yake ni shilingi 95,000, anaanza na laki sita ili waanze kujadiliana mpaka ifike shilingi laki mbili. Sasa hawa kwa sababu hawana kumbukumbu waondolewe. Sisi Wabunge kila siku tuko *TRA* kuwatetea hawa, sasa dawa yao tuwaondoe, tushike wale samaki wakubwa ambao ndio viwanda vikubwa, ndiyo hao *real estate owners* ambao wanapanga kodi ya nyumba wenye. Sasa namna ya *TRA* kuwashika hawa, kila mmoja mwenye nyumba afungue faili na pia labda tuwaite watu labda *house rangers* watakaokuwa kila mtaa au Mwenyekiti wa Mtaa aandikishe nyumba zote za kupangisha na mtu kama hajapata *clearance* ya *TRA* asipangishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda wangu haujaisha, naomba niwapongeze *TRA* kweli sasa hivi wanawaheshimu walipa kodi, tunazungumza nao vizuri, kama wakiendelea, eneo hili tutapona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninasisitiza bajeti kutizamwa upya, si katika jazba bali katika *noble mind*, mimi namheshimu Waziri wa Fedha, ni msomi na wale wengine wawili, juzi nimewasikia Waheshimiwa Manaibu Waziri ni wasomi, kwa hiyo, kutazama bajeti upya siyo kitu kibaya. Itazamwe upya warudi hapa waseme haiwezekani ni ileile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kwenye karne nyingine sasa ya Teknohama sasa kama mambo haya madogo yatatushinda je, hayo makubwa ya Teknohama tutaweza wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ahsante nashukuru. (*Makofii*)

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwako tena bila kupingwa na kuweza kupata nafasi ya kutuongoza jioni hii ya leo, nasema hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niungane pia na wenzangu kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili pamoja na wasaidizi wao wote ambao wametuandalia bajeti nzuri ambayo inatupa nafasi ya sisi Waheshimiwa Wabunge kuichambua na kuweza kuchangia mawazo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mawazo yangu, naomba na mimi nirejee kwanza kwenye wasemaji walitangulia mbele yangu na hasa yule dada Mheshimiwa mwenzangu ambaye ametoa nakuu ya Mwalimu ikitukumbusha ni kwa nini vyama vingi vilikuja na mimi naomba nichukue nafasi hii kutoa nukuu ambayo alitoa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Hayati Baba wa Taifa kwenye mkutano wa CCM mwaka 1995 ilisema hivi:-

*"Rais anaweza akatoka katika chama chochote lakini Rais bora atatoka ndani ya Chama cha Mapinduzi".* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 kwenye mkutano mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Hayati Baba wa Taifa alisema Rais anaweza akatoka kwenye Chama chochote lakini Rais bora atatoka ndani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba wale wote walioanza kuonyesha nia ya kuwania nafasi ya Urais mwaka 2015, wajilize je, watagombea kuitia chama gani? (*Makof*)

**WABUNGE FULANI:** Sawasawa!

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nianze kutoa salamu kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Masasi. Nataka niwahakikishie kwamba hawakufanya makosa kunichagua mimi Mariam Kasembe na hiyo ilikuwa ni ridhaa yao wao wenyewe na mimi ninawahakikishia kwamba nitawasemea, nitawatetea matatizo yao yote bila wasiwasi wa aina yoyote. Ninaomba wasisikilize maneno ya wapita njia, kuna usemi unaosema, kitanda kinachouma kunguni anayekijua ni yule anayekilalia. Sasa mtu pekee ambaye anaweza akajua matatizo ya Wanamasasi ni mimi Mariam Kasembe ambaye mlinipa ridhaa yenu ninyi wenyewe na si mtu mwingine yeyote. Nimezaliwa Masasi, najua matatizo mengine ya watu wa Masasi na nimeshaanza kuyasimamia na baadhi ya mambo yameanza kuonekana katika Jimbo la Masasi. Naomba wasitetereke na nitaendelea kuwasimamia, ahsante. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisikiliza kwa makini mijadala inayoendelea ndani ya Bunge letu, nawapa pole sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti kwa sababu mna kazi kubwa sana ya kuendesha vikao hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa natafakari, nimegundua jambo moja, nchi yetu inatawaliwa na utawala bora lakini inawezekana kabisa hii dhana ya utawala bora tumekuwa tukilisema mdomoni tu bado haijalngia miyoni mwetu. Kama dhana ya utawala bora ingekuwa imeingia miyoni mwetu, ninaamini hizi kauli tunazozitoa ndani ya Bunge kwa kweli tusingeweza kuzisema. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoiomba Serikali, iangalie sehemu yoyote watakayopata fedha warejee tena kutufanyia semina ili tuelewe majukumu yetu, tuelewe wajibu wetu, tujue mipaka yetu ya kazi kwa sababu sasa hivi nimeshaona hata Waheshimiwa Wabunge hatujui mipaka yetu ya kazi, tunaacha kusimamia Majimbo yetu, watu tunaenda kusemea Majimbo ya wengine. (*Makof*)

## **WABUNGE FULANI:** Sawaaa!

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haikufanya makosa kuanda utaratibu wa kuweka Majimbo na kama kuna Mbunge yeyote ambaye anataka kuwa Mbunge wa nchi nzima, maoni ya Katiba yapo, pelekeni kwenye maoni ya Katiba mchaguliwe muwe Wabunge wa nchi nzima muweze kuyasemea Majimbo yote Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nichukue nafasi hii kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo wameanza kutekeleza yale yaliyomo ndani ya llani ya Chama chetu kwenye Mkoa wetu wa Mtwara na hasa kwenye Jimbo langu la Masasi, si vibaya nikasema machache ili wale wasiofahamu waanze kufahamu. Ndani ya llani ya Chama cha Mapinduzi, tuliahidiwa watu wa Masasi suala la maji, tuliahidiwa watu wa Masasi kujengewa daraja la mto Nangoo ambalo kwa miaka mingi watu wamepoteza maisha lakini kwa hivi sasa navyozungumza kwenye lile daraja mkandarasi yuko kazini, anafanya kazi usiku na mchana. Mradi wa Majimbwiji, mkandarasi yuko kazini anafanya kazi usiku na mchana na Serikali tayari inafanya jitihada ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuchimba mabwawa kwenye mji wetu wa Masasi kuondoa shida ya maji. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kukipongeza Chama cha Mapinduzi na Serikali yake kwa kutekeleza llani yake. Nachoomba kwa yale ambayo yako ndani ya llani ya Chama cha Mapinduzi, ambayo bado hayajaanza kutekelezwa, msichoke, Serikali yetu iweze kutekeleza kwa sababu tuliahidi kuyatekeleza ndani ya miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwanza suala la uwanja wa ndege wa Mtwara. Uwanja wa Mtwara sasa hivi unakaribia kuwa uwanja wa kimataifa kwa sababu wenzetu wawekezaji kutoka nchi mbalimbali wamekuwa

wakitua katika uwanja wa Mtwara. Nachoiomba Serikali ikamilishe chumba kile cha kuingilia abiria, pale tunapotokea kwa sababu huu ni karibu mwaka wa tano tumeanza kufanya ukarabati lakini ukarabati huu hauishi. Naomba mfanye haraka sana kwa sababu itakuwa ni aibu wawekezaji wanakuja lakini wanafikia kwenye mabanda, naiomba sana Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo naliomba ni suala la umeme Masasi. Mtwara tumepata gesi, gesi ambayo watu wa Mtwara na Lindi tulitarajia kwamba shida ya umeme itakuwa imeisha lakini hadi hivi ninavyozungumza sisi watu wa Masasi umeme umekuwa ukikatikakatika kila dakika na mara nyingine siku mbili, siku tatu hakuna umeme. Kilichopelekea hivyo ni kwamba bado hatujakamilisha miundombinu kwa kukarabati zile nguzo zilizokuwepo kutoka Mtwara kupitia Tandahimba, Newala na kutoka Mnazimoja kuja Masasi. Naomba zitafutwe fedha sehemu yoyote tuweze kukamilisha ukarabati huu kwa sababu itakuwa haina maana gesi iko Mtwara lakini sisi watu wa Mtwara tunalala katika giza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie vijana wetu wa bodaboda. Mimi nakotoka usafiri pekee sasa hivi tunaoutegemea ni bodaboda. Bodaboda zinabeba mpaka wagonjwa, bodaboda zinabeba mpaka akina mama wajawazito, naomba niungane na Wabunge wenzangu ambao wameomba tuwapunguzie hawa vijana wetu kodi ya bodaboda. Kwa sababu hawa vijana tukiwawezesha, kwa kweli tutapunguza kasi ile ya vijana wetu kuingia katika mambo yasiyokuwa na msingi lakini kwa sisi wa Mtwara, vijana wengi wamepunguza kukimbilia Dar es Salaam kwenda kufanya kazi ya umachinga kwa sababu wamejajiri wenyewe katika sekta hii ya bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naona tunaweza tukawasaidia vijana ni lile la viwanda vyatya ndani vyatya nguo viweze kusamehewa kodi ili kuleta maendeleo kwa

haraka. Kama tunavyoju, tukiwa na viwanda vy a kutosha humu ndani, vijana wetu watapata ajira za kutosha lakini hata sisi wenyewe tutakuwa tunajivunia kupata bidhaa zinazotoka humuhumu nchini. Ni aibu leo hii sisi akina mama wa Kitanzania hasa sisi Wabunge ukituangalia humu ndani kila mmoja amevaa kitenge cha kutoka nje, lakini kumbe kama tungeweza kuviwezesha hivi viwanda, tukaviboresha, tungeweza kutengeneza vitenge humuhumu nchini, khanga za kutosha humuhumu nchini, tukauziwa kwa bei ya chini kuliko bei ambayo tunanunua hivi sasa, naomba kodi hii londolewe. (*Makof*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Njwayo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nami niungane na Wabunge wenzangu kutoa mchango wangu kwenye bajeti iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikupongeze mtani wangu, tena unaharibu jina langu, mimi naitwa Njwayo siyo Njwao. Hongera kwa kukalia kit, umependeza mtani, tutakupa ushirikiano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini nimesoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ile hotuba ya Waziri wa Mahusiano na Uratibu na kwa hiyo nasema jambo moja, jambo lenyewe ni kwamba kawaida mwembe unaozaa sana ndiyo unakobolewa sana. Kwa hiyo, CCM ndiyo wanaongoza hapa lazima hawa jamaa wapige maneno, ni changamoto, tusonge mbele kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi bajeti kiasi fulani imeniridhisha lakini naushauri katika maeneo yafuatayo. Mimi wasiwasi wangu mkubwa ni jambo moja, jambo lenyewe ni kwamba watendaji walioko Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ni lazima wasimamiwe vizuri. Kule ndiko kwenye matatizo, tukiwabana, tukiwasimamia vizuri, mambo yatakwenda. Tuhakikishe tunawasimamia vizuri na kila senti tano yetu inajulikana ilivyotumika. Kwa kufanya hivyo, nadhani hakutakuwa na mambo makubwa na tutasonga mbele barabara! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nawaomba, ile dhana ya utawala bora ichukue nafasi yake vizuri, tuhakikishe Serikali inawadhibiti wapotoshaji, kama kuna wapotoshaji tusimame, tuseme na tuseme ukweli. Ninasema hivi kwa sababu kwangu tarehe 17/4, ofisi ya *OCD* Tandahimba ilichomwa moto. Jambo hilli baadhi ya watu wamelipotosha na kwamba hata Serikali wamelichukua kwa dhana ile ya upotoshaji wakati mambo si sahihi. Ni vizuri viongozi walio katika ngazi ya Uwaziri, Serikali wangekimbia kuwasikiliza wananchi wale, wakapima ukweli wananchi wanawaambia nini. Inatia shaka kuona ofisi ya *OCD* ambayo ina ulinzi wa masaa 24 mfululizo eti inachomwa moto, inakuwaje maduka yanayoungua yachaguliwe? Ndiyo maana nasema suala hapa ni kuwa na umakini tu na kufuata utawala bora. Tusimamie vizuri kila jambo ili maendeleo yaendelee kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika mchango wa leo ni kwamba zaidi ya 75% ya Watanzania wanafanya shughuli za kilimo. Mimi naomba kuungana na baadhi ya Wabunge kusema kwamba tuhakikishe kwenye mwaka huu wa fedha ushuru na kodi mbalimbali zisizo za lazima kwa wananchi wetu zinafutwa. Tunawabebesha mzigo mkubwa mno wakulima na unavunja ari ya utendaji wao kwenye shughuli zao za kila siku za kilimo. Kwa mfano, vyama vyangu vya msingi yaani nina maana wananchi kupitia vyama vyetu vya msingi katika Wilaya ya Tandahimba, hivi sasa ninavyoongea vimechangia 50% ya pembejeo lakini haohao wanatakiwa wachangie ujenzi wa shule ya sekondari na mambo mengine ya kijamii. Kwa hiyo, kwa kupunguza kodi au kuzifuta, watahamasika na watafanya vizuri na kilimo kitaongezeka mara dufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja, nimeangalia bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Maji, sijafurahishwa sana. Mimi kama Mbunge ni lazima nitoe ushauri kwa Serikali. Kwenye bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Maji, unaona kwenye *sector* ya *rural water supply*, zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 24.7 lakini fedha zinazotegemewa kupatikana za ndani ni shilingi bilioni 2.6 na za wafadhili ni shilingi bilioni 12.1. Kwa nini hizi shilingi bilioni 12.1 zisingekuwa zinatokana na vyanzo vyetu vya ndani? Mimi nilitarajia kwamba tumepata somo kwenye ule mradi wa maji wa vijiji kumi kila Wilaya unavyozubaazubaa, unakwenda polepole na usivyo-*perfom* vizuri kwa sababu ya kutegemea fedha za rafiki zetu au ndugu zetu au majirani zetu. Wakati umefika sasa tuamue kabisa kwenye yale maeneo ya msingi na muhimu sana kwa maendeleo ya watu wetu fedha zetu wenywewe ndiyo zifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la maji, upo mradi wa Makonde, unachelewa kwa mazingira hayahaya. Juzi nilipokuwa nachangia swali la Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, nilieleza suala la kukamilika kwa upembuzi yakinifu lakini leo

yule Mhandisi wa mradi kanitumia *email* anasema kwamba ni kweli tulikamilisha lakini kuna tatizo kwamba wale watu wanaofanya upembuzi yakinifu walisahau kuangalia kiwango cha maji kwenye ardhi na hilo linahitaji muda mrefu? *Why takes longer?* Waziri wa Maji, naomba usaidie jambo hili ili tuepukane na adha zisizo za lazima kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, llani ya uchaguzi ya CCM inataja suala la kuanza upembuzi yakinifu kwenye barabara inayotoka Mtwara kwenda Tandahimba, Newala hadi Masasi na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Rais pia walipokuwa kwenye kampeni waliwaahidi wananchi hasa Mheshimiwa Rais kwamba kabla hajatoka madarakani atahakikisha kuna mkandarasi yupo *site* akifanya kazi. Katika bajeti ya mwaka jana zilitengwa karibu shilingi milioni 375 lakini mradi ule wote unahitaji fedha ya ziada shilingi bilioni 1.2. Mimi natoa rai kwa Serikali kwamba hizo shilingi bilioni 1.2, nimeangalia kwenye kitabu hakuna zilipoonyeshwa wazi. Naomba mfanye kila inavyowezekana zipatikane na mimi natangulia kusema awali kwamba hatutaelewana na Waziri wa Miundombinu na Waziri wa Ujenzi kwenye jambo hili kama sitazona hizo fedha wakati wa bajeti yake. Nasema hivyo kwa sababu barabara ile ni ya uchumi na barabara ile ndiyo tegemezi kubwa katika maendeleo ya Mkoa wa Mtwara. Barabara hiyo ndiyo inayounganisha Wilaya zote za Mkoa wa Mtwara na kwa sababu iko kwenye ahadi, tusilegelege tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya kwanza imegonga na nisingependa inigongee kengele ya pili lakini ninachotaka kusema ni kwamba Mkoa wa Mtwara na Lindi ndiyo ilikuwa *base* ya ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Wakati tupo kwenye harakati hizi, tulismama kufanya shughuli za kimaendeleo na kwa hiyo wenzenzu walisonga mbele sana kwa sababu hawakuwa na jambo, wao ni kufanya mambo ya maendeleo na mambo mengine ya kawaida ya kijamii lakini sisi ndiyo ilikuwa ngome ya kuhakikisha jirani zetu walio kusini mwa Tanzania na kusini mwa Afrika wanajikomboa. Sasa

mambo yale yameisha, kwa hiyo sasa na sisi mtupe kipaumbele maana tumesimama muda mrefu, mtupe upendeleo maalum. Kwenye bajeti ya sasa na ya baadaye ni lazima tuhakikishe tunatoa upendeleo maalum kwa maeneo hayo maana hatukusogea sana kwa sababu hiyo na yale maeneo mengine ambayo sasa yanaitwa Wilaya au Mikoa iliyopo pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiko Chama cha Walimu, Chama cha Walimu kinawachangisha Walimu wake michango kadhaa kwa ajili ya mambo mbalimbali kwenye chama chao. Nimekutana na Walimu wengi wakilalamika kwamba hakuna mpango ulio mahsus wa kufanya *auditing* ya zile fedha na hizo fedha ni nyingi kwelikweli. Naomba Serikali isaidie ama kwa kuwatumia *COASCO* ama taasisi yoyote iwe inakagua zile fedha ili kusaidia maendeleo ya Walimu na siyo kuwaacha kama walivyo. Wapo wajanjawajanja wachache inaonekana wanazitumia fedha hizo pasipo makusudi yaliyolengwa kwenye sekta hii ya Chama cha Walimu.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kengele imenigongea, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Njwayo na sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Kebwe, hayupo? Namwita Mheshimiwa Rev. Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa nukuu ambayo naipenda sana inayosema:-

*"Insanity is keeping doing the same thing in the same way and expecting different result"* yaani uwendawazimu ni kufanya jambo lilelile kwa njia ileile huku ukitegemea matokeo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafalsafa Albert Einstein anasema:-

*"Problems can not be solved by the same level of thinking that creates them".*

Ndugu zangu, kabla sijawa Mbunge kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Akunaay, nilikuwa nawa-*admire* sana Wabunge wanavyokuwa Bungeni, wakivaa suti, nilikuwa naona hapa ni mahali ambapo tuna *reason*, mahali ambapo tuna *question* na mahali ambapo tunatoka na *solutions* ambazo zinalikabili taifa lakini kwa bahati mbaya nimeona *is the opposite*, binafsi najisikia vibaya sana. Kama taifa tupo hapa, *we are dealing* na *future* ya taifa hili, tunashughulika na mamia ya maskini wa Tanzania, tunashughulika na barabara mbovu za Watanzania, tunashughulika na hospitali mbovu za Watanzania, halafu tunakuja hapa tunaongea mambo ya khanga!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujisoma historia, nchi za Ulaya karne ya 14, Marekani na Ulaya na nchi zilizoendelea, zilikuwa na fikra na mawazo kama tunavyofanya sasa hivi lakini ilipofika karne ya 18, inaitwa *age of enlightenment, reasoning age*, walianza kufikiri, kuhoji na kudadisi. Tunapofika katika karne hii katika Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, tunapojadili bajeti maana yake tunazo changamoto zinazotukabili kama taifa. Badala ya kukaa na kujiuliza kwa nini tupo hapa, tunatokaje hapa tulipo, tunaanza kuongea ngonjera na maneno ya uswahiliuswahili yaani unafiki, woga, kujipendekeza na kutokujadili mambo ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najisikia uchungu sana mamia ya wananchi wametuamini tuje tujadili vitu vya maana hapa lakini tunakubaliana akili ndogo itawale akili kubwa. James Madison mwaka 1822 alisema, “*knowledge forever will govern ignorance*”. Tumekubali Bunge hili *knowledge* ndogo i-govern *knowledge* kubwa, tumekubali *ignorance* i-govern *knowledge*, tunalipeleka wapi taifa? Akichangia *professor* hapa hana tofauti na mtu wa darasa la pili. Huwezi kutofautisha mtu mwenye *masters* na mtu wa darasa la pili, *where are we taking this nation?* Watu wametupa kura, tunapoteza fedha za Watanzania, tumekaa hapa tunaacha kujadili mambo ya msingi kwamba tunawezaje kutoka kwenye matope haya? karne hiyo ya 18 ninayoisema walipoanza kuhoji, walipoanza kudadisi ndipo mapinduzi ya viwanda yalivyojitekeza, *no wonder* watu wanaosema ni wataalamu wa uchumi wametufikisha hapa tulipo, *if that is the case*, haya ndiyo masuala ambayo tunapaswa tuyajadili kama taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inaonyesha hapa, kitabu cha uchumi cha Mheshimiwa Wassira kwamba deni limekuwa shilingi trilioni 20. Ukitawala ni kama karibu kila Mtanzania anadaiwa shilingi laki nne na themanini na zaidi, hata mimba inadaiwa, ndiyo taifa tulipofika hapa sasa hivi. Pia ninashangaa katika mapango wake wa bajeti taifa hili kama tunafuutilia na tunakwenda na takwimu, mdogo wangu amezungumza hapa kwamba tunatumia takwimu za nyuma, unawezaje kupanga mambo na takwimu za nyuma? Leo hii katika taifa hili 44.2% ni watoto walio chini ya miaka 15 maana yake hawa ni *consumers*, wanakula zaidi hawa-produce, wako shulenii na wanao-produce katika nchi hii ni wachache sana kuliko wanaokula ukijumlisha na wazee tuna mzigo mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa utaratibu wa bajeti tulio nao hapa, *there is no way* kama tunaweza tukafanya maendeleo, *it will take ages* kubadilisha taifa hili kama tunaendelea na ngonjera za namna hii na kuruhusu akili

ndogo itawale akili kubwa. Watu wenyewe akili kubwa wanaweka akili zao mfukoni kwa sababu ya ushabiki wa kivyama badala ya kukaa tuka-*discuss* namna ya kutatua matatizo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama wanao-*consume* ni wengi na wanao-*produce* ni wachache maana yake nini? Tutaendelea kuomba fedha nje na kukopa fedha nje ili tuwalishe kwa sababu ni wajibu wa Serikali kusomesha watoto, ni wajibu wa Taifa kuhakikisha watoto wanavaa na kusoma shule nzuri lakini mpango mzima wa uchumi uko kimya, hauzungumzi. Hapa watu wasomi ambao tupo 350 taifa limetuamini tukae hapa tunatakiwa tujihoji, ndiyo maana nimesema *problems can not be solved by the same level of thinking that created them, you guys you are tired!* Kwa sababu hamuwezi kutetea matatizo haya, mmetuweka kwenye mess ninyi wenyewe, ni lazima akili ya juu zaidi iweze kutatua, ni *principle* hii yaani huwezi kubadilisha *that is the principle*, iwe ni mwanamahesabu na nikiunganisha na *insanity is keeping doing the same thing in the same way and expecting different results and this is what we are doing*. Tunafanya hayohayo kila mwaka bajeti ya namna hiyohiyo. Ukienda kwenye elimu ni matatizo, ukienda kwenye kilimo ni matatizo, ukienda kwenye afya ni matatizo mwaka baada ya mwaka ni matatizo yaleyale, *why can't we think a little bit more? We can't stretch our brain a little bit more kama taifa?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na watu wengine ambaao ni ma-*professor* wanasema mara nyingi wakitoa ushauri wa kitaalamu, Serikali hamsikilizi na inawezekana wanakaa watu wachache, wanajifungia halafu wanatoa maamuzi kwa sababu wanajua mambo ni yaleyale, *business as usual*. Ndugu zangu, *where are we going? Where are we heading?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha tena karibu 42% ya watoto wanaozaliwa wanadumaa, *they can not think properly, they can not question, they can not ask*. Ubongo aliotupa Mungu ni lazima uwe *stretched* ili uweze kuchambua kwani tumeumbwa ili tutatue matatizo hapa duniani na siyo tu-*create* matatizo. Tulipokuja hapa Bungeni tunatakiwa tu-*solve problems*, Bunge hili naliomba liwe Bunge la kimapinduzi, tu-*change* namna ya kufikiri na tu-*change* namna ya kufanya vitu na wengine wanapata taabu hapa kwa sababu tumezoea Bunge la chama kimoja. Tuna mfumo na *traditional* ya chama kimoja cha zamani, ulimwengu ume-*change* halafu tunesimama mahali pamoja hatuendi na ulimwengu unavyokwenda. Maendeleo duniani yamekuja kwa kuwa na mawazo tofauti yanayopingana, badala ya kutuzomea mtusikilize, huu ndiyo wajibu wetu. Mimi kama *opposition* siwezi kusifia bali nakukosoa ili ufanye kazi yako vizuri ili na wewe utimize wajibu wako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa deni kama hili kila mwaka linaongezeka halafu tunakaa hapa tunasema Serikali ya CCM itaendelea kutawala, *so what?* Ili iweje? Kwa sababu lengo la Serikali kuwepo ni kutatua matatizo ili tuhakikishe tuna-*improve* maisha ya watu lakini watu kwa sababu wanalinda vyeo, kuna mmoja amesema Mchungaji, lakini nitasema tu hata kama mtasema au kunitoa nje ya Bunge lakini kama ukweli unakosewa / *will speak out* kwa sababu hiyo ndiyo kazi ya Wachungaji vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge mmoja alishauri hapa tuombewe lakini sioni hata *theory* ya uchumi inayosema kama unataka kutatua matatizo ya uchumi eti ufanye maombi, ninashangaa huyu amepata wapi hilo? As a *Theologians* hata Paul anasema asiyefanya kazi na asile siyo aombewe, unamnyima chakula lakini yeye anasema watu waombewe. Mimi kama Mchungaji naombea wazinzi, wanaofumanika na wake za watu, ndiyo tunawaombea, mimi kama Mchungaji tunawaombea wenyе mapepo na hii ni

*principle tuna apply, una-consumers wengi lakini producers wachache maana yake you have to produce more tafuta njia za ku-produce zaidi, we don't pray for this, we don't have to pray for this. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tumekaa hapa tumezalisha taifa la watu waoga, wanafiki na wanajipendekezapendekeza, mimi sijaja hapa kwa kupewa fedha bali wananchi wa Iringa wamenichangua, wananiamini na ninajua wananiunga mkono, wananiwikiliza. Sasa sihitaji kujipendekeza nitaeleza ukweli *as a nation* tupo kwenye matatizo. We *have to address this problems* lakini siyo tunakuja hapa tunaweka ngonjera maneno ya khanga halafu watu mnawapigia makofi, tunalipeleka wapi taifa hili? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajisikia uchungu, naomba niachie hapo. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Chomboh!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii jioni ya leo ili kuchangia mchango wangu katika bajeti hii. Vilevile nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu. Aidha, nawapongeza pia Mawaziri, Waziri wa Fedha na mwenzake waliota hotuba yao juzi na leo tunaijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naanza kwa kuona Bunge letu sasa hivi tunavyoolekea, mimi hiki ni kipindi changu cha pili lakini Wabunge ambao tumeaminika na tuliopewa heshima na wenzetu huko nje kwamba tunaanza kulitumia Bunge badala ya kujadili mambo yenye maslahi tukaanza kujilabu hapa kila mmoja kwa nafasi yake na kwa uwezo wake wa kuweza kuvunja heshima yetu Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchangiaji mmoja asubuhi alisema kwamba nafikiri ni Mheshimiwa ...

**MBUNGE FULANI:** Siyo lazima!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Alisema asubuhi kwamba, Tanzania ni moja kati ya nchi zeny sifa sana huko nchi za nje na ndiyo maana tunapata misaada na kila kitu. Heshima hii haikuja hivihivi, ilikuja kwa maadili na uzoefu ambao wazee wetu walitufundisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu kinakwenda na kinasifika vizuri kwa sababu kila jambo lolote duniani lina maadili yake, sifa zake na miiko yake. Sisi Watanzania ni watu ambao tumefunzwa kwa maadili mazuri. Hiyo ni kawaida. Tuna makabila yasiyopungua 100 hapa, lakini karibu makabila yote maadili na mafunzo yetu sisi ni kuheshimu wakubwa, kuheshimiana na hasa ukiwa mbele za watu kuzungumza jambo ambalo hata likiwa baya lakini kwa lugha ambayo ni ya kufurahisha au ya kuwapongeza wengine jambo likafanikiwa leo tumekiuka mwelekeo huo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu mimi kwa umri wangu nimeona mambo mengi sana, lakini tunakoelekea na kwa wale mnaojulikana au mnajiita ni watu wa kiroho, lugha zinazotumika si za kiroho. Nashauri tubadilishe lugha hizi tuweze kujenga zaidi kuliko kupotosha. Tunaipotosha nchi yetu, tunawapotosha wananchi wetu. Tujitahidi sana kuelekeza nguvu au uelekeo wetu katika kujenga nchi yetu kwa mustakabali wa wananchi waliotutuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ningefurahi sana au ningependa nichangie kidogo kuhusiana na bajeti yetu. Bajeti yetu ni bajeti inayomjali Mtanzania kila alipo na kwa kila hali ilivyo. Chama cha Mapinduzi kina uzoefu mzuri sana. Mkisikia hiyo miaka 50 mnayoizungumza ilianzia na TANU baadaye ikaja Chama cha Mapinduzi (CCM) mpaka hivi

leo ni uzoefu huo uliotufikisha hapa tulipo na ikawa kila mmoja hapa anajinasibu, anazungumza kwa ufasaha mpaka ikafika wakati hadi yeye mwenyewe anajitukana. Kwa sababu unapotukana Chama cha Mapinduzi, si unajitukana mwenyewe? Si ndiyo iliyokufikisha hapo ulipo kielimu, kimaadili na kila kitu? Una uhuru wa kuweza kukosoa lakini jaribu kutumia busara uliyofundishwa na maadili uliyotokana nayo. Ikiwa wewe unazungumza kuikosoa Serikali nje ya maadili, huo sio Utanzania. (*Makofi*)

### **WABUNGE FULANI:** Mmmmh!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Watanzania hatuko hivyo. Mnatutia wasiwasi au ndiyo kwa sababu wengine mnataka kujitenga? Mnataka kuanzisha Jamhuri yenu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka kule Zanzibar. Ngoja niwaambieni kitu kimoja kwanza, kama siyo kweli nisikilizeni nasema nini ndio mtajua. Kwa sababu hili suala lipo, vijana wa sasa hivi mnajitokeza kuuliza kitu ambacho sidhani kama ni misingi ambayo tunatokana nayo. Wanasema kwamba wao Wazanzibari. Wao Wanzanzibari! Kuna watu walikuwa hawajui Zanzibari ni nini. Zanzibari inatokana na neno moja 'Zanji' hilo ni neno la kiarabu linalowiana na *black*, mbantu, *negros*, ndiyo maana yake. Sasa na wale waliojitokeza kule na wa hapa amba wanakuja kuitukana Serikali ya Mapinduzi zamani walikuwa hawataki Muungano, ni kitu kimoja. Kwa sababu na Zanji atakayesema kwamba yeye ni Mzanzibari halafu hataki Muungano *that is nonsense* kwa sababu ikiwa Zanji ni mtu mweusi na kama katoka Zanzibar, mtu mweusi katoka wapi? Ikiwa yeye kachanganya kidogo na yule mweusi maana yake nini? Yeye ni Muungano tayari maana yake kokote aliko na ule weusi uko pale, Muungano anaukataaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nilikuwa nataka kuonesha tu nidhamu ya sasa hivi, vijana tunakwenda wapi? Jaribuni kutazama watu wanakotokea. Unapotaka kukosoa kitu kikosoe kwa mtazamo na kwa maelezo mazuri ya kujenga nchi yetu. Hii nchi ina sifa dunia nzima. Ina sifa kwa misingi iliyotokana na watu wetu huko nje. Tujaribuni kuweka heshima. Hili ni Bunge na siyo kijiwe. Tujitahidini sana tukosoe mambo kwa njia ya busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba sana kuzungumzia suala la ndugu zetu hasa wafanyakazi wa *Tanzania Revenue Authority (TRA)*. *TRA* ni chombo ambacho ninakiamini na ndiyo ambacho tunakitegemea kukusanya kodi. Mjitahidi kupanua wigo wa kodi, lakini pia muwe waadilifu katika kukusanya kodi hiyo ili kusudi ifike katika vyombo vinavyohusika na itumike kizalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja ambacho leo ninataka kukizungumzia kuhusu ndugu zangu wa *TRA*. Katika chombo hiki tunachokitegemea, kuna kesi moja ambayo inahusu wizi wa magari yanayopungua 300 ambayo yalitoka nje wakabadilisha *transfer as if* yanatoka Zanzibar waka- *clear Dar es Salaam* bila kulipiwa ushuru. *Three hundred cars!* Nina mfano wa karatasi hizi hapa. Hapa nina kampuni moja, ninatumia kampuni hewa. Kampuni nyingine wamezisajili na wakashirikiana na watu wa *TRA*, gari hizi zimetolewa bila ushuru. *TRA* mnakwenda wapi? Wizi umetendeka na ushahidi wa makaratasi ninao. Fedha hizi ndizo tunazozitegemea na kodi hii ndiyo tunaitegemea kwa ajili ya kuweza kuendesha nchi yetu na kuondoa umaskini ambao tunauzungumza, tunauimba kila siku. *TRA* jitahidini kufanya uadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tunahitaji pia kubadilika hasa watendaji. Watendaji tumekuwa wavivu sana wa kufanya kazi. Tumeweke starehe mbele. Tunafanya starehe zetu *throughout the week*. Wiki nzima watu hawataki kufanya kazi. Tunatakiwa tunabadirishie *mind set* zetu sasa hivi tufanye

kazi, tuache kulaumiana tu, tufanye kazi. Hii siyo kazi ya Waziri. Hii ni kazi ya kila mmoja katika sehemu yake. Tunatumia muda mwingi sana Watanzania sasa hivi kwa starehe na kulaumu. Muda wote tuko kwenye starehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kitu kimoja Serikali inaweza kukizungumzia kwamba, hii ya kutegemea kodi ya pombe tunaona kama ni jambo la maana sana. Hii kodi ndiyo maana tunafanya Watanzania wawe walevi sana kwa sababu kila siku tunakusanya kodi. Hii tuache, tafuteni njia nyingine kwa sababu kuanzia saa nane, saa tisa, kuna baa za ndani mpaka barabarani watu wanalewa *through out the week*. Hatuwezi kufika, lazima tufanye kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania, vijana tumekuwa sasa hatuna kazi nyingine ya kufanya, sisi ni starehe tu kuanzia Jumatatu mpaka Jumapili. Leo ukumbi huu, kesho ukumbi ule. Lazima tubadilike tujue wakati wa kufanya kazi, tubadilishie *mind set* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi lakini kimsingi nipongeze mabadiliko ya Baraza la Mawaziri. Wote tunawapongeza. Tunaamini kabisa kazi zitafanyika vizuri na ninaamini na wewe Mwenyekiti jirani yangu hapa kazi utaifanya vizuri. Tuna ku-*miss* hapa lakini tunakuona hapo ulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema hotuba ya Mheshimiwa Waziri imekuwa nzuri sana, lakini nitajikita katika maeneo machache kwa sababu ya muda. Kwanza kuna hayo aliyojasema kwamba ni msingi na shabaha ya bajeti yenye. Yako maeneo sita (6) ambayo ameyataja. Katika hayo sita, mimi nitajikita katika moja tu, hili la kupunguza makali ya maisha. Pale amezungumzia maeneo makubwa mawili; ametoa mfano kwamba tumezalisha umeme zaidi MW 234,

imetusaidia kuchangia kupunguza hali ya maisha. Mimi nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, kama kuna eneo limetuletea matatizo katika nchi hii ni sekta hii ya umeme wa kukodisha. Hizo *MW* anazozizungumzia ni ambazo sehemu kubwa zimezalishwa na kampuni inayoitwa *IPTL*. Kampuni hii ya *IPTL* wanatuzamisha na wanatukandamiza. Nilikuwa mmoja kati ya wajumbe wale wa Kamati ya Richmond, lakini ripoti ya Richmond siyo ya wajumbe, baada ya kujadiliwa Bungeni ni ripoti ya Bunge. Katika maeneo ambayo kweli kuna mikataba mibaya ni *IPTL*. *TANESCO* wanabeba mizigo mikubwa *IPTL*. Gharama hizo zinatumiza na hazisaidii kubadilisha hali yetu ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la pili katika eneo hilohilo ambalo pia umelizungumzia, ningependa pia nitoe ushauri wangu. Hilo ni eneo la ununuzi wa mafuta kwa ajili ya nchi hii kwa utaratibu wa kununua kwa pamoja (*bulk procurement*). Katika kipindi kilichopita, tulishauriana hapahapa Bungeni, nilisema na wenzangu wakaniunga mkono kwamba, kama hatutatoa fedha za kuhakikisha mpango huo unatekelezwa, huu mpango hautatusaidia. Leo tujiulize fedha kwa ajili ya *bulk procurement* zimetolewa kiasi gani? Je, zina uhakika wa utekelezaji kwamba ni endelevu na mpango huo utaisaidia nchi? Mafuta ambayo pengine kama kweli yamekuja, je, yamesaidia kupunguza gharama za bei ya mafuta hapa nchini kama tulivyo kuwa tumetarajia? Napenda kuwahakikisha kwamba fedha hazikutolewa za kutosha na kwa hiyo, mpango huo ambao kwa kweli ni mzuri lazima tuufanyie kazi uweze kusaidia taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotaka kusaidia kuchangia hotuba ya bajeti lazima pia uje na mapendekezo yatakayosaidia angalau kuongeza kipato cha Taifa. Ningombaa kuelekea katika maeneo mawili; wenzangu wamezungumzia sana bodaboda. Mimi naomba niwakumbushe na kulipongeza Bunge hili kwa kupitisha Sheria ya kukubali hizi pikipiki, bodaboda kuwa ni chombo cha

biashara. Kama tusingepitisha, leo ajira hiyo ambayo kwa uhakika tunayo kwa waendeshaji wa pikipiki isingekuwepo. Mimi nachukulia mfano pikipiki zaidi ya 25,000 sasa zipo barabarani. Ni zaidi ya hizo lakini mimi nazungumzia 25,000 tu. Sasa idadi hiyo ya pikipiki baadhi ni madereva na siyo wanaozimiliki. Sina tatizo lolote kwa sababu sheria ya kodi ya mapato hapa iko wazi na inasema wale ambao kipato chao ni chini ya shilingi 3,600,000 kwa mwaka hawatalipa kodi. Kwa hiyo, wale wanaoendesha pikipiki kwa uhakika hawastahili kabisa kulipa kodi ya mapato lakini wale wanaomiliki, zile shilingi 10,000 kwa siku wana shilingi 300,000 kwa mwezi na kwa mwaka wana shilingi 3,600,000. Kwa sheria hii hao wanaomiliki wanapaswa kulipa kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mabadiliko haya tuliyoyafanya hapa kodi watakazolipa kwa mwaka ni shilingi 100,000 tu kwa mwaka mzima. Unapata shilingi 300,000 kwa mwezi na shilingi 3,600,000 kwa mwaka, kwa nini usichangie taifa lako kwa shilingi 100,000 tu? Mahitaji ya taifa ni mengi na makubwa, tunahitaji kuboresha sekta za afya, barabara hizo tunazotumia na bodaboda. Fedha zitatoka wapi kama sisi wote tutasema hatulipi kodi na tusilipe kodi? Ukichukua idadi ya hizo pikipiki nilizoisema kwa shilingi 100,000 tu kwa mwaka kwa pikipiki 25,000 basi fedha itakayopatikana ni zaidi ya shilingi bilioni 2.5. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu na hili nililisema miaka michache iliyopita nilipokuwa nikitoa mapendekezo ya mpango huu wa kodi ya mapato ambao ndiyo unaotumika leo. Nilzungumzia ada ya leseni za biashara ili tuweze kuwafanya wafanyabiashara ndogondogo wajitambulish. Leo ninataka nikuhakikishie kwamba wamejitambulisha. Hebu kaangalie ni vibanda vingapi vya biashara vimejengwa. Hata katika baadhi ya nyumba zetu tumeweka hayo maduka ya biashara, mengi tu. Kwa nchi nzima hayapungui 500,000. Sasa katika wafanyabiashara hao, yapo makundi ambayo yameanzisha biashara hizo lakini

mapato yao hayazidi shilingi 3,600,000. Hawa hawapaswi kulipa kodi, lakini wale wenye biashara zinazozidi kiwango hicho wanapaswa kulipa kodi. Kiwango cha chini ambacho tumekiona hapa ni shilingi 100,000. Je, kama wako 500,000 wakilipa shilingi 100,000 kwa mwaka ni shilingi ngapi hizo zitaongeza mapato yetu? Hizo ni zaidi ya shilingi bilioni 50. Ni lazima Mheshimiwa Waziri atuambie je, *TRA* wana mchakato wa uhakika wa kukusanya hizo fedha nilizozitaja shilingi bilioni 50 kwa mpango huo ambao tuna uhakika utaongeza mapato ya Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuangalie sekta ya utalii. Sasa hivi watalii wengi wameondoka katika sekta ile ya utalii wa kwenda kuangalia wanyama wa porini wanakwenda sasa katika maeneo ya bahari (*marine areas*). Kwa hiyo, lazima tuboreshe *marine parks*. Huko ndiko sasa biashara ya utalii iko na itasaidia sana kukuza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie pia unaposema unataka bajeti isipite *implications* zake kubwa ziko tatu. Kwanza ni aidha kufanya marekebisho katika bajeti iliyopo, pili ni kuipitisha kama ilivyo na ya tatu inaweza ikasaidia kkuondoa na tunayoizungumza hapa ni Bunge. Bunge ni mhimili, tusipopitisha bajeti mhimili huu unaweza ukaondoka kutokana na hilo. Lakini nimetazama hata katika bajeti ya wenzetu wa Upinzani ambao wao dhamira ni hiyo ya kutopitisha bajeti. Sasa nikatazama katika bajeti kama kweli dhamira yao ndiyo hiyo je, wameweka fungu la kufanya kazi ifuatayo? Mhimili huo ukiondoka ni lazima twende kwenye uchaguzi, je, garama za uchaguzi mpya zimebekwa? Mimi sikuziona huku. Vilevile unapoondoa mhimili huu unaondoa pia kazi za mhimili wa pili, Serikali. Unaondoa pia kazi za mhimili wa tatu ambao ni Mahakama kwa sababu hakutakuwa na fedha za kuendesha Serikali wala Mahakama. Je, tumetenge fedha za kusaidia katika kipindi cha mpito kuwezesha mihimili hiyo miwili kufanya kazi? Mimi sijazona humu. Kwa hiyo, sidhani kama dhamira ndiyo hiyo. Dhamira ni kutaka upande wa pili

usaidie kuchangia kufanya kazi ya kupitisha bajeti lakini wao waonekane kwamba walikuwa hawataki bajeti ipite. Kwa hiyo, lazima tuangalie hizo *implications* za bajeti ambazo zinaweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie la mwisho. Ukitazama mpango wa barabara ulivyo kwa nchi nzima, Kamati yetu imepita tumeangalia, tuna mzunguko wa kitaifa kama Taifa kuanzia Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Ningetaja vituo vyote kutoka Tanga tunaanzia Horohoro - Tanga, Bagamoyo - Dar es Salaam, Somanga ndiyo panatutia aibu kwenda pale mbele kilomita 60, lakini utakwenda mpaka Mbeya, utatoka Mbeya utakwenda Masasi - Songea- Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Kibaoni - Kigoma na huko utafika Kagera - Mwanza - Musoma...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru *donors* wawili waliko Uingereza bwana Damian Ursin na Amos George *of Aspno Foundation* ya Wanyama ambao wame-donate *black rhinos* watatu (3) kwa Tanzania na wamepelekwa Hifadhi ya Mkomazi ambayo iko Mkoa wa Kilimanjaro. Najua Serikali kwa upande wake imeshukuru, lakini na mimi kama mdau wa utalii Mkoani Kilimanjaro, naomba niwashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa kuileta bajeti hii. Hii bajeti inatekelezeka kama tutafuatilia vizuri yale ambayo tumeandaa kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea idara tatu; utalii na mazingira, viwanda na Kilimo. Nikianza na utalii na mazingira, mapato ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ni asilimia 38 ya mapato ya *TANAPA*. Kila mwaka hifadhi ya Mlima Kilimanjaro inapata shilingi bilioni 80 (US\$ 50 milioni) kutokana na watalii wanaopanda mlima ule. Nimelisema hilo ili niendelee kusema kwamba, ile hifadhi inahitaji kutunzwa kwa kuzuia watu kukata miti, kulinda vile vyanzo vya maji, kupanda miti mipya, kuzuia watu kuchoma moto na yote hayo yanahitaji fedha lakini naona kwenye bajeti kuna kiasi cha shilingi bilioni tano (5) kwa ajili ya mazingira na hii fedha haijulikani kama ni kwa ajili ya Mlima Kilimanjaro tu au ni hifadhi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *TANAPA* na *KINAPA* kufanya vizuri kutunza hifadhi ya mlima, lakini bado kuna Halmashauri za Wilaya zinazozunguka mlima ule lakini na uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro, nimshukuru sana Mheshimiwa Gama amekuwa anafanya kila *effort* kuhakikisha kwamba miti inapandwa mingi kwa ajili ya kulinda hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iweke mkakati kwamba ni namna gani hifadhi hii inaendelea kulindwa kwa sababu ni chanzo kikubwa sana cha pato la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo basi nimeona kwenye mpango wa Serikali kwamba bomba la gesi litatoka Mtwara linaishia Tanga. Naomba niishauri Serikali kwamba bomba hili liishie Arusha, kwa sababu hata Arusha kuna pato kubwa sana la utalii, wale watu wakipata gesi wataacha kukata miti. Sasa Mkoa wa Kilimanjaro *square meter* moja inakaliwa na watu 126, ni Mkoa ambao uko *highly density populated* wa tatu baada ya Dar es Salaam na Mwanza lakini hawa watu wengi wako kule mlimani na wanapunguza lile eneo la hifadhi kwa kulima kidogo kidogo baadaye

wanawasha moto unachoma hifadhi, unafukuza wanyama lakini unaondoa na uoto wa asili. Naomba niishauri Serikali kwamba miaka ya 1970 Mwalimu Nyerere aliweza kuwaondoa watu kwenye vyanzo vya maji na kwenye Mlima Kilimanjaro kule karibu kabisa na *Crater* akawapeleka kwenye maeneo mengine ya kilimo kama Kilombero, kwa hiyo ningeishauri Serikali iliangalie hili kwa ajili ya kutunza hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende katika viwanda. Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria Na.19 ya mwaka 2010 kwa ajili ya *PPP*. *PPP* imeletwa tena kwenye bajeti ya sasa hivi. Mimi niseme, naishukuru sana Serikali kwamba imeona umuhimu sasa wa kuweka mkakati wa kuruhusu Halmashauri za Wilaya ziweze kushirikiana na watu binafsi kwa ajili ya kuleta maendeleo. Naomba nishauri basi Serikali ifanye haraka mpango huu lakini na huko kwenye maeneo kwa sababu kila eneo kuna mazao ambayo ni mengi kwa mfano kuna maeneo ambayo yana mahindi mengi inawezekana viwanda vikaanza, mashine zikawekwa za kukoboa mahindi, zikasaga na kuuza unga, lakini kuna maeneo yana mpunga mwingi, kuna maeneo yana matunda mengi yakatengeneza *concentrates* na *juice*, kuna maeneo yana ndizi nyingi yakatengeneza mvinyo haya yote yataongeza thamani kwenye mazao ambayo yatakuwa yanatengenezwa na wakulima na watakapokuwa wanauzwa mazao yao liko soko la Afrika Mashariki ambalo ni kubwa ambalo najua kabisa watakuwa hawana hasara. Naomba niiombe Serikali iweke mkakati wa kuharakisha huu mpango wa *Public Private Partnership* kwa ajili ya wananchi wa Tanzania waweze kupata ajira kwenye yale maeneo ambayo viwanda vinaweza kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine pia kwa sababu viwanda vidogovidogo vitaleta ajira nyingi, mimi ningedhani pia kwa viwanda vyetu hasa vile vinavyotengeneza nguo ambavyo tayari vingine vinafanya kazi hiyo ingeangaliwa kupunguziwa kodi kidogo ili waweze kushindana na nguo zinazoletwa kutoka

nje ya nchi. Yako Mashirika au viwanda ambavyo vilitaifishwa na Serikali na havifanyi kazi. Naishauri Serikali mikataba ile ifutwe ili viwanda hivi viweze kukabidhiwa Halmashauri na Halmashauri iweze kuviingiza kwenye ubia. *SIDO* inaweza ikaendelea kuwezeshwa kwa ajili ya kutengeneza mashine ndogondogo ambazo zitasaidia viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kilimo, asilimia 80 ya wakulima wanatumia zana duni, wachache wanatumia *power tillers*, wachache wanatumia majembe ya kukokotwa na jembe. Bajeti ya shilingi bilioni 191.2 ukilinganisha na idadi ya wakulima na eneo la hekta milioni 5.1 inayolimwa, ni fedha kidogo. Wazo la Serikali kuajiri Maafisa Ugani 5,000 ni wazo zuri sana na naipongeza Serikali kwa hilo lakini ningeomba Serikali tuweke mkakati kwenye kukarabati mabwawa yale ambayo tayari tunayo, kwenye kukarabati *irrigations schemes* ambazo tayari tunazo, kwenye kukarabati malambo ambayo tayari yapo hatuna haja ya kutengeneza mabwawa mapya wakati ya zamani yapo ili kila mahali wapate maji na waweze kuendelea na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Kaskazini, Kilimanjaro, Arusha na Manyara takriban miaka mitatu sasa imekumbwa na mabadiliko ya tabianchi na ukame wa hali ya juu. Sio rahisi sana kuendelea kupata tu chakula cha msaada, kwa hiyo naomba Idara ya Kilimo, Serikali ije na mpango tofauti au mpango mbadala pengine kufanya *drip irrigation* inaweza ikasidia. Tumesema kuna bonde la Malagarasi na la Kilombero ambayo yanafaa kwa kilimo lakini mabonde hayo tayari mifugo imevamia. Kwa hiyo, naomba Serikali pia ije na mkakati wa kuangalia *movement* ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema, naomba kodi ambayo imeondolewa kwenye *crude edible oil* iondolewe kwa wakulima kwa sababu wakulima wa alizeti watashindwa kuza alizeti na watakuwa *discourage* hata

kulima hiyo alizeti yenye. Tukumbuke kwamba pale ambapo panaota mahindi panaota pia alizeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nijielekeze katika Mpango wa Maendeleo. Tulipoanzisha Mpango bila shaka ilikuwa ni dira ambayo tumekubaliana kama Taifa itatuondoa mahali tulipo hivi sasa na kutupeleka mbele zaidi na ndiyo maana Serikali ikasema hivi katika Mpango huu. Mpango huu ni kipimo cha ufanisi wa Serikali na uchumi kwa ujumla. Sasa kama Mpango huu tulikubaliana kwamba utakuwa ni kipimo cha ufanisi wa Serikali na uchumi, hebu tuangalie basi namna ambavyo Serikali inajitathmini na kujipima katika utekelezaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango uliainisha ili uweze kutekelezeka kila mwaka zitatengwa shilingi trilioni 8.6. Huu ni mwaka wa pili wa utekelezaji wa mpango. Mwaka wa kwanza wa utekelezaji badala ya kuchangia shilingi trillioni 8.6 kama Mpango ulivyosema na kama Bunge lillyoridhia mwaka huo zilitengwa shilingi trillioni 4.9 tu. Mwaka wa kwanza kabisa wa Mpango tukaanza kwa kuuvunja Mpango na kwa kuunja Azimio lenyewe la Bunge. Mpango pia ulisema zitatengwa asilimia 35 ya mapato ya ndani kwa ajili ya shughuli za maendeleo na asilimia 65 zitakuwa kwa ajili ya matumizi mengine. Mwaka wa kwanza wa utekelezaji zilitengwa shilingi trillioni 1.87 sawa na asilimia 26.2 tu ya mapato ya ndani kwa shughuli za maendeleo na hii ilikuwa ni kinyume kabisa na Mpango wa Taifa wa Maendeleo. Tuliambiwa mwaka uliopita ulikuwa ni mpito kwa hiyo tukasubiri utekelezaji uanze rasmi mwaka huu. Cha kushangaza mwaka huu tumekuja na

kiwango pungufu kuliko kile kilichokuwa kipindi cha mpito. Zimetengwa shilingi trilioni 4.5 tu kwa ajili ya shughuli za maendeleo na shilingi trilioni 2.2 ni mapato ya ndani na ni sawa na asilimia 24.4 tu na sio asilimia 35 kama mpango ulivyoainisha. Sasa ikiwa huu ndio utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo na ikiwa Serikali ilisema Mpango huu utakuwa ni kipimo cha ufanisi wa Serikali na uchumi je, ni kweli tunatekeleza kile ambacho tulikubaliana je, kuna ufanisi wowote?

## TAARIFA

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelazimika kutoa taarifa kwa sababu ya upotoshaji mkubwa ambao unashindikana kuvumilia. Msemaji aliyetoka kuongea muda huu anasema kwamba mpango umesema shilingi trilioni 8.6 zitakuwa zinatengwa kila mwaka na Serikali imekuja na shilingi trilioni 4.5, huu ni upotoshaji. Mpango unasema hivi, bajeti itakayokuwa inatumika ni shilingi trilioni 8.6 kati ya hizo shilingi trilioni 8.6 Serikali inatakiwa kutenga shilingi trilioni 2.7 tu zingine ni za *PPP*. Hivi nitawafundisha mpaka lini akina Lissu, nimemfundisha jana kaka yake leo dada yake. Asome kwenye utangulizi tu wa mpango ndivyo unavyosema. (*Makofii*)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayoisema ni sahihi na mimi ni Mchumi, darasa alilolisoma Mheshimiwa Nchemba na mimi nimesoma na nimefundishwa na Walimu walewale waliomfundisha Mheshimiwa Nchemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo hauko sawasawa na umevunjwa na Serikali na ndiyo maana sisi tulisema hii bajeti irudi ili itekeleze Mpango wa Taifa wa Maendeleo ikiwa kweli tunataka kuondoka hapa tulipo na kuelekea mbele kwenye maendeleo kwa manufaa ya wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la mfumuko wa bei. Hadi kufikia Desemba mwaka 2011, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 19.8 lakini chakula kilichangia kwa asilimia 24.7. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa ni tatizo lakini Serikali mwaka jana ilisema inatoa misamaha ya ushuru na tani laki mbili za sukari ziliingizwa nchini ili kukabili mfumuko wa bei lakini mwaka huo ambapo tani laki mbili ziliingizwa kutokana na msamaha wa ushuru badala ya sukari kushuka bei ilipanda kutoka shilingi 1,700/= kwa kilo hadi shilingi 2,800 katika baadhi ya maeneo. Mimi nilidhani Serikali safari hii itakuja na wazo mbadala baada ya kuona kwamba lile wazo la kutoa ushuru halikufanikiwa lakini bajeti ya Mheshimiwa Waziri safari hii inakuja na *solution* hiyo hiyo inasema, hatua za haraka ambazo Serikali itachukua ni pamoja na kutoa vibali vya uagizaji wa sukari na mchele kutoka nje. Hivi ndivyo ilivyofanya mwaka jana lakini bei ziliendelea kupanda. Sasa ndio maana sisi Kambi ya Upinzani tunasema hivi, matatizo yaleyale tuliyonayo siku zote yaliyosababishwa na watu walewale ni kweli yatatatuliwa kwa majawabu yaleyale, kwa nini Serikali haileti suluhisho tofauti? Kwa hiyo, kwa mkakati ambao Serikali inauleta wa kupunguza mfumuko wa bei ni dhahiri wananchi wa Tanzania wataendelea kuumia na kushindwa kuhimili ugumu wa maisha na wataendelea sasa kama wanakula mlo mmoja kwa siku hata huo mlo mmoja na wenyewe utaanza kuwa wa taabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la uchukuzi. Bajeti ya uchukuzi ina takribani shilingi triliioni 1.38, lakini kati ya hizo shilingi triliioni 1 ziko katika Wizara ya Ujenzi. Wizara ya Uchukuzi ambayo ndiyo inahusisha reli, bandari, viwanja vya ndege imeachiwa shilingi bilioni 880 na kitu hivi na siku zote tumekaa kwenye vikao tukakubaliana kwamba uchumi unaweza ukahamishwa hapa ulipo na kwenda mbele zaidi kwa kutumia usafiri wa reli lakini leo tunakuja na bajeti ya uchukuzi ambayo ina reli, bandari, viwanja vya ndege shilingi bilioni 388 na barabara au ujenzi ikatengewa shilingi triliioni moja. Najiuliza Baraza la Mawaziri wanapokaa wanaangalia

vipaumbele vya taifa au ni umahiri wa Waziri anayehusika anavyoweza kuli-*convince* Baraza la Mawaziri na akatengewa fedha nyingi zaidi, hebu tuangalie vipaumbele. Mizigo yetu ambayo inakuza uchumi itaweza kuhamishwa na barabara au na reli. Nashawishika kwamba inawezekana kuna watu ambao wananaufaika na usafiri wa barabara na ndio maana hazichukuliwi jitihada za dhati za kuhakikisha kwamba reli zetu zinaimarishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la matumizi ya anasa ya Serikali. Tumekuwa tukiongelea suala la magari ya kifahari katika Utumishi wa Umma. Mimi nilipata faraja wakati fulani nimesikia Mheshimiwa Waziri Mkuu amekataa gari la kifahari, lakini je Mheshimiwa Waziri Mkuu unapokataa wewe gari la kifahari wakati kuanzia chini yako na watu wengine wote unaona wanatumia magari hayo, je, huo ni utendaji sahihi? Je, Serikali ina utaratibu gani, ni viongozi wa kada gani ndio wanaruhusiwa kutumia magari gani na wanapewa na madereva? Kwa sababu utakuta Afisa Mwandamizi ana gari, ana dereva, Mkurugenzi ana gari ana dereva na kadhalika mpaka juu, hivi hakuna utaratibu wa nani awe na gari na nani awe na dereva. Haya ni matumizi makubwa ambayo nayo ni lazima yadhibitiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la mwisho, changamoto za *millennium*. Napenda kuzungumzia suala la afya, tunajua wote kwamba ugonjwa wa malaria ndio unaosumbua sana hapa nchini lakini jitihada zinazochukuliwa maana Serikali wanasema kwamba watu wanahamasishwa kutumia vyandarua, nikiangalia sehemu kubwa ya wananchi walioko vijijini hivi vyandarua vinafungwa wapi, mbona hamna hata hivyo vitanda vya kufungwa vyandarua? Kule kwetu Singida tunalalia ngozi, sasa sijui hiyo chandarua itafungwa wapi? Halafu tunapohamasishwa kununua vyandarua vyenye dawa hivyo vyandarua vyenye dawa vinauzwa maduka yapi, mimi sijui maduka hayo maana najua vyandarua vya kawaida ndio vinauzwa, hivi hivyo tunavyoambiwa vina dawa viko

katika maduka yapi hasa na wananchi wanajua vilipo hivyo vyandarua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho lingine tunajua kwamba tunaweza tukapambana na malaria kwa kuangamiza mazalia ya mbu lakini sisi tunakuja na suluhisho la kutumia chandarua, hivi kweli tuna mkakati wa dhati wa kupunguza malaria au tunalinda wenyewe viwanda vyatya vyandarua na wenyewe viwanda vyatya madawa ya malaria? Kwa hiyo, naiomba Serikali wakati wanassema wanajiandaa kujenga kiwanda pale Kibaha cha kuzalisha madawa ya kuua mazalia ya mbu, kwa nini tusianze kwa kununua hizo dawa wakati kiwanda kinajengwa? Kwa nini hapa katika malaria tunasubiri tutatue tatizo hilo kwa kuanzisha kiwanda ilihali dawa zingine zote zinanunuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi jirani ya Kenya wameruhusu matumizi ya dawa ya *DDT* ambayo hata hapa ilikuwa inatumiwa zamani. Hivi ni kweli Tanzania tu ndio tuliona *DDT* haifai? Utafiti ulionyeshaje kwamba wenzetu wanaweza wakaitumia kwa makini na ikafaa na sisi kwa Tanzania tukaona ina madhara na mbona miaka ya nyuma ilikuwa inatumika na madhara yake yalikuwa ni kwa kiasi gani kuliko sasa ambavyo wananchi wengi wanakufa kwa malaria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na siungi mkono bajeti ya Serikali. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nami nachukua nafasi hii kuwashukuru wote waliochangia na natoa taarifa ya wachangiaji wa kesho ili wajiandae. Wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Salvatory Naluyaga Machemli na Mheshimiwa Albert Obama.

Naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatano,  
Tarehe 20 Juni, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*